**12 APRILI, 2023**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Tano – Tarehe 12 Aprili, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. David M. Kihenzile) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):**

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

1. Toleo Na. 05 la tarehe 03 Februari, 2023;
2. Toleo Na. 06 la tarehe 10 Februari, 2023;
3. Toleo Na. 07 la tarehe 17 Februari, 2023;
4. Toleo Na. 08 la tarehe 24 Februari, 2023;

5. Toleo Na. 09 la tarehe 03 Machi, 2023;
6. Toleo Na. 10 la tarehe 10 Machi, 2023;
7. Toleo Na. 11 la tarehe 17 Machi, 2023;
8. Toleo Na. 12 la tarehe 24 Machi, 2023; na
9. Toleo Na. 13 la tarehe 31 Machi, 2023.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na maswali, na moja kwa moja tutaanza na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Namwita Mheshimiwa Martha Festo Mariki, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake.

Na. 56

### Uhitaji wa watumishi katika Mkoa wa Katavi

**MHE. MARTHA F. MARIKI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto ya upungufu wa Watumishi katika Mkoa wa Katavi?

**MWENYEKITI:** Haya. Naibu Waziri, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala

Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Mariki, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Katavi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutatua changamoto ya upungufu wa watumishi wa Mkoa wa Katavi kila mwaka kwa kuendelea kutenga Ikama na Bajeti kama inavyopitishwa na Bunge lako. Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Serikali ilitenga nafasi 522 za kada mbalimbali kwa Mkoa wa Katavi na katika mwaka wa fedha ujao (2023/2024) tunakusudia kutenga Ikama ya ajira mpya 914 kwa Mkoa wa Katavi iwapo Bunge lako likiridhia na kuipitisha Bajeti ya Serikali iliyopendekezwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Swali la nyongeza, Mheshimiwa Martha Mariki.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu ya Serikali, lakini katika Mkoa wetu wa Katavi changamoto bado ni kubwa sana. Serikali imewekeza fedha nyingi sana katika vituo vya afya pamoja na Hospitali za Wilaya, lakini hospitali hizo zinashindwa kufanya kazi kama hadhi ya Hospitali ya Wilaya na badala yake kufanya kazi kama zahanati kutokana na upungufu mkubwa sana wa watumishi katika hospitali zetu za Wilaya za Mkoa wa Katavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka nijue, zipi hatua za haraka za Serikali kuhakikisha kwamba wananchi wa Mkoa wa Katavi wanaweza kupata watumishi ili waweze kupata huduma zilizo bora? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Martha Mariki kwa swali lako la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza Mheshimiwa Martha Mariki, Mbunge wa Katavi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali inatambua upungufu uliopo katika hospitali ndani ya Mkoa wa Katavi, lakini katika kupitia utaratibu ambao Serikali imeuweka kupitia mifumo ambayo tumeianzisha ndani ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma, ambapo mojawapo ni pamoja na *HR Assessment System,* tumeweza kugundua hilo tatizo. Pia kwa kupitia mifumo ya upangaji wafanyakazi, tumeshaliona jambo hilo na ndiyo tumeahidi kupitia bajeti hii inayokuja ambayo tutawasilisha mbele ya Bunge lako hapa, kwamba hilo jambo la upungufu wa watumishi katika Mkoa wa Katavi nalo pia ni moja kati ya jambo tunalokwenda kulishughulikia.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Selemani Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa watumishi wengi wanaojitolea wamefanya kazi ya ziada, na kila mara ajira zinapotoka hawa wanaojitolea huwa hawapewi nafasi ya kupewa ajira: Je, Serikali mna mpango gani wa kuwasaidia wale wanaojitolea katika nafasi za Ualimu na Unesi waweze kupewa nafasi hizo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Kakoso, Mbunge wa Tanganyika, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anayoyasema kwamba kumekuwa na watu wanaojitolea lakini wakati mwingine inapotokea ajira zimefunguliwa wanapata matatizo. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mwongozo wa ajira katika nchi yetu unataka ajira zote ziwe katika ushindani. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama watafuata taratibu zilizowekwa, hatuna tatizo katika jambo hilo.

Mheshimwia Mwenyekiti, ni kweli kwamba tatizo la upungufu wa walimu na kada nyinginezo katika utumishi wa umma ni jambo ambalo tunalijua na Serikali imeendelea kulishughulikia jambo hilo. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kufanya hivyo kama ambavyo tumeahidi na katika bajeti yetu tunakuja kusoma hapa hivi karibuni ya mwaka 2023/2024, majibu yote atayapata.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Katika Halmashauri ya Lushoto yenye shule za msingi 180, ina uhaba wa walimu takribani 1,400, hali inayosababisha sasa angalau wastani wa shule moja kuwa na walimu wanne tu: Je, Serikali ina mpango gani mahususi wa kuhakikisha kwamba inakwenda kuboresha ikama katika Halmashauri ya Lushoto? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza lililoulizwa na Mheshimiwa Rashid Shangazi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba upungufu upo kama nilivyokiri katika jibu la msingi, lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo la ikama la mahitaji ya walimu au madaktari au kada zozote katika maeneo yetu linaanza kwenye mchakato ndani ya Halmashauri zetu. Kwa hiyo, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Halmashauri yake ya Lushoto ilete mahitaji hayo, nasi kama Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, tutalichukua jambo hili na kwenda kulifanyia kazi na tutakapopata kibali cha ajira, basi tutahakikisha kwamba tunampelekea wafanyakazi kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge anahitaji.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Utumishi na Utawala na Bora. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, namwita Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda, aweze kuuliza swali lake.

Na. 57

**Ujenzi wa barabara ya Masasi – Nachingwea**

**MHE. CECIL D. MWAMBE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Masasi – Nachingwea kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Eng. Kasekenya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE),** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Waziri Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Masasi – Nachingwea yenye urefu wa kilometa 45 ni sehemu ya barabara ya Masasi – Nachingwea – Liwale yenye urefu wa kilometa 175 ambayo ipo katika hatua ya Manunuzi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa kutumia utaratibu wa *EPC+F*. Uchambuzi wa zabuni upande wa *technical* umekamilika na sasa unafuata uchambuzi wa *financial* ambao utafanywa na Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza kabisa majibu ya Serikali, swali langu lilisema ni lini? Sasa Serikali wanasema wapo kwenye hatua za kukamilisha utaratibu wa *financial*. Sasa nataka kufahamu, huu utaratibu wa *financial* utakamilika lini ili kuweza kutoa pesa kwa ajili ya kujenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami kwa sababu Wilaya ya Nachingwea na Wilaya ya Masasi na Wilaya nyingine pale hazijaunganishwa kwa muda mrefu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kuna barabara ambayo pia inaendelea kujengwa kwenye eneo hilo hilo kati ya Nanganga – Ruangwa, inaunganisha hizo Wilaya mbili, lakini jengo la Chama cha Mapinduzi, Ofisi ya Kijiji, Msikiti pamoja na majengo ya wananchi mbalimbali yalivunjwa sawa sawa na hii barabara ninayoisema ya Nachingwea – Masasi: Ni lini Serikali italipa fidia kwa watu hawa waliopata athari za kuvunjiwa majengo yao kwa sababu ya ujenzi wa barabara? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Cecil.

Mheshimiwa Naibu Waziri, hilo swali la kwanza ambalo ameuliza Mheshimiwa Mbunge, hebu toa maelezo ambayo

Wabunge wote wataweza kuyaelewa vizuri. Kwa sababu tunafahamu kuna barabara saba zikiwemo za Mufindi ambazo zilikuwa zimepitishwa kwenye Mfumo wa *EPC + F*, mpaka leo tunaambiwa majibu yanatolewa nusu nusu ikiwemo Mafinga – Mgororo, kwamba ipo kwenye *technical,* imeamalizika kwenye *financial*. Anataka kujua lini jambo hili litakamilika? Kama majibu pengine hayajitoshelezi, hebu mje na majibu hapa Bungeni mwaambie wananchi kwa sababu muda unazidi kwenda.

Karibu Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mbunge wa Ndanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na suala la kwanza ambalo pia umetaka nitoe maelezo kwa Waheshimiwa wote. Ni kweli tuna barabara nane ambazo zimeingizwa kwenye mpango wa *EPC + F*. Katika barabara nane, barabara itakwenda kwa Mpango wa *PPP* ambayo ni barabara ya Kibaha - Chalinze hadi Morogoro. Hiyo itaingia kwenye *PPP* na barabara zilizobaki hizo saba ambazo ni pamoja na hii niliyoisoma ya Masasi – Nachingwea hadi Liwale zimeingizwa kwenye Mpango wa *EPC + F*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu ni mfumo ambao ni mpya ambapo wakandarasi wanatafuta fedha, wanajenga, halafu Serikali inatafuta utaratibu wa namna ya kuja kuwalipa kwa makubaliano ambayo yatakuwepo. Sasa kuna sehemu mbili; kuna sehemu ya *Engineering* ambayo ni Wizara ya Ujenzi wanakwenda na wakandarasi wanaangalia, wana-*bid,* wanaagalia kwa upande wa ufundi na kuona kwamba wamekubaliana, halafu baada ya hapo sasa, wanapeleka hiyo mikataba Wizara ya Fedha ili kuona kama kwa kuingia nao mikataba hiyo Serikali itakuwa imefanya jambo sahihi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mfumo ambao ni mpya ambao ni lazima Serikali iende kwa umakini sana ili tusije tukaingia kwenye mkataba ambao hatukujipanga vizuri. Kwa hiyo, kuna umakini mkubwa sana ambao unafanyika ili tuweze kwenda na miradi hii mikubwa ambayo kama tutaijenga, basi tutakuwa tumepunguza kero nyingi sana za usafiri. Tumechukua barabara nyingi zile ambazo ni ndefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa idhini yako nitataja barabara chache. Ni Barabara ya kutoka Ifakara – Malinyi – Kilosa kwa Mpepo hadi Namtumbo. Tuna barabara ya Mafinga hadi Mgororo, tuna barabara ya Kongwa – Kibaya hadi Arusha, tuna barabara ya Karatu hadi Arusha, tuna barabara ya Karatu – Mbulu – Hydom hadi Sibiti. Pia tuna barabara ya Masasi – Nachingwea hadi Liwale; na tuna barabara ya Igawa – Songwe hadi Tunduma. Hizo ni baadhi ya barabara ambazo zimeingia kwenye mpango huu. Kwa hiyo, ukiangalia ni barabara kubwa ambazo tungetamani tuzijenge kwa wakati mmoja kwa utaratibu huu wa *EPC +F*, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, kwa majibu yako Mheshimiwa. Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Barabara inayotoka Dodoma kwenda Iringa ina mashimo, yaani haipitiki, ni shida tupu.

Je, Serikali haioni iko haja sasa ya kwenda kufukia tu yale mashimo badala ya kusubiri muda eti ya kuikwangua barabara yote kiasi ambacho itachukuwa muda mrefu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ntara, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba barabara ya Dodoma – Iringa ina mashimo lakini atakubaliana nami kwamba jitihada zimekuwa zikifanyika sana za kuhakikisha kwamba yale maeneo ambayo ni korofi yanazibwa na yanaendelea kuzibwa. Nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hizi zina madaraja. Kwanza, ukiangalia madaraja yapo mengi, sasa wakati tunajenga hiyo barabara *traffic* haikuwa imetegemewa kama ilivyo sasa. Kwa hiyo sasa hivi bado tunaendelea kufanya *economic design* kuona namna ya kuboresha hiyo barabara kwa sababu sasa imeoneka ni barabara ambayo inapitisha *traffic* nyingi lakini pia kuna magari mengi makubwa na mazito ambayo yanapita kwenye hiyo barabara, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Timetheo Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. TIMETHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ukizingatia kwamba kazi ya upembuzi na usanifu ulikamilika muda mrefu: Ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kuijenga kwa lami barabara ya kutoka Korogwe – Dindira – Bumbuli mpaka Songwe?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mnzava, Mbunge wa Korogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema ni kweli barabara hiyo ni muhimu na ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tusubiri bajeti tutakayoisoma, naamini kuna mapendekezo ya kuianza kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dennis Londo, swali la nyongeza.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya kutoka Kilosa kwenda Mikumi inaungana na Mji wa Kilosa ambako kuna uwekezaji wa mabilioni ya hela *station* ya *SGR* lakini kipande hiki kimekuwa kimeingia kwenye bajeti kwa miaka mitano mfululizo bila utekelezaji. Sasa kwa kuwa sisi wengine hatujui kuruka sarakasi ndani ya Bunge, ni lugha ipi ambayo unataka tutumie kuwaeleza Serikali barabara hii ni muhimu kutengenezwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu swali hilo muhimu sana.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno yake ya mwisho sikuyapata vizuri.

**MWENYEKITI:** Atumie lugha gani; yeye hana uwezo wa kuruka sarakasi, atumie lugha gani ili hoja yake iweze kueleweka ya barabara?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI - (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Londo, Mbunge wa Mikumi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba Serikali ilishaanza kuijenga hiyo

barabara kwa kiwango cha lami hadi Kilosa na tumetenga na tumeendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kuendelea kwenda Ulaya hadi Mikumi na ni azma ya Serikali kuunganisha hii Barabara ya Morogoro kutoka Dodoma kwenda Morogoro na Morogoro kwenda Iringa kupitia Kilosa hasa tukitambua umuhimu wa hiyo barabara kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inafahamu na ndiyo maana imeanza kutenga fedha na hata kwenye kipindi hiki cha bajeti nina hakika hiyo barabara itaendelea kutengewa fedha ili kuijenga japo siyo yote lakini kwa awamu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, napenda kujua ni lini Barabara ya Omugakorongo kwenda mpaka Murongo itajengwa ukizingatia Wilaya ya Kyerwa haina lami hata kilometa moja ukiachana na lami ya mchongo ambayo iko Nkwena? Nataka kujua ni lini kwa sababu imechukua muda mrefu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anatropia, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara aliyoitaja ya Omugakorongo hadi Murongo tunavyoongea sasa hivi iko kwenye hatua za manunuzi na nina hakika kabla ya kumaliza mwaka huu wa fedha barabara hiyo itakuwa imeanza na nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii itaanza kujengwa upande wa Murongo kuja Omugakorongo

ili tuweze kujenga lile Daraja la Mto Kagera ambao unapakanisha sisi na Uganda.

**MWENYEKITI:** Sasa namuita Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa aulize swali lake.

Na. 58

**Barabara ya Njiapanda ya Iyula – Idiwili hadi Ileje**

**MHE. JAPHET N. HASUNGA** aliuliza:-

Je, ni lini barabara ya kutoka njia panda ya Iyula – Idiwili - Nyimbili hadi Ileje itajengwa kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* imeanza kujenga barabara ya Njiapanda ya Iyula – Idiwili – Nyimbili hadi Ileje (kilometa 79) kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Mkandarasi amepatikana kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kilometa 2.1 kwa sehemu ya barabara ya kuanzia Njiapanda ya Iyula kuelekea Idiwili. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu iliyobaki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Japhet Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza naishukuru Serikali kwa kuanza kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo lakini kwa kuwa kuna baadhi ya maeneo ambayo barabara hiyo imewafuata wananchi. Je, Serikali inampango gani kuhakikisha kwamba wananchi hao wanapewa fidia stahiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa barabara hiyo ina urefu wa kilometa 79 na bado haijakamilika upembuzi yakinifu, Serikali inamkakati gani wa kuhakikisha kwamba inakamilisha upembuzi yakinifu kwa kilometa zote zilizobaki?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Jimbo la Vwawa kwamba tayari jedwali baada ya kuhakikiwa la malipo ya fidia kwa wale ambao barabara imefuata liko hazina kwa ajili ya uhakiki na hatua inayofuata sasa ni kwenda kufanya *disclosure,* yaani kuwaonyesha kila mtu atalipwa nini kwa maeneo ambayo bado. Kwa hiyo, naomba niwahakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi kwamba suala hili linaendelea na watalipwa hiyo fidia yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kukamilisha upembuzi na usanifu tuko kwenye hatua za mwisho kabisa kukamilisha usanifu ambapo ni hiyo Barabara ya Idiwili lakini Mahenge – Hasamba hadi Ileje.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kuuliza swali Mheshimiwa Naibu Waziri. Je, ni kweli kwamba miradi ya barabara ile nane aliyoisema kwenye majibu yake ya msingi ikiwemo ya Masasi – Nachingwea itakayojengwa kwa *program* ya *EPC + F* ni kwamba haijulikani lini itaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hokororo, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda na barabara hizi zote kwa pamoja na kama Mheshimiwa Mbunge alinisikiliza, hizi ni hatua na ni mfumo mpya. Kwa hiyo, kusema ni lini tarehe itakuwa ngumu lakini tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara ya Fedha sasa hivi inapitia kila barabara na kuona kwamba tunafanya tunavyotakiwa ili tutakapoanza kuzijenga hizo barabara tuwe na uhakika kwamba tulichofanya ni maamuzi sahihi na yatakwenda. Kwa hiyo, cha msingi tu ni kwamba ni hatua, ni *process* ambayo inaendelea lakini tutakapokuwa tumekamilisha upande huu tukishaanza kuitangaza sasa unaweza ukasema sasa baada ya kuitangaza tuna muda huu na huu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, swali la nyongeza.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Barabara ya kutoka pale Nyashimo kwenda Dutwa yenye kilometa 47 tumekuwa tukiahidiwa kujengwa kwa kiwango cha lami zaidi ya miaka 10 sasa na kila nikiuliza toka nimekuja hapa Bungeni nimekuwa nikiambiwa kwamba itaanza kujengwa mwaka wa fedha ujao. Sasa naomba

kuuliza ni mwaka wa fedha upi barabara hii sasa itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lusengekile, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama anavyosema lakini kujenga kwa barabara pia kunategemea kwa kweli na upatikanaji wa fedha na mpango wa Serikali kwa kweli ni kuzijenga hizi barabara kwa kiwango cha lami ikiwepo na barabara ya Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, tunakwenda kwenye bajeti naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira, kadiri muda unavyokwenda na kadiri tutakapoendelea kupata fedha barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chaurembo swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nataka kujua ni lini Serikali itajenga kipande cha Barabara kutoka Mbande Kisewe mpaka Msongola ili kuunganisha Wilaya ya Temeke na Wilaya ya Ilala?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chaurembo, Mbunge wa Mbagala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama tulivyoongea barabara hii imeshakabidhiwa kwa *Manager* wa Mkoa wa Dar es Salaam kukamilisha hicho kipande kidogo sana ambacho kimebaki kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunda, Mbunge wa Mbinga Mjini swali la nyongeza.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya Mbinga – Litembo – Nkili ni barabara muhimu sana kwa wakulima wa kahawa. Nataka nipate majibu ya Serikali ni lini Serikali itaanza kujenga barabara hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunda, Mbunge wa Mbinga Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara aliyotaja itaanza kujengwa mara tu tutakapokuwa tumefanya *review* ama kukamilisha usanifu wa kina ikiwa sasa tutakuwa tumepata gharama ya hiyo barabara kuijenga kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtemvu swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona. Kwa kuwa ipo Barabara ya Makondeko – Kwembe – Kisopwa hadi Mloganzila ya kilometa 14.66 imekuwa kwenye mpango na bajeti kwa miaka mitatu mfululizo. Je, ni lini sasa Serikali itaanza kujenga kipande cha Makondeko kuelekea Kwembe hadi Kisopwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mtemvu, Mbunge wa Kibamba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Makondeko – Kwembe kwenda Kisopwa ni kati ya barabara ambazo zimejumuishwa kama barabara za kupunguza misongamano katika majiji. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge mpango upo wa kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Jimbo la Geita Vijijini wananchi wake hawajawahi kuona lami na tulipata lami kilometa 20 kutoka Nkome mpaka Kijiji cha Igate na upembuzi yakinifu tayari Mkandarasi tayari.

Je, ni lini mkandarasi huyo anaingia *site* kuanza kazi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Musukuma, Mbunge wa Geita kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupo kwenye hatua za mwisho kabisa ili mkandarasi aweze kukabidhiwa hiyo *site* na nadhani Mheshimiwa Musukuma pia anajua kwamba taratibu zote

karibu zimeshakamilika kwa hiyo kilichobaki tu ni hatua za mwisho ili mkandarasi aweze kukabidhiwa hiyo *site*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ighondo swali la nyongeza.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kuniona.

Ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi wa kiwango cha lami kwa barabara inayotoka Singida Mjini – Ilongero – Mtinko mpaka Haydom kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ighondo, Mbunge wa Singida kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Singida – Ilongero inayoelekea Hydom tupo tunakamilisha usanifu wa mwisho. Tulifanya usanifu wa awali lakini sasa hivi tupo tunakamilisha usanifu na baada ya kupata hiyo *detail design* ndiyo sasa mipango ya kuijenga kwa kiwango cha lami itaanza.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mtenga Mbunge wa Mtwara Mjini swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru, nataka nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna barabara ambayo inatoka Mtwara Mnivata inayojengwa kwa kiwango cha lami kuelekea Newala mpaka Masasi. Kwa taratibu ambazo zinaendelea sasa hivi kuanzia Mnivata – Newala – Masasi wapo kwenye hatua za kulipa malipo kwenye zile nyumba ambazo zimeondolewa na miche. Lakini kipande cha kilometa 50 ambacho tayari

kimejengwa barabara ya lami mpaka leo wananchi hawajalipwa fedha zao kama fidia. Je, ni lini Serikali itarudi kuwalipa fidia wananchi wale?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi barabara Mtwara – Mnivata imetekelezwa kwa fedha ya Serikali ya Tanzania na Barabara ya kuanzia Mnivata – Newala kwenda Masasi itatekelezwa kwa kusaidiana na wahisani ambao ni *African Development Bank.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwamba kama kuna wananchi ambao katika eneo la Mtwara Mnivata bado wana changamoto ikiwa ni nje ya zile kilometa 45 tuweze kuonana nae ili niweze kupata taarifa kamili kwa wananchi ambao bado wanadai fidia eneo hili la Mtwara – Mnivata kilometa 50.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Barabara inayoanzia *USA River* kupitia *Arusha National Park* kwenda mpaka Oldonyo Sambu imejengwa kwa kiwango cha lami hadi kwenye lango la kuingia hifadhini.

Je, Serikali inampango gani wa kumalizia kipande kilichobaki kuanzia Ngarenanyuki kwenda Oldonyo Sambu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, Mbunge wa Arumeru kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, azma ya Serikali ni kukamilisha hicho kipande ambacho kimebaki lakini ukamilishaji wake pia utategemea na upatikanaji wa fedha na kwa kuwa tuko kwenye kipindi cha bajeti naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira tuone kama tutakuwa tumependekeza nini katika bajeti ambayo tunaiendea kuileta mbele ya Bunge lako.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi *Engineer* Kasekenya Msongwe ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia. Namuita Mheshimiwa Kabula Enock Shitobelo, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake. Swali lake litaulizwa kwa niaba yake na nani? Dkt. Mnzava haya uliza swali kwa niaba yake.

Na. 59

**Kudhibiti matukio ya ubakaji na ulawiti katika shule za bweni**

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA K.n.y. MHE. KABULA E. SHITOBELA** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kudhibiti matukio ya ubakaji na ulawiti katika shule za bweni?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Kipanga.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Kabula Enock Shitobela Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sehemu ya kudhibiti matukio ya ubakaji na ulawiti kwa wanafunzi, Serikali imetoa Waraka wa Elimu namba 11 wa mwaka 2002 kuhusu malezi, unasihi na ulinzi wa mtoto ambapo Waraka unaelekeza kila shule na chuo cha ualimu kuanzisha huduma za malezi na ushauri nasaha kwa wanafunzi. Katika utekelezaji wa Waraka huo Serikali imewezesha mafunzo kwa walimu wawili wa ushauri na unasihi kwa kila shule pamoja na kuanzisha dawati la ulinzi na usalama wa mtoto shuleni kwa lengo la kutoa fursa kwa wanafunzi kuzungumza na kuripoti vitendo vya unyanyasaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imetoa Waraka wa Elimu namba mbili wa mwaka 2023 kuhusu utoaji wa huduma ya bweni kwa wanafunzi wa elimu ya awali na msingi ambapo waraka huu unaelekeza kuwa huduma ya bweni itolewe kwa wanafunzi kuanzia darasa la tano na kuendelea. Hatua hii imezingatia ukweli kuwa wanafunzi wa umri huo walau wana upeo wa kutambua baya na zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wito wangu kwa wazazi, walezi na jamii kwa ujumla ni kushiriki kikamilifu katika ulinzi wa mtoto dhidi ya vitendo vya unyanyasaji wawapo shuleni na majumbani pia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu lakini vitendo vya ubakaji na ulawiti wa watoto wadogo ni vitendo ambavyo vimekithiri katika nchi yetu na moja ya

sheria ni kufungwa kifungo cha miaka 30 jela. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kwa sababu ubakaji ni uuaji, kuleta mabadiliko ya sheria ili wabakaji na walawiti wa watoto waweze kuhukumiwa kifungo cha kifo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mnzava kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anayozungumza Mheshimiwa Mbunge kwamba imekuwepo sheria ya miaka 30 lakini inaonekanika kama ni sheria legevu kidogo naye Mheshimiwa Mbunge anatoa mawazo, anatoa mapendekezo kwa nini isiwepo adhabu hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba tubebe mawazo yake hayo twende tukayafanyie tathmini tuweze kuangalia namna gani sheria hiyo inaweza kubadilishwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, namwita Mheshimiwa Omar Issa Kombo, Mbunge wa Wingwi aulize swali lake.

Na. 60

**Hitaji la Kituo cha Polisi na samani Wilaya ya Micheweni**

**MHE. OMAR ISSA KOMBO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo kipya cha Polisi cha Wilaya ya Micheweni pamoja na kupeleka samani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jumanne Sagini, Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la mheshimiwa Omar Issa Kombo Mbunge wa Wingwi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Micheweni ina kituo cha Polisi daraja *B* ambacho kinakidhi mahitaji ya kutoa huduma ya Polisi eneo hilo. Tatizo pekee la kituo hiki ni uchakavu unaohitaji kufanyiwa ukarabati. Tathmini ya uchakavu wa kituo imefanyika mwezi Januari 2023, na kubaini kuwa jumla ya shilingi 65,000,000 zinahitajika kwa ajili ya kubadilisha paa, dari, milango na madirisha, mfumo wa maji safi, maji taka, umeme, kuziba nyufa na kupaka rangi. Fedha hizo zimetengwa katika bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2023/2024 na kiasi cha fedha shilingi 17, 870,000 kwa ajili ya ununuzi wa samani za ofisi zinatarajiwa kuombwa kutoka kwenye mfuko wa tuzo na tozo kwa mwaka 2023/2024 mara ukarabati wa kituo utakapo kamilika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Omary Issa Kombo Mbunge wa Wingwi, swali la nyongeza.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini nina swali dogo tu la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni awamu ya pili hii kuambiwa tumetengewa fedha kwa ajili ya ukarabati wa kituo hiki. Na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba kwa kweli uchakavu ni wa hali mbaya sana. Tunaomba *commitment* ya Serikali; kama ni kweli kituo hiki kitajengwa

kwenye bajeti ya mwaka unaokuja, ni *quarter* ipi wamepanga kufanya ukarabati wa kituo hiki?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kombo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, atakumbuka Mheshimiwa Kombo kwamba nilitembelea Kituo hiki cha Micheweni nikajionea hali halisi; na kwa msingi huo tukakubaliana ndani ya Wizara na Jeshi la Polisi kutenga fedha. Atakumbuka kwamba miaka iliyopita hata kama alipewa ahadi hakuna fedha iliyotengwa lakini mwaka ujao namhakikishia fedha imetengwa na tutahakikisha tutakapopata fedha za maendeleo basi kituo hiki tutakipa kipaumbele, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deus Sangu swali la nyongeza.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kituo cha Polisi Mji Mdogo wa Mpui na Kaengesa vimechakaa sana na vinahudumia kata 11.

Je, ni lini Serikali inakarabati vituo vya polisi katika mji mdogo wa Kaengesa na Mpui?

**MWENYEKITI:** majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deus kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake ameliuliza kwa ujumla, kwamba ni lini Serikali itakarabati vituo vilivyochakaa

kama ilivyo cha kwakwe cha mji mdogo alioutaja. Nimuahidi tu kwamba pale tutakapokuwa tunapata fedha na vituo hivi vikiingizwa kwenye bajeti basi vitafanyiwa ukarabati. Atakumbuka kwamba mwaka huu maeneo mengi ikiwemo hata Zanzibar na Bara baadhi ya vituo vimekarabatiwa. Kwa hivyo nimwahidi tu kwamba kadri hali ya fedha itakavyoruhusu kituo chake pia kitafanyiwa ukarabati, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya swali la nyongeza. Wananchi wa Kata ya Nanjirinji wakishirikiana na mimi Mbunge wao wamejenga na kukamilisha kituo cha polisi ili kupunguza uhalifu mkubwa katika eneo la Nanjirinji. Je, Serikali iko tayari sasa kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani kuelekeza uongozi wa polisi Mkoa wa Lindi wakakague kituo hiki wafanye tathmini na hatimaye kupanga askari wakafanye kazi pale?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ally Kassinge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Kassinge kwa kujumuika na wananchi wake wakajenga na wakakamilisha kituo cha polisi kama ilivyoelezwa hapa Bungeni. Ni maelekezo yangu kwa *IGP* kupitia Kamanda wake wa Polisi wa Mkoa wafanye ukaguzi wa kituo hiki ili kama kina kidhi haja kiweze kupangiwa askari na kuanza kuwahudumia wananchi wa eneo hilo, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana; Wilaya ya Skonge tangu ianzishwe mwaka 1996 *OCD* amejibanza kwenye vijumba ambavyo vilianzishwa na Mtemi Haruna Msagila Lugusha, 1957, havitoshi na havifai;

Je, Wilaya ya Skonge itajengewa lini kituo cha polisi cha Wilaya chenye hadhi?

**MWENYEKITI:** majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joseph Kakunda kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tuungane naye kwamba baadhi ya majengo yanayotumika na polisi si yale yaliyojengwa na Serikali bali ni yale yaliyotolewa na wadau waliokuwa kwenye maeneo hayo miaka kadhaa iliyopita. Sasa kupitia Bunge lako Tukufu nimwombe *IGP* kupitia *RPC* wake wa Mkoa wa Tabora waweze kufanya tathmini ya eneo hilo la kibanda anachosema kinakaliwa na *OCD* wa Sikonge kuangalia kiwango gani cha ukarabati tunahitajika kufanyika ili tukitengee fedha kikarabatiwe kikidhi mahitaji ya *OCD,* nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naomba kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwamba maeneo mengi yaliyojengwa vituo vya polisi ikiwemo kituo kikuu cha polisi pale Nyegezi ambacho kitasaidia maeneo mengi sana, kwa maana ya ukanda wa kata za Buhongwa, Mkolani, Ruanima, Nyegezi, Luchelele pamoja na Mkolani yenyewe.

Je, ni lini sasa Serikali itafanya ukamilishaji wa kituo hiki?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mabula kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nielekeze Mkuu wa Polisi Nchini *(IGP)* Wambura kupitia Kamanda wake wa Mkoa wa Mwanza wapiti kituo hiki cha Nyegezi alichokieleza Mheshimiwa Mbunge kuona kiasi gani cha umaliziaji unaotakiwa kufanyika ili gharama zake ziweze kutengewa fedha na kikamilishwe ili kiweze kuwanufaisha wananchi wa maeneo yaliyotajwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi kwa majibu yako. Tunaendelea na Wizara ya Afya, namwita Mheshimiwa Minza Simon Mjika Mbunge wa Viti Maalum aweze kuuliza swali lake.

Na. 61

**Hitaji la watumishi Hospitali ya Rufaa ya Simiyu**

**MHE. MINZA S. MJIKA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaongeza Watumishi wa Afya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu mwaka 2018 ilikuwa na watumishi 130. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara iliwapanga watumishi 70 katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu na kuhamisha wengine 18 hivyo kufanya jumla ya watumishi kuwa 218.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuwapanga watumishi katika mikoa hii ya pembezoni mwa nchi ili kufikia malengo kwa kadri tutakapokuwa tunapata vibali vya kuajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Minza Simon Mjika, swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, napenda kumshukuru sana Waziri kwa majibu yake mazuri. Nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Busega na Wilaya Itirima tuna hospitali nzuri sana za wilaya, tatizo ni moja majengo ni mazuri na yanapenda hatuna watumishi wa kutosha. Kwa hiyo hospitali zile hazina hadhi ya kuitwa hospitali ya wilaya kwa sababu watumishi hawatoshi;

Je ni lini Serikali itapeleka watumishi wa kutosha ili na wananchi wa kule wafaidike?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge jinsi

anavyofuatilia masuala ya afya kwenye mkoa wake kwa kushirikiana na Wabunge wa majimbo. Kama ambavyo nimesema kwamba kwa mwaka huu tunategemea kupata watumishi takribani 12,000 hivi. Tutaendelea kushirikiana na wenzetu wa TAMISEMI ili tuweze kuona ni namna gani tunaweza kupeleka watumishi maeneo hayo ili wananchi waweze kupata huduma kulingana na ukubwa wa hospitali yenyewe.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Furaha Matondo.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe ina changamoto kubwa sana ya watumishi kada ya elimu na afya;

Je, ni lini Serikali itapeleka watumishi katika Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe ili kuondoa changamoto iliyopo hasa ukizingatia Ukerewe ni kisiwa ambacho kimejitenga na wananchi wake wanapata shida sana?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kuuliza swali zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si tu suala la watumishi kwenye Kisiwa cha Ukerewe, tumeamua kama Wizara ya Afya tuchukulie Ukerewe kama kanda maalum; na ndiyo maana Hospitali ya Wilaya ya Ukerewe sasa inaenda kupewa hadhi kama hospitali ya mkoa. Maana yake ni kwamba sasa yenyewe haitaenda kupata watumishi na vilevile vifaa tiba na mambo mengine kama hospitali ya wilaya bali inaenda kupata kama hospitali ya mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunajua kwamba kuna visiwa mbalimbali; ukisema umemaliza kijiji kimoja kumbe kijiji hicho kina visiwa mbalimbali. Maana yake ni kwamba ukizungumzia zahanati hutaenda kufikiria Ukerewe ukasema kijiji ukadhani umemaliza. Tunatamani kila kisiwa kiwe na zahanati yake kwa ajili ya *logistic* zilizopo kule. Kwa hiyo tunachukua tutashirikiana na wewe Mbunge na Mbunge wa Jimbo tuhakikishe tumefikia azma yenu ambayo mnaitamani.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri; tunaendelea na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara namwita Daktari Oscar Ishengoma Kikoyo Mbunge wa Muleba Kusini aweze kuuliza swali lake.

Na. 62

**Kuongeza mtaji Kiwanda cha *TANICA***

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukiongezea mtaji kiwanda cha Kahawa cha *TANICA*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Jimbo la Muleba Kusini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua mwenendo wa kibiashara usioridhisha wa Kiwanda cha *Tanganyika Instant Coffee Company Limited (TANICA)* unaochangiwa na

changamoto ya ukosefu wa mtaji, uchakavu wa mitambo, matumizi ya teknolojia iliyopitwa na wakati na kiwanda kuwa na madeni makubwa. Kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina, Serikali imefanya upembuzi yakinifu wa mahitaji ya rasilimali fedha kwa ajili ya kuendesha kiwanda hicho, ambapo imebainika kuwa zinahitajika takribani dola za Marekani milioni 1.31.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Serikali inafanya mashauriano na wanahisa wa kiwanda ili wawekeze kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya kukiboresha na kuendesha kiwanda hicho. Serikali ina nia ya dhati kuhakikisha kuwa kiwanda hicho kinafanya kazi kwa ufanisi na tija ili kuendeleza zao la kahawa ambalo linalimwa kwa wingi katika Mkoa wa Kagera, nakushukuru.

**MWENYEKITI :** Mheshimiwa Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana; Mkoa wa Kagera unafahamika kwa uzalishaji wa zao la kahawa, na ni zao la kimkakati, na Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imejikita kuboresha na kuongeza thamani ya zao la kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya wabia wa Kiwanda cha *TANICA* Serikali ni mbia na kuna hisa za zaidi bilioni 8.6…

**MWENYEKITI :** Mheshimiwa Kikoyo naomba uulize swali.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:…** ambazo hazijalipiwa. Je, Serikali ina mkakati gani kuhakisha kwamba hizo hisa ambazo hazijalipiwa za bilioni 8.6 zinalipiwa ?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Jimbo la Muleba Kusini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, Serikali iliunda kamati maalum kwa ajili ya kuangalia namna ya kukikwamua kiwanda hiki muhimu sana cha kuzalisha kahawa katika Mkoa wa Kagera; hivyo tuko katika hatua za mwisho za kuona namna gani ya kupata fedha hizo pia kuona wanahisa wanaongeza hitaji ili, moja, kupata hizo fedha ambazo ni mtaji muhimu pili, kupata teknolojia ya kisasa ambayo itasaidia uzalishaji wenye tija wa kiwanda hicho ; kwa sababu moja ya changamoto tuliyonayo ni uchakavu wa mitambo au mashine zilizofungwa tangia mwaka 1967.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Serikali inafanyia kazi na fedha zitakazopatikana tutaweza kuboresha kiwanda hiki pia kuhakikisha uzalishaji unakuwa na tija kwa ajili ya manufaa Taifa hili na Mkoa wa Kagera, nakushukuru.

**MWENYEKITI :** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, namwita Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete Mbunge wa Viti Maalum aweze kuuliza swali lake. Swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Bilakwate.

Na. 63

**Kuwasaidia wakulima wa zao la kahawa Tarime**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE K.n.y. MHE. GHATI Z. CHOMETE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia wakulima wa Tarime wanaolima kahawa aina ya Arabika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Bodi ya Kahawa inaendelea kukiwezesha na kukiongezea uwezo Kituo Kidogo cha Utafiti wa Kahawa (*TaCRI)* kilichopo eneo la Nyamwaga Tarime ili kuzalisha miche milioni moja kwa mwaka. Miche hiyo inaendelea kuzalishwa na kusambazwa bure kwa wakulima wa Kahawa Wilaya ya Tarime na Wilaya nyingine za Mkoa wa Mara. Kupitia jitihada hizi kuanzia mwezi Septemba, 2022 hadi kufikia mwezi Machi, 2023 jumla ya miche 173,471 imezalishwa na kugawiwa bure kwa wakulima. Aidha, Serikali imeboresha mfumo wa masoko kwa kuwezesha kuanza kufanya kazi kwa mitambo ya kuchakata kahawa katika maeneo ya Muriba na Nyantira.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bilakwate, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana; zao la kahawa limevamiwa na ugonjwa wa mnyauko ambao unaweza ukasababisha zao hili kutoweka zao hili muhimu;

Je, Serikali imechukua hatua gani za haraka ili kulinda zao hili muhimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; zao la kahawa ni zao la kimkakati lakini bado halijaweza kumnufaisha mkulima ipasavyo;

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweka masoko mazuri ambayo yatamnufaisha mkulima apate bei nzuri?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali la kwanza, kahawa inaathiriwa na magonjwa makubwa matatu chulebuni, kutu ya majani pamoja na mnyauko fuzari. Mnyauko fuzari ndio umekuwa ni changamoto kubwa sana. Hatua ambazo tumezichukua, kituo chetu cha utafiti wa zao la kahawa *TaCRI* hivi sasa kinakuja na *variety* mpya ambayo itakuwa ni himilivu katika magonjwa, hasa ugonjwa huu wa mnyauko fuzari. Pia tumeendelea kutoa elimu kwa wakulima juu ya kufanya palizi ; kwa sababu moja ya changamoto kubwa ni mashamba kuwa machafu, vilevile kung'oa miche yenye changamoto na isipandwe kabla ya miezi sita ndio elimu tumekuwa tukizitoa.

**MWENYEKITI :** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako. Tunaendelea na Wizara ya Maji namwita Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro Mbunge wa Ngara aulize swali lake.

Na. 64

**Mradi wa Maji wa Kabanga**

**MHE. NDAISABA G. RUHORO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Mradi wa Maji Kabanga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, kwa niaba ya Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii, Mary Francis Masanja, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro Mbunge wa Ngara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Mradi wa Maji Kabanga unaendelea kwa gharama ya Shilingi 941,351,342.74. Utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 75 na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2023 na kuhudumia wananchi zaidi ya 15,000 wa Vijiji vya Kabanga, Murukukumbo na Kumwuzuza. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa dakio, nyumba ya mashine, tanki la kukusanyia maji lenye ujazo wa lita 120,000, tanki la kuhifadhia maji lenye ujazo wa lita 230,000 na ujenzi wa viosk vitatu. Kazi zinazoendelea ni pamoja na uchimbaji wa mitaro kwa ajili ya kulaza mabomba umbali wa kilometa 20.694 na ukamilishaji wa ofisi ya *CBWSO*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, swali la nyongeza.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana; pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri mimi nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, mkandarasi wa mradi huo wa Kabanga hajalipwa fedha zake kwa mwaka mzima. Naomba kujua ni sababu gani zimesababisha mkandarasi huyu asilipwe fedha yake kwa mwaka mzima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; naomba kujua, Wizara ya Maji na Serikali wana mfumo wa kuweza ku-*track*

*status* ya miradi ya maji ili kuepukana na changamoto hizi za miradi kusimama na mkandarasi kutokuwa *site* kwa mwaka mzima? Naomba kupata majibu ya Serikali ya maswali hayo mawili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mbunge wa Ngara kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niendelee kuwaomba tu wakandarasi ambao wanaidai Serikali kwamba kwa sasa Serikali imeshaanza kulipa na tayari fedha zimeshaanza kupelekwa katika maeneo husika. Kwa hiyo wakae mkao wa kupokea fedha hizo ili waweze kuendelea na kazi ambazo ziko katika *site* hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa *strategy,* tunaamini kwamba lengo la Serikali ni kumtua ndoo mama kichwani, na *strategy* mojawapo ni kuhakikisha huduma ya maji inawafikia wananchi kwa ukaribu zaidi. Hivyo nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kuwa Serikali imeshaweka mikakati mahususi ya kuhakikisha maji haya yanawafikia wananchi tutaendelea kusimamia kwa ukaribu zaidi ili miradi hii iweze kukamilika na wananchi waweze kupata huduma iliyo bora.

**MWENYEKITI:** Ahsante namwita Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale aulize swali lake.

Na. 65

**Kujenga chujio chanzo cha maji cha Nyamtukuza**

**MHE. IDDI K. IDDI K.n.y. MHE. HUSSEIN N. AMAR** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga chujio la kuchuja na kutibu maji toka chanzo cha maji Nyamtukuza kabla ya kuyapeleka kwa wananchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyangh'wale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali Serikali ilipanga kujenga chujio la maji kwenye chanzo cha maji cha Nyamtukuza kwa ajili ya kuwapatia huduma ya maji safi na salama wananchi wa vijiji vya Nyangh'wale. Hata hivyo, kwa kuwa bomba kuu la *KASHWASA* linapita karibu, Serikali ilifanya usanifu wa kuchukua maji eneo la Mhangu na kubaini unafuu wa gharama ikilinganishwa na ujenzi wa chujio hivyo ilijenga mradi kupitia bomba hilo na hadi sasa vijiji 21 vinanufaika. Maji ya *KASHWASA* tayari yametibiwa na ni safi na salama na yatatosheleza mahitaji ya maji kwa wananchi wa Nyangh'wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa chujio sasa zinatumika kujenga miundombinu ya kusambaza maji kwenye vijiji vya Nyaruguguna, Nyamgogwa, Iseni, Nyangalamila, Kabiga, Nwiga, Bukungu, Bumanda, Kanegere, Mimbili na Isonda. Serikali itajenga chujio la kuchuja na kutibu maji Nyamtukuza kulingana na mahitaji ya huko baadaye.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Iddi Kassim, swali la nyongeza, kwa niaba ya Mheshimiwa Mbunge wa Nyangh'wale.

**MHE. IDD K. IDD:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana. Kwanza kabisa tunaipongeza Serikali kwa majibu mazuri haya na kwa kuwa mradi huu tayari umekamilika, sasa ni lini Wizara itatenga fedha ili kupeleka maji katika Kata ya Shabaka, Kata ya Kaboha, Kata ya Busolwa na Kata ya Mwingiro?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili la nyongeza; kwa kuwa Mradi huu wa Mangu – Ilogi umeshakamilika, je, ni lini sasa Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kupeleka maji katika Kata ya Runguya na Kata ya Segese? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Idd kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, kwa kuwa tunaendelea na mpango na bajeti wa mwaka huu unaokuja wa 2023/2024, maombi yake tutayaingiza katika bajeti hiyo ili wananchi wa maeneo husika waweze kufaidika na huduma bora ya maji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Magige, swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa muda mrefu sana Jimbo la Monduli hasa katika Kata ya Sepeko, Mswakini, Lepulko, Narami na Lemoti kumekuwa na changamoto kubwa ya maji. Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi zake katika maeneo haya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali

la nyongeza la Mheshimiwa Catherine Magige, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee tu kuwakumbusha wananchi kwamba miradi ya maji imeweza kutekelezwa katika miaka hii iliyopita, lakini kuna baadhi ya maeneo ambayo bado hatujawafikia. Tuwaahidi tu kwamba kwa kuwa tunaenda kwenye bajeti husika tutawaingiza katika bajeti hii inayokuja ili waweze kupata huduma bora ya maji safi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masanja, ahsante.

Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii. Namwita Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake.

Na. 67

**Kubadili majina ya kigeni kwenye rasilimali za Taifa**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itabadili majina ya kigeni kuwa ya Kitanzania kwenye rasilimali za Taifa ikiwemo Mlima Livingstone na Ziwa Victoria?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo baadhi ya Rasilimali za Taifa zenye majina na maeneo ambayo zilipewa tangu kipindi cha utawala wa ukoloni. Majina hayo yalitolewa kutokana na juhudi za waasisi katika ulinzi na uhifadhi wa rasilimali hizo. Majina na maeneo hayo yameendelea kufahamika kihistoria kutokana na kutangazwa na Taifa na kuandikwa kwenye nyaraka na vitabu mbalimbali na rasilimali hizo zimeendelea kuhifadhi historia ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa rasilimali hizo kwa historia ya nchi yetu na kuendelea kufahamika zaidi kitaifa na kimaitafa pasipokuwa na changamoto yoyote, Serikali haioni haja ya kubadili majina na maeneo hayo ambayo kwa sasa yana mchango mkubwa kiuchumi kwa Taifa letu. Aidha, Serikali kwa sasa inaendelea pia kuzingatia majina ya wazawa kwenye rasilimali mbalimbali za Taifa kadiri zinavyoanzishwa**.**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Mheshimiwa Waziri amezungumzia suala la historia, simba wa jina la *Bob Junior* aliyekufa siku za karibuni tumeona mataifa mbalimbali, vyombo vya habari zikichukua habari zake kama simba ambaye ni shujaa. Hivi ni kweli hatuna mashujaa hapa Tanzania ambao watapewa majina kama huyo simba aliyekufa? Ambaye pia watoto wake wanaitwa Rihana na majina mengine ya kizungu, hatuna watu mashuhuri kama kina Mkwawa, akina Mwansasu, aakina Mwakatumbula wakapewa majina hayo na mwisho tukaweza kufanikiwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; ukishasoma historia Livingstone na majina mengine kama hayo tuna Machifu katika maeneo yale ambao wangeweza kupewa majina

yao. Je, ni lini Serikali italeta Muswada wa kubadilisha majina kama hayo yaliyopewa wakati wa kikoloni ili watu wetu waweze kupewa hizo nafasi na majina yao ya Kiafrika yakasimama zaidi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimkumbushe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba utalii wa Tanzania au utalii wowote hapa duniani ni utalii unaohusisha wazawa kwa maana ya wenyeji, lakini pia na watalii wa nje. Tunapotumia majina maarufu hatutangazii Watanzania peke yake, tunatangazia ulimwengu, kwa hiyo hiyo historia inabebwa kiulimwengu. Kwa mfano tuna mchukulia *Bob Junior* ambaye ni simba ambaye amekufa hivi karibuni na alikuwa na watoto wake mmoja alikuwa anaitwa Rihana. Tunapotumia jina Rihana ina maana hata mtalii anetoka Marekani anaweza kuja kumwangalia Rihana, lakini tutakapompa *let say* Masanja, aliyesimama hapa watakao mfahamu wa hapa hapa Tanzania, kwa hiyo tunatangaza utalii duniani ili kuonyesha jinsi gani Watanzania tumejaliwa na rasilimali tulizonazo hapa nchini, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakagenda, hilo swali lako unaweza ukaleta kama swali la msingi kama hujaridhika na majibu hayo, maana Mheshimiwa Waziri, anasema ukiwapa majina ya hapa nchini haitambulishi kimataifa, sasa nafikiri inaleta maswali pia.

Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante kwa majibu yako. Tunaendelea na Wizara ya Madini, namwita Mheshimiwa

Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 66

**Wanawake kushiriki kwenye mnyororo wa madini**

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI K.n.y. MHE. ZAYTUN S. SWAI** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuhakikisha Wanawake wanashiriki kikamilifu kwenye mnyororo wa madini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wazari wa Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wamekuwa wakishiriki kwa kiasi kikubwa kwenye sekta ya madini kupitia vyama mbalimbali ikiwemo Shirikisho la wachimbaji wadogo nchini *(FEMATA)* lenye lengo la kuwaunganisha wachimbaji wadogo wa madini wakiwemo wanawake pia Umoja wa Wanawake Wachimbaji Madini *(TAWOMA)* ambao unajumuisha wanawake wote wanaojishughulisha na shughuli za uchimbaji na utengenezaji bidhaa mbalimbali zinazotokana na madini. Pia wako Muungano wa Wanawake Wanaouza Bidhaa Mbalimbali Migodini *(WIMO)* na Chama cha *Tanzania Women in Mining and Mineral Industry (TWIMMI)* ambacho kimeundwa kwa lengo la kuwaweka pamoja wachimbaji wa madini wanawake na wote walioko kwenye sekta ya madini ili kuweka mazingira bora ya kuwawezesha wanawake na ustawi wa sekta ya madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na uwepo wa vyama hivyo Wizara imekuwa ikisaidia wanawake kwenye sekta ya madini katika mnyororo mzima kwa kuwapa leseni za uchimbaji, uongezaji thamani na uuzaji madini, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangai, swali la nyongeza.

**MHE EMMANUEL L. OLE–SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri, kuhusiana na wanawake wanaoshiriki katika madini Mkoa wa Arusha lakini naomba kuuliza maswali mawili.

Swali la kwanza; wanawake wanapojishughulisha na shughuli za madini Mkoani Arusha wanakutana na changamoto nyingi sana; je, ni nini Mkakati wa Serikali wa kutatua changamoto zinazowakabili wanawake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Wilaya ya Ngorongoro yamegundulika madini mengi, lakini inaonekana kwamba wanawake hakuna mazingira yanayowawezesha kushiriki katika shughuli za madini. Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba maeneo ya madini kwenye Wilaya ya Ngorongoro yanapimwa ili wanawake nao waweze kushiriki ipasavyo katika shughuli hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Ole–Shangai, Mbunge wa Ngorongoro, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa changamoto za wanawake Serikali imeendelea kutoa elimu, kuwahamasisha wajiunge na vikundi mbalimbali ambavyo nimevitaja kwenye swali la msingi ili waweze kusaidiwa

kupata elimu juu ya sheria, kanuni na taratibu za madini pamoja na kufahamu fursa za biashara na uwekezaji kwenye sekta ikiwa ni pamoja na kuelekeza namna ya kupata mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali lake la pili kuhusu Wilaya yake ya Ngorongoro, ni kweli kwanza nimpongeze Mbunge maana yake mwisho wa mwezi uliyopita aliniomba nifanye Wizara kwenye Jimbolake ili kwenda kubaini changamoto zinazowakabili wachimbaji wa madini. Tukagundua kwamba Ngorongoro ina madini mengi sana ya vito, lakini uendelezaji wa sekta uko chini sana hasa kwa upande wa wanawake. Nitumie fursa hii kumhakikishia kwamba baada ya ziara ile tuliagiza Taasisi yetu ya Jiolojia na Utafiti wa Madini pamoja na Tume ya Madini waende kule wakahamasishe ile jamii na wabainishe maeneo yenye madini ili wanawake nao wa Ngorongoro wajiunge waweze kufaidi fursa hii iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukuishia hapo, Wizara hii imeteua Mabalozi wa Madini, wanawake wanaongozwa na Dkt. Ritta Kabati ambao kazi yao ni kuwahamasisha wanawake wote wanaopenda kujiingiza katika biashara ya madini, wafahamu biashara ya madini na fursa zilizoko za wawekezaji, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Mwandabila, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka kufahamu ni lini Serikali itaipatia Kampuni ya *Peak Resources* leseni? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba utaratibu wa kupata leseni za madini uko katika mfumo wa kieletroniki na mfumo huo unafikika kwa njia ya kimtandao. Baada ya mtu kuingia kwenye mtandao na akaomba leseni utaratibu mzima wa jinsi ya kujaza fomu, ada zinazohitajika unalipiwa kimtandao na kwa kawaida kama mifumo iko sawa na hakuna *break down* kwenye *system* ndani ya wiki, mbili leseni huwa zinatoka, lakini kama kuna changamoto kwenye leseni yoyote, Ofisi yetu ya Madini iko wazi saa zote na tuko tayari kutoa ushirikiano ili leseni anayoisemea iweze kupata.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, namwita Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, Mbunge wa Kiteto, aweze kuuliza swali lake.

Na. 53

**Ajira kwa walimu Kiteto**

**MHE. EDWARD O. KISAU** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itawaajiri walimu wanaojitolea katika Jimbo la Kiteto?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshiwa Edward Kisau Olelekaita, Mbunge wa Jimbo la Kiteto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto ina jumla ya walimu 752 wa shule za msingi na walimu

wa kujitolea 86. Aidha, kwa shule za sekondari kuna jumla ya walimu 298 na walimu wa kujitolea 34.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uwepo wa Walimu wa kujitolea katika shule za msingi na sekondari na kwa kuwa Serikali huajiri kulingana na upatikanaji wa fedha. Hivyo nafasi za ajira zikitangazwa, tunawashauri Walimu hawa wanaojitolea waombe nafasi hizo ili wale wanaokidhi vigezo waweze kuajiriwa kwa kupewa kipaumbele, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Olelekaita, swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa majibu ya Serikali.

Swali la kwanza; kwa kuwa Kiteto ina upungufu wa walimu karibu 800 ukichanganya shule za msingi na sekondari. Kwa hivyo kama isingekuwa siyo hawa 120 hali ingelikuwa mbaya; je, ni lini ni lini Serikali italeta Sheria ya Ajira hapa tuweke kigezo cha kujitolea iwe ni sababu ya mtu kuajiriwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; ni lini Mheshimiwa Waziri atakuja Kiteto akutane na Walimu hawa wazalendo wanaojitolea wanaojitolea ili azungumze nao? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Edward Kisau Olelekaita, Mbunge wa Jimbo la Kiteto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Halmashauri ya Kiteto ina upungufu wa walimu, lakini niwapongeze Halmashauri ya Kiteto kwa kuweka bajeti angalau kidogo

kwa ajili Walimu wanaojitolea. Nimhakikishie kwamba Serikali imeweka mpango na mwongozo kwa ajili ya kuwawezesha Walimu wanaojitolea kutambulika rasmi, lakini pia kupewa kipaumbele wakati fursa za ajira zinapojitokeza na kwa kuwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan leo kupitia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ametangaza jumla ya ajira 21,200 za Kada ya Elimu lakini pia na Kada ya Afya, niwatie shime hawa Walimu wanaojitolea Kiteto na maeneo mengine kuomba ajira hizo ili waweze kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili kuhusiana na kukutana na Walimu hawa sisi tuko tayari baada ya shughuli hizi za Bunge, basi tuambatane na Mheshimiwa Mbunge, ili tuweze kuonana na Walimu hao na kuwatia moyo kufanya kazi nzuri, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea namwita Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba aweze kuuliza swali lake.

Na. 54

**Hitaji la watumishi na vifaa katika Kituo cha Afya Majengo – Nanyamba**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupeleka watumishi na vifaa tiba katika Kituo cha Afya Majengo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Jimbo la Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua changamoto ya uhaba wa Wataalam wa afya katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Hata hivyo, Serikali imeendelea kutoa vibali vya kuajiri Watumishi wa Kada ya Afya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2020/2021 na 2021/2022, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI iliajiri Watumishi wa Kada za Afya 10,328 ambapo Halmashauri ya Mji Nanyamba ilipata watumishi 51 wa kada mbalimbali za afya. Aidha, Kituo cha Afya Majengo kilipangiwa watumishi wanne ambao ni Mteknolojia wa Maabara, Tabibu Msaidizi na Wauguzi wawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imepeleka vifaa na vifaa tiba katika Halmashauri ya Mji Nanyamba vyenye thamani ya shilingi milioni 300 kwa ajili ya vituo vya huduma za afya, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, pamoja na majibu ya mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; upungufu uliopo katika kila Kituo cha Majengo tuna upungufu huo katika Kituo cha Afya Jinyecha, Kiromba na Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Nanyamba na kupelekea kuwa na upungufu wa watumishi 610; je, Serikali ina mpango gani wa dharura kupunguza tatizo hilo la watumishi katika Halmashauri ya Mji wa Nanyamba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; Wizara ya Afya imetoa mwongozo wa wanachuo wa kada ya afya ambao wamemaliza waweze kujitolea katika vituo vya kutolea huduma.

Je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka wa kutenga fedha kiasi ili wahitimu hawa sasa waanze kufanya kazi katika maeneo yenye upungufu mkubwa wa watumishi? Kwa sababu kwanza itasaidiia tatizo la watumishi, lakini pili watakuwa wanatumia ujuzi wao wakati wanasubiri ajira za kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chikota, ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Jimbo la Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Halmashauri ya Nanyamba ina upungufu wa watumishi takribani 610 ambayo Mheshimiwa Mbunge amewataja na Mpango wa Serikali ni kuendelea kuajiri watumishi, lakini pia kupeleka watumishi wengi zaidi kwenye maeneo yenye changamoto kubwa zaidi ya watumishi hao kama ilivyo katika Halmashauri ya Nanyamba. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge hasa kwenye hizi ajira ambazo tayari zimetangazwa tutahakikisha halmashauri zote ikiwemo Nanyamba ambazo zina upungufu mkubwa zaidi wa watumishi zinapewa kipaumbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Serikali ni kweli kupitia Wizara ya Afya, lakini pia Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumetoa

mwongozo wa namna ya watumishi wa kada za afya kujitolea kwenye vituo vya huduma zetu. Tumeelekeza Wakurugenzi kutenga fedha za angalau posho kwa ajili ya wanaojitolea katika vituo vyetu, niendelee kusisitiza kwamba suala hili ni muhimu Wakurugenzi wafanye hivyo ili kuendelea kupunguza upungufu wa watumishi katika sekta hizo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Namwita Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mbunge wa Iramba Mashariki, aweze kuuliza swali lake.

Na. 55

**Ujenzi wa Vituo vya Afya Kinyangira na Mkalama Wilayani Mkalama**

**MHE. FRANCIS I. MTINGA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga majengo ya kisasa katika Vituo vya Afya vya Kinyangira na Mkalama katika Halmashauri ya Mkalama?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mbunge wa Jimbo la Iramba Mashariki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kujenga na kukarabati vituo vya afya kwenye Kata za kimkakati ili kusogeza huduma za afya karibu na wananchi. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetoa fedha shilingi

bilioni 117 kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya 234 kwenye Tarafa na Kata za kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vituo vya Afya vya Kinyangiri na Mkalama ni miongoni mwa vituo vinavyoendelea kutoa huduma katika ngazi ya Kituo cha Afya pamoja na changamoto ya upungufu wa miundombinu hususan ya upasuaji wa dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya nchini kote vikiwemo vituo vya afya Kinyangiri na Mkalama. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Isack Francis Mtinga, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali yanayojaribu kuwafariji wananchi wa Kinyangiri na Mkalama nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya Kinyangiri ni cha enzi ya ukoloni, ni kituo cha siku nyingi sana na kinahudumia Tarafa nzima, kilipelekea mpaka kiongozi mkubwa wa chama kinachounda Ilani kuwaahidi wananchi wa Kinyangiri kwamba ifikapo Disemba kama hawajapata majengo waandamane ofisini kwake. Serikali na Wizara ina kauli gani kuhusu kauli hii nzito ya Kiongozi mkubwa wa chama kinachounda Ilani?

Swali la pili; Kituo cha Afya Mkalama pia ni cha wakati wa ukoloni hakina uwezo hata wa kufunga *P.O.P* kama mtu amevunjika mkono au mguu, hivyo wananchi wanateseka na kinahudumia wananchi takribani 15,000. Serikali ina-*commitment* gani kuhusiana na bajeti hii inayokuja kuhusiana na Kituo hiki cha Afya cha Mkalama? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mbunge wa Jimbo la Iramba Mashariki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Kituo cha Afya cha Kinyangiri ni kituo chakavu na kituo kongwe, Serikali imeshaweka mpango wa kutafuta fedha ili kwenda kukikarabati pia kuongeza majengo ambayo yanapungua. Nimhakikishie kwamba Serikali hii kwa sababu inatekeleza Ilani cha Chama cha Mapinduzi na Kiongozi wetu alifika pale na kutoa maelekezo hayo, tunachukua maelekezo hayo na tunaanza kuyafanyia kazi kuhakikisha tunapata fedha kwa ajili ya kituo cha Kinyangiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pili; kuhusiana na kituo cha afya cha Mkalama ambacho nacho ni chakavu tutaendelea kutenga fedha kwa awamu ili tuweze kuvikarabati vituo kama hivi pia kuongeza miundombinu ambayo inakosekana. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali na majibu. Hapa mezani nina matangazo kadha wa kadha, naomba nianze na wageni waliopo Bungeni asubuhi ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 10 wa Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, Mbunge ambao ni Viongozi

wa Dini ya Kiislam kutoka Jimbo la Vunjo Mkoa wa Kilimanjaro, karibuni sana viongozi wetu wa dini. *(Makofi)*

Pili, ni wageni 75 wa Mheshimiwa Jonas Zeeland, Mbunge ambao ni Viongozi wa Tawi la UVCCM kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe, Mkoa wa Morogoro, karibuni sana Viongozi wa Tawi la UVCCM kutoka Chuo Kikuu Mzumbe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Innocent Kalogeris, Mbunge ambao ni Viongozi wa Taasisi mbalimbali kutoka Mkoa wa Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Minza Mjika, Mbunge ambao ni ndugu zake kutoka Meatu Mkoa wa Simiyu, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Pia tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mbunge ambao ni mkwe wake na watoto wake kutoka Vwawa, Mkoa wa Songwe, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Pia tunao wageni 33 wa Mheshimiwa Michael Kembaki, Mbunge ambao ni wanafunzi wa Shule ya *Mgambi Mission* wakiongozwa na Mkuu wa Shule Ndugu Ester Lakaki, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; moja; wanafunzi 60 kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* cha Jijini Dodoma. Hawa ni majirani zetu hawa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 100 kutoka Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini cha Jijini Dodoma. Wanafunzi kutoka Mipango, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hii ilikuwa ni *session* ya upande wa wageni, lakini kuna tangazo la Katibu wa Bunge ninaomba niwasomeeni na Waheshimiwa Wabunge tusikilizane wote.

Katibu wa Bunge anasema; naomba uwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yupo pale mmemuona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameandaa *Iftar* maalum kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge na watumishi wa Bunge. *Iftar* hii itafanyika katika viwanja vya Bunge leo siku ya Jumatano tarehe 12 Aprili, 2023 kuanzia Saa 12.30 jioni. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge anaendelea kusema kwamba Waheshimiwa Wabunge na watumishi wote wanaalikwa katika *Iftar* hii bila kukosa kama ilivyoelekezwa pia na Mheshimiwa Spika, yuko pale! *(Makofi)*

Sasa tunawaomba, hawa ni viongozi wetu wakubwa wakitualika jambo kama hili itakuwa ni heshima tukijumuika nao. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

Katibu.

## HOJA YA JAMBO LA DHARURA

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu jambo la dharura.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:** Hoja za Serikali…

**MWENYEKITI:** Ngoja Katibu.

Mheshimiwa King Kanuni?

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 54(1).

**MWENYEKITI:** Kanuni gani?

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Kanuni 54(1) ambayo inazungumzia kuahirisha shuguli za Bunge ili kujadili jambo la dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hivi karibuni kuna jambo limejitokeza ambalo nahisi kwamba linaweza likaleta usumbufu kwa Watanzania wengi. Jambo lenyewe linahusiana na Bima ya Afya kwa Watoto - *Toto Afya Card*. *Toto Afya Card* sasa hivi zimezuiliwa zile ambazo katika mfumo tuliouzoea na tulivyojaribu kutaka kupata ufafanuzi tuliambiwa kwamba zitapitia mashuleni. Tunafahamu watoto wapo katika *scenario* nyingi siyo wote ambao wako shuleni, hawa wengine tayari walikuwa wapo katika mwendelezo na wengine walikuwa wana-*renew*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipotaka ufafanuzi zaidi tukaambiwa wengine watapitia wazee wao, lakini katika *category* za bima ya afya ya chini ni 360,000 na wazee wengine hawana uwezo wa kupata bima hiyo akambeba mwanawe katika *Toto Afya Card*. Tulipotaka ufafanuzi zaidi tukaambiwa wale ambao wadogo na hawajaweza kwenda shule na wazee wao hawajawa na uwezo huo watapitia Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu taratibu za Wizara ya Afya katika masuala ya afya kwa Watoto, tunaelewa sote hali ikoje. Ninaliomba Bunge tujadili kwa dharura ili tujue hawa watoto ambao wako katika *scenario*

tofauti na hizi ambazo ziko hapa ili wasiweze kwenda kupata taabu kule. Tukijadili hili Wizara ya Afya Serikali itatuambia kwamba hawa wengine tunawafanya nini? Kwa sababu vinginevyo inawezekana tukaja tukawakosa watu kupitia hili tatizo ambalo limeingia sasa hivi, kwa sababu mfumo wa zamani sasa hivi umezuiliwa ule ambao tuliuzoea na Watanzania hawana habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ngoja kwanza. Hoja anayotoa ukiisoma kwenye Kanuni yetu ni Hoja ya kuahirisha Shughuli za Bunge. Hoja ya kuahirisha Shughuli Bunge, maana yake Bunge lisijadili jambo jingine lijadili hoja hiyo, wakati Mheshimiwa yeye amesema hoja ya dharura, ndiyo maana nikawa najaribu kukutazama hoja ya dharura unataka kujenga hoja gani? Maana yake hoja yake kama kwa Kanuni hii ni ya kuahirisha Bunge, shughuli zingine ili tujadili, hiyo ni namba moja. Mbili, ukisoma Kanuni yetu ya 54 na Kanuni ya 55(2) nenda *part* III inaeleza sifa za hoja hiyo labda niisome kwa haraka haraka:

(a) Athari zake ni dhahiri na zinaweza kutokea wakati wowote;

(b) Limetokea siku hiyo au siku za hivi karibuni na limeletwa bila kuchelewa;

(c) Hakutatokea fursa ya kujadili siku za karibuni kwa njia ya kawaida ya kushughulikia mambo ya Bunge;

(d) Jambo lolote litahesabiwa kuwa ni lenye maslahi kwa umma iwapo tatizo lake inategemea hatua zaidi kuliko zile za utekelezaji wa kawaida wa sheria peke yake.

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na maelezo mengine ambayo tumeyatoa pale jumla, tutawaelekeza Serikali

walete maelezo kuhusu hoja ambayo imetolewa ili tuweze kufahamu ni jambo gani kwa sababu halikutokea asubuhi ya leo. Haya ahsante.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Haya mwongozo wa Spika, Kanuni gani?

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa Kanuni ya 76 kuomba mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Endelea.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuomba mwongozo wako kwamba kuna jambo limekuwa linaongelewa hapa Bungeni na Wabunge wengi sana linahusu suala la *acquisition* ya Twiga *Cement* kutaka kuinunua *Tanga Cement*. Jambo hili endapo litafanyika litaruhusu Twiga *Cement* kuwa na *market share* ya zaidi ya asilimia 65 kwenye soko kiasi kwamba inaweza ikalazimisha Twiga *Cement* aka-*determine* bei ya *cement* na wazalishaji wengine kwa sababu watakuwa na *share* ndogo wakalazimishwa kupandisha bei ya *cement* ili kuendana na mtu mwenye *market share* kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilishatolewa amri ya Mahakama kulipinga hili, Mahakama ya Ushindani wa Kibiashara lakini sasa hivi inaonekana linataka kurudi tena likajadiliwa kwa sababu bado wao wanayo *interest* ya kutaka kununua *Twiga Cement,* jambo ambalo litakenda kuongeza *inflation* kwenye vifaa vya ujenzi na tumekuwa tunapambana nalo hapa kila mara. Sasa naomba mwongozo wako na Serikali labda itoe maelezo kwamba kwa nini wanataka kuruhusu jambo hili litokee, ambalo

litakwenda kuathiri sana kwenye soko la *cement* hapa nchini kwetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kwanza nilishalitolea tayari utaratibu Serikali italeta maelezo kwa ajili ya kushughulikia hoja yake.

Waheshimiwa Wabunge, naomba twende kwenye Kanuni ya 76 nawasomea. Mwongozo wa Spika kama alivyosimama Mheshimiwa Cecil Mwambe kwa ajili ya kuuomba leo; ''Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na Taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo au baadae kadri atakavyoona inafaa." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mbunge hoja yake inaweza kuwa na maslahi lakini hai-*qualify* kuingia kwenye Kanuni hii, kwa sababu haikutokea mapema leo. Kwa hiyo, kama tulivyosema ile hoja nyingine ya kwanza Serikali iko hapa italichukua italichakata na kuwajulisha Wabunge juu ya jambo hilo likoje. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Katibu tuendelee.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji, tunayo orodha ya wachangiaji hapa mezani na utaratibu ni kwamba Mbunge hatosimama wala kuzungumza bila kibali cha Spika. Kwa hiyo, tunaendelea na hoja iliyo mezani. Mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuwa mchangiaji wa kwanza kuanzisha shughuli hii asubuhi hii, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambae ameendelea kuonesha mapenzi makubwa kwa Watanzania kupitia kuachilia fedha ziende zikatekeleze miradi ya maendeleo. Wabunge watakubalina nami kwamba wao ni mashuhuda wa upendo mkubwa wa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan ambae anasukuma fedha nyingi kwenye Majimbo kwa ajiali ya kutatua changamoto nyingi za Watanzania. Nami na wananchi wangu wa Jimbo la Ngara tunamshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, juzi ameidhinisha 2,700,000,000 kwa ajili ya kwenda kujenga Chuo cha Ufundi - Ngara. Tunamshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hasssan na tunaendelea kumuunga mkono.

Mhehsimiwa Mwenyekiti, vilevile nimshukuru Waziri Mkuu, kwa kazi kubwa anayoifanya pia na kuwasilisha hotuba nzuri sana hapa Bungeni ambayo imejaa matumaini kwa Watanzania, kwa kweli ukisoma hotuba ile ya Waziri Mkuu inatuonesha inatupeleka kwenye Tanzania tunayoitaka. Ninamshukuru tena Waziri Mkuu na Waziri wa Kilimo kwa jambo lile la Kahawa, wananchi na wakulima wa Kagera na wale wa Wilaya ya Ngara kwa miaka zaidi ya 50 iliyopita tulikuwa hatujawahi kupata bei ya nzuri ya Kahawa. Katika msimu iliopita kwa mara ya kwanza tumeuza kilo moja shilingi

3,700 mpaka shilingi 2,000. Ni matarajio yetu kwamba msimu unaokuja Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wa Kilimo wataendeleza hatua ambazo zilichukuliwa kwenye msimu uliopita ili wananchi wa Jimbo la Ngara na wale wa Mkoa wa Kagera tuendelee kufurahia matunda mazuri ya Serikali yetu kwa kuendelea kuuza Kahawa kwa bei nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nielekeze sasa mchango wangu kwenye eneo la sekta ya madini. Katika hotuba ya Waziri Mkuu alielezea malengo na dira na mwelekeo wa sekta ya madini hapa nchini. Alielezea kwamba kwa upande wa makusanyo ambayo Wizara ya Madini ilikuwa imelenga kwenye mwaka wa fedha uliopita, walikuwa wamepanga kukusanya bilioni 479.51 na wakafanikiwa kukusanya bilioni 409.66 ambayo ni sawa na asilimia 85 ya *target* yote ambayo Wizara ilikuwa imejiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumweleza Waziri Mkuu na Mawaziri wengine hasa Waziri wa Madini kwamba kuna mambo kadha wa kadha kwenye sekta ya madini ambayo yanakwamisha juhudi za Serikali ili kuweza kufikia makusanyo ambayo yanatarajiwa, yamkini pengine makusanyo yangefika mpaka trillioni moja endapo vitu ninavyokwenda kuvizungumza vingefanyiwa kazi na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ambalo napenda kuchangia na naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu alichukulie kwa umuhimu wa aina yake ni eneo la kodi la mapato asilimia 30. Wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu, leseni wanazopewa ni zile leseni za kuwaruhusu kufanya utafiti na kuchimba madini kwa wakati mmoja, hii ina maana kwamba anachimba shimo hapa anakwenda anachimba shimo pale, fedha anazozipata hapa anazirudisha tena kwenye utafiti, *TRA* wao wanachokiangalia ni mchimbaji huyu kwenye akaunti yake zimeingia Bilioni ngapi, wanaomba nyaraka za viambatanisho, anapotoa

nyaraka ambazo siyo risiti za *EFD* wanazi-*reject* na wana–*subject* kwenye kodi ya mapato ya asilimia 30.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi hiyo haipo, wachimbaji wadogo hawana na hawataipata na sana sana Serikali itakwenda kuwafilisi kupitia *TRA,* kwa sababu, shughuli zao zile ni za kusaga mawe, kuchimba mashimo, kusogeza vifusi, na kusomba maji. Shughuli zote zinafanywa na Watanzania wa chini ambao hata *TIN Number* hawana, hata *line* za simu kwa kuwa hawana vitambulisho vya *NIDA* wanatumia za ndugu zao. Kwa hiyo, matokeo yake ni kwamba, ni watu ambao wako kwenye *informal sector* kuweza kupata risiti, haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Serikali katika eneo hili. *TRA* waachane na kodi ya asilimia 30 *(Corporate Tax),* waache kuwalazimisha wachimbaji wadogo kufunga mahesabu kwa sababu, hawawezi kufunga mahesabu kwa *nature* ya biashara zao. Naomba Serikali baada ya kukata mrahaba asilimia sita, baada ya kukata ada ya ukaguzi asilimia moja, baada ya kukata *Service Levy,* Serikali ikate asilimia moja kama kodi ya mapato kutoka kwenye mauzo ya dhahabu *on point of sale*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ni sawasawa na ule mchezo wa Biko au Bingo au ule mchezo wa Tatu Mzuka, kwamba, unapocheza Bahati Nasibu ukawa umeshinda pale, Serikali pale pale inachukua kodi yake.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndaisaba, naomba upokee Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Iddi Kassim.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilindie muda wangu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**T A A R I F A**

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa tu mchangiaji. Ukiacha *Corporate Tax* ambayo ni asilimia 30, sasa hivi *TRA* wanaenda wanazunguka, wanataka kuweka kodi nyingine asilimia mbili kumwongezea mchimbaji mdogo huyu ambaye hajawezeshwa kupewa mitaji na kupewa maeneo yenye utafiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ndaisaba unapokea Taarifa?

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea vizuri sana. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Kengele yako ya kwanza imeshagongwa.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli muda wangu nimekuomba unilindie. Niongezee hata dakika tano tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa endelea kuchangia, kengele ya pili itapiga sasa hivi.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Sasa nielekee eneo la pili la *VAT*. *TRA* wameendelea kuwabana *dealers* wote ambao wanafanya biashara ya dhahabu. Wanawataka hawa *dealers* waweze kulipa *VAT* kwenye dhahabu wanazonunua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamaanisha kwamba, *dealer* akiweza kununua dhahabu ya shilingi milioni 100, akishai-*subject* kwenye *VAT* anatakiwa kwenda kuuza ile dhahabu shilingi milioni 118. Hii fedha haipo kwa sababu

dhahabu, inanunuliwa kwa thamani ya bei ya Soko la Dunia. Hii inamaanisha kwamba, dhahabu inayonunuliwa Tanzania kwa mfumo huo wa *VAT,* haiuziki mahali popote pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuwaambia *TRA,* hii fedha kwa *dealers* haipo na wale *dealers* wanaowasumbua kule Kahama, Tanga na maeneo mengine kwamba walipe *VAT* asilimia 18, hawataipata na matokeo yake ni kwamba wachimbaji na *dealers* wote wataendelea kutorosha dhahabu hapa nchini. Kwa sababu ukinunua dhahabu kwa utaratibu ulivyo hapa Tanzania, huwezi kuiuza mahali popote pale duniani. Naomba niishauri Serikali na *TRA,* waachane na mambo ya *VAT* kwenye dhahabu. Warudi kwenye utaratibu ule ambao nimesema wa nipe nikupe, ama nilipe nisepe. Tukutane sokoni, wachukue asilimia moja, iwe inawatosha na Serikali wataona mapato yanavyoongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho ni eneo la kuchimba madini kwenye hifadhi. Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan, alishaeleza kwamba, tembo na wanyama wengine huko porini hawali madini. Ukienda kwa mfano kwenye *Game Reserve* ya *Kigosi,* mle utakutana na sungura na nyoka tu, hata swala hakuna, wala simba hakuna, lakini pale kuna madini ya dhahabu. *STAMICO* wamepewa leseni wanatakiwa wachimbe madini yale, lakini ukienda *TANAPA* ni wagumu utafikiri ukipeleka *grader* mle linamaliza miti yote linaifyeka wakati unachimba kwenye kaeneo kadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda muafaka sasa, naishauri Serikali watengeneze mkakati, watengeneze *task force,* watengeneze Mwongozo ili uweze kuja na mbinu nzuri za kuweza kuchimba madini kwenye hifadhi, hata yale madini ya *Emerald* kule Mayoka kwenye Hifadhi ya Manyara, madini yale yachimbwe yaweze kufaidisha Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, Mbunge. Wakati huo Mheshimiwa Charles John Paul Mwijage, Mheshimiwa Ali Hassan Omar na Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi wanajiandaa.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa fedha nyingi sana ambazo zimeletwa katika Wilaya yetu ya Biharamulo, lakini pia ziara mbili alizozifanya mwaka jana 2022 mwezi wa Sita na mwezi wa Kumi katika Wilaya yetu ya Biharamulo na akapata nafasi ya kuongea na wananchi katika maeneo ya Biharamulo Mjini na Nyakanazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita kwenye mambo mawili siku ya leo. Jambo la kwanza ni mipango bora ya matumizi ya ardhi, ili kuondoa migogoro kati ya wafugaji na hifadhi zetu za Taifa, halikadhalika wafugaji na wakulima; na wakulima na hifadhi. Jambo la pili, nataka niongelee habari au njia bora ya kuzuia wizi au ubadhirifu kwenye miradi ya umma au miradi yetu inayotekelezwa na Serikali. Ni mambo mawili nataka niyaongelee kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na suala la mipango bora ya matumizi ya ardhi; kwa muda mrefu sana wakulima wa nchi hii au wafugaji wa nchi hii wamekuwa kama watu ambao hawana sehemu ya kukaa. Sasa tulizoea ugomvi kati ya wafugaji na wakulima, lakini leo hii tunashuhudia ugomvi kati ya wafugaji na Serikali yao kupitia *TANAPA* au kupitia *TFS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaotoka maeneo haya yenye hifadhi wafugaji wa nchi hii wanapata tabu sana. Wafugaji wengi sana wamefilisiwa. Kila ng'ombe anapokamatwa anatozwa shilingi 100,000 kwenye yale maeneo. Mimi si-*support* watu kuingiza ng'ombe mle, lakini wafugaji hawa wamedhalilika na wamefilisiwa kwa sababu Serikali haijawawekea mpango bora wa kujua wanafugia wapi? Hii ndio shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaotoka maeneo kama ya Biharamulo, kwa sehemu kubwa; mimi naongea na wananchi wangu na wananipigia simu; na mara nyingi nimekuwa nawauliza, kwa nini mnaendelea kuweka ng'ombe huko wanakamatwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, makundi makubwa ya ng'ombe kutoka nchi jirani yamewekwa kwenye Hifadhi ya Burigi. Sasa wananchi wetu wanapoingiza ng'ombe mle, wanakamatwa, lakini ng'ombe wa wageni wako mle. Hii ni aibu na udhalilishaji wa wafugaji wa nchi hii. Ninachoomba, kama Bunge ni lazima tupate hatua nzuri ya kuwasaidia wafugaji wa nchi hii. Hatuwa-*support* kuingiza mifugo kwenye hifadhi, lakini tuje na mpango bora wa kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri wewe ni Mwenyekiti wa Kamati yangu ambayo ninatoka na Kamati ya Mifugo iko chini yako. Tulipata ripoti kutoka kwa Waziri wa Mifugo, *a very good report* kwamba wanao mpango wa kuleta majani kutoka nje ya nchi waanze kuotesha kwa ajili ya kuwasaidia wafugaji wa nchi hii, lakini wanasaidia wafugaji wangapi? Anayejua ng'ombe wa Biharamulo ni wangapi? Ng'ombe Mufindi ni wangapi? Hatujafanya sensa ya kujua idadi ya mifugo kwenye nchi hii. Sasa naomba hili jambo lifanyike, tujue idadi ya ng'ombe kila eneo na Serikali itusaidie kutenga maeneo kwa ajili ya wafugaji. Halikadhalika, hata ng'ombe ambao tunasema, ni nani anayeweza kuwa-*identify?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumeanza mnada wa kuuza ng'ombe *live*. Huko ng'ombe wanakopelekwa, ng'ombe wetu hawana alama wala hawana *identification*. Tulijaribu kuongelea *issue* ya alama hapa ya kuwawekea sijui imepotelea wapi? Matokeo yake tutaenda kwenye mnada wa dunia unapeleka ng'ombe kule, wenzetu tunawajua, hata maparachichi yalivyokuwa yanakuwa mabovu kule watasema yametoka Tanzania. Kesho utapeleka ng'ombe pale anaonekana ana ugonjwa katoka sehemu nyingine, kwa sababu hawana alama, watasukumia, watasema ametoka Tanzania. Kwa hiyo, kesho na keshokutwa, hata kizuri ambacho tunakifanya kwenye soko kitaharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba hilo tusaidiwe, ng'ombe wafanyiwe *identification,* pia maeneo yatengwe, na hayo majani yatakapokuja, watu tuwe tunajua, tunapata majosho mangapi kwenye maeneo yetu? Tunapata mabwawa mangapi ya kunyweshea ng'ombe? Halikadhalika, hata hayo majani yaje yaoteshwe. Wafugaji wako tayari kutoa hata pesa kuliko kuhangaika na makundi ya ng'ombe watoke Biharamulo wayapeleke Sumbawanga. Wako tayari kutoa pesa hata hayo majani yakioteshwa ili waweze kuyapata kwenye maeneo yao. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hilo liangaliwe kwa ajili ya kulinda wafugaji na kulinda hii mifugo tunayoiuza nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 18/09/2021 Mheshimiwa Waziri Mkuu alitembelea Biharamulo, akafanya mkutano pale kwangu Nyakanazi. Nakumbuka kwenye mkutano ule wananchi wa Nyakanazi walimwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu eneo la kulima. Kuna *Swamp* pale kwenye eneo la *TFS,* wakawa wameomba na Waziri Mkuu akatoa maelekezo kwamba, Waziri wa Maliasili, aliyekuwepo wakati ule aje, nami nikamjulisha, lakini *as I am speaking today,* hakuna Waziri aliyekanyaga Biharamulo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba, kuheshimu maelekezo aliyotoa Waziri Mkuu tarehe 18/09/2021, naomba Waziri wa Maliasili na Utalii afike Biharamulo, aongee na wananchi wale wa Nyakanazi awaambie lile eneo linapatikana au halipatikani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kibaya sana, kitu kibaya mno, Maaskari wa *TFS* walioko maeneo ya Nyakanazi kwenye ule msitu wetu pale, wamekuwa wanawalaghai wananchi wa Biharamulo, wanawalipa pesa, wanaenda wanalima kwenye hifadhi, muda wa kufanya mavuno unapofika, wale Maaskari wanawakamata wale wananchi na yale mavuno wanayachukua. Huo ni udhulumishi na udhalilishaji wa ajabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kabla ya kumaliza bajeti hii, Waziri Mkuu atakapokuwa ana-*wind up* tupate majibu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. *ENG.* EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ulinde muda wangu. Maana nadhani Mawaziri wanayo nafasi ya kujibu hoja zetu.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba tu nimpe Taarifa Mheshimiwa Mbunge wa Biharamulo kwamba, Wizara ya Maliasili na Utalii na Utalii imekasimiwa madaraka na Serikali kusimamia maeneo yote yaliyohifadhiwa. Kazi kubwa kwetu ni kulinda na kuyahifadhi hayo maeneo. Linapofika suala la kuomba eneo, tunawaomba wananchi wanaandaa vikao, wanakuja

wanaleta-*proposal* yao, tunaiangalia kama itawezekana. Kwa sababu, tunapolinda tunaangalia mambo mengi, kuna masuala ya shoroba, kuna masuala ya maeneo ya mtawanyiko, kuna mandhari ambazo tunazitunza kwa ajili ya faida ya wananchi wao wenyewe walioko katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unapoomba usitarajie wakati wowote utapata. Ni pale ambapo tutaona: Je, kuna umuhimu wa kulitoa hilo eneo ama la?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, maeneo tunayoyahifadhi sisi ni kwa ajili ya faida ya wananchi wenyewe pamoja na Watanzania wote na siyo ya maliasili na watumishi wake peke yake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Ezra unapokea Taarifa?

**MHE. *ENG.* EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa siipokei. Mimi nawakilisha wananchi wa Biharamulo, ningeomba nisikilizwe hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sipingani na Serikali, na sijasema wananchi waingize ng'ombe au wafanye kazi kwenye hifadhi. Nilichokisema hapa, kitendo cha askari kuwaambia wananchi wakalime kwenye hifadhi, wakampa pesa akawaruhusu wakalima, kesho wakati anaenda kuvuna wakamkamata, *that is insubordination* kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawana maeneo. Tunapoomba maeneo kwa Serikali hapa, Waziri umekaa hapa, watakuletea taarifa walioko kule *site.* Aliyeko *site* kama anafanya bishara ya kuwakodisha wananchi pale, anawadhulumu ardhi, kesho utamwuliza akupe ushirikiano? Hicho ndicho ninachokitaka. Sitaki wananchi wakalime mle

bila kibali, lakini ninachotaka, wananchi watendewe haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeomba ardhi, Mheshimiwa Rais tarehe 16 akiwa Nyakanazi nilisimama nikaomba, tumeshawasilisha, Mkoa wa Kagera umeleta, Serikali inafanyia mchakacho, lakini kipindi inafanya mchakato wananchi hawa wasiumizwe na watu wenye uchu kwa kuwadanganya halafu baadaye wanawadhulumu ardhi yao. Hicho ndicho ninachokisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameniwahi, sijasema wananchi wakafanye…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ezra, unaweza kukaa pale tu nikiruhusu taarifa. Taarifa hizi zinakula muda wako. Kwa hiyo, endelea kuchangia mpaka itakaponipendeza. *(Kicheko)*

**MHE. *ENG.* EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *Anyway,* sasa hilo la hifadhi nadhani limesikika, limeeleweka, naomba mlifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili, naomba unilinde muda wangu maana nimekalishwa mara nyingi hapa. Sehemu ya pili, nilikuwa nataka kuongelea njia bora ya kuzuia wizi na ubadhirifu katika miradi ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni shahidi, tumesema tusiongelee habari ya Ripoti ya *CAG* hapa kwa sababu muda bado, lakini ukweli ni kwamba, wananchi wa nchi hii kinachoendelea kila mmoja anakijua. Kwenye vijiwe, kwenye mitandao na kila maeneo, kila mmoja anajua yaliyofanyika na kila mmoja anajua yanayoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wangu nilitaka niseme jambo moja, kidogo nina uzoefu kwenye hii miradi. Kinachofanyika hapa kwenye Ripoti ya CAG…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Naomba uhitimishe Mheshimiwa Ezra, dakika zako zimeisha.

**MHE. *ENG.* EZRA J CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kengele ya kwanza.

**MWENYEKITI:** Haya, nakuongeza dakika moja nyingine.

**MHE. *ENG.* EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haitanitosha, naomba nihitimishe.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Haya, tunaendelea na Mheshimiwa Charles John Paul Mwijage, kama nilivyokuwa nimemwita.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kujadili bajeti na hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inaakisi sawasawa hali halisi ilivyo nchini au tulikotoka. Mahususi kwangu, aya ya 62, Mheshimiwa Waziri Mkuu ametamka kazi nzuri ya mpango wa Serikali kujenga Soko la Kimataifa la samaki katika bandari ndogo ya Kyamkwikwi. Napenda nichukue fursa hii kushukuru. Namwomba Waziri wa Mifugo asimamie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo suala lingine dogo la kitaifa linalohusu *pension* za watu waliowahi kuitumikia Serikali. Wako watu walitumikia Serikali, leo wana miaka 70, 90 na wengine 100, lakini ukiangalia *pension* wanayopewa na ukatumia ile *time value of money,* naishauri Serikali

tuwaangalie watu hawa. Hawa watu kwa sababu ya umri, wana magonjwa yanayoendana na umri, lakini mfumo wetu wa Bima ya Afya kama *NHIF,* hawa watu wakienda hospitali bima za afya haziwasaidii. Serikali tuliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msiwe na wasiwasi, hesabu za haraka, hawa watu ni wachache. Mnaweza kuwaongezea. Msiwe na wasiwasi, kwa idadi hawa watu ni wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia uchumi wa dunia na uchumi wa Taifa. Nina hofu muda hautatosha, lakini naipongeza Serikali namna inavyodhibiti uchumi wa Taifa letu. Ukiangalia kwa jirani kunavyofukuta, ukaona nyumbani mmetulia, unaweza kujua kwamba aliyeko jikoni anahangaika kusudi mle. Nitarudi hapo muda ukiniruhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze mambo matatu. Mkoa wa Kagera tumepata mapigo matatu. Nasimama hapa kuwaeleza mila za kiafrika. Unapopatwa na shida au kama una shughuli, watu wakija kwako kukuona, inakupa faraja. Ilipoanguka ndege ya *Precision* Serikali kwa nguvu zote ilifika Kagera, Mheshimiwa Waziri Mkuu ulikuja Kagera; hilo jambo liliwafurahisha watu wa Kagera na Watanzania wote. Tunachoomba, Waziri wa Uchukuzi, imeanguka ndege ni historia, lakini lazima tujenge uwanja wa ndege Kagera, Bukoba, utakaoweza kusaidia Soko la Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kagera tuna soko la ndege, *economically* ni *viable,* lakini uwanja wa ndege Kagera ni suala la kiusalama. Kwa hiyo, mnaweza mkaangalia Omukajunguti, na Kashaba. Naomba pamoja na pole mliyotupa, tuliangalie na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni ugonjwa uliotukumba juzi, *Marburg.* Napenda niwahakikishie, mimi nimezungumza na wahusika, nimezungumza na Mbunge

mwenye Jimbo, Mheshimiwa *Advocate Captain Pilot* Rweikiza, Marukuni shwari, Kanyangereko ni shwari. Eneo lote liko shwari, lakini jambo la muhimu kwa wananchi wa Kagera, *response* ya Wizara ndiyo iliwafurahisha. Ujio wa Naibu Waziri na kufuatiwa na Mheshimiwa Ummy, ndiyo jambo liliwafurahisha, lakini zaidi namna Serikali ilivyoweza kudhibiti ugonjwa ule. Nchi nyingine bado ugonjwa unaendelea na limekuwa dondandugu. Katika mambo ya kujivunia tujivunie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa zaidi ya hayo, tunaiomba Wizara: Moja, mjenge hospitali kubwa ya rufaa Kagera ya kudhibiti milipuko. Hii milipuko nimemwambia Waziri, ilikuja Juliana ikaua watu, ni mlipuko; ukaja ugonjwa wa *Covid,* ukaua watu, kwa hiyo, umekuja na huu *Marburg* umeua watu, ijengwe hospitali ya kimkakati, *special* yenye eneo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza na Waziri, sisi tunapakana na ziwa. Karibu 1/3 ya Ziwa Viktoria liko kwetu na tunapakana na nchi nyingi, kuna mwingiliano. Kuna namna ya kutuangalia kipekee. Katika kata tano za Wilaya ya Muleba kututengenezea vituo vya afya vya kuweza kukabili mapigo haya. Nimeomba na ninadhani Serikali mmenielewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende suala la tatu. Desemba tarehe 17, timu ya Mawaziri ilifika Wilaya ya Muleba. Katika timu hiyo Waziri mwenye dhamana ya mifugo wakati ule na wenzake alioambatananao, namwona Mheshimiwa Silinde, Mheshimiwa Mavunde, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, walikuwepo; wakatamka kwamba, uliokuwa mgogoro wa Rutoro umekwisha kwa sababu, mgogoro ulikuwa kati ya *NARCO* na wananchi, umekwisha. Serikali itakuja kupima, lakini wakaenda mbele wakasema watu wakae bila kuhasimiana, tukamaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali yangu, msisubiri kuja kunipimia, mtupimie leo ikiwezekana kesho. Iddi yangu ninayoweza kuipokea, futari yangu inayoweza kunishibisha ni kwenda kuwapimia watu wangu leo. Watu wangu wanateseka, wana-Kagera wanateseka. Aliyozungumza Mheshimiwa Ezra pale, amezungumza kidogo; kuitendea haki sekta ya mifugo, sekta ya ardhi, sekta ya uhamiaji Kagera, ni kuunda tume huru iende ikaangalie watu wanapigwa katika nchi yao, watu wanabakwa katika nchi yao, mashamba yao yanaharibiwa. Mimi nitakuwa mgeni wa nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile *clip* mliyoiona ya kuuaa kwa Aspro, Katibu wa Chama cha Mapinduzi, ilikuwa *edited*. Ukiuona mkanda mzima unaweza ukakubaliana nami kwamba, Mheshimiwa Mwijage tukapime Rutoro kesho, tukamalize mgogoro wa Rotoro keshokutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema Mwijage mimi vile ni vijiji na hati za Serikali ninazo hizi. Anatoka mtu, eti ni mteule, anasema pale sehemu ya kuchunga ng'ombe, ndipo hapo tunapoachana. Na kwa umri huu siwezi kuogopa kutofautiana na mtu mimi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema ile ni sehemu ya Serikali na Waziri anasema kwamba pale watu wakae, anatoka mtu anasema mimi sijapewa barua; upewe barua zaidi ya hii? Serikali imeandika yenyewe kwamba hapa watu wanapaswa kukaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba – hayo Mungu atatulipia mbinguni – ninachomba, wale watu ni maskini, nendeni muwapimie ardhi yao. Mtu aende aseme *communal land. What does communal land mean?* Wale ndiyo nchi yao, hawana kwao kwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inauma, mtu yuko kwao anapigwa na mtoto wa jirani, unasikia mtoto wa jirani anampia mtoto wako kweli utalala? Watu wanasema Mwijage ni kichaa. Itakuaje wewe umelala na mkeo, mtoto anapigwa na anayempiga anazungumza lugha ya mwezini; unalala baba usingizi unakuja? Na mnaamshana na mkeo wakati watoto wanaumia, haiwezekani. Mtoto wa mjomba nenda kalelewe ujombani, lakini ukifanya shari ujombani watakwambia wewe siyo mtoto wa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mtusaidie. Na zaidi katika hayo, nimesikia watu wanazungumzia kufuga, kufuga kuna tija. Ninaomba muitumie Kagera kama *model* ya kufuga, siyo kuchunga. Mwenyekiti ni dhamana yako, uje unite nikueleze. Tuanzie Kagera, hii biashara tunayofanya tunapoteza muda. Anza kufuga kuanzia Kagera mkiiga mfano wa Mbarara. Hatuwezi kuchunga tukaweza kuingia kwenye soko la dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo futari yangu na *Eid al-Fitr* naomba tuandamane twende kwenye vijiji vyangu vinne mkavipime, wananchi watajijua. Nilikuwa nimewaombea chakula, sasa naomba muwapimie wakajilimie wenyewe watavuna wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Charles John Poul Mwijage kwa mchango wako. Nilimuita Mheshimiwa Hassan Omar King, wakati huo Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi anajiandaa.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, awali ya yote kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na kutujalia leo kuja kukaa hapa kujadili bajeti ya kuendesha nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi. Kuna mambo hapa yalisemwa na wengi walizungumza toka tumeanza Bunge hili kuhusu Ripoti ya CAG. Sitozungumza, ila nina shairi dogo ambalo lilitungwa na Haji Gora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Haji Gora alisema kwamba;

Kuna la ajabu mno la kushanagaza moyoni,
Kuna wakongwe watano wanashindana kwa fani,
Wakata mawe kwa meno na kujaza matumboni,
Nasema kinaganaga mengine yasikieni,
Farasi kula mizoga na kufukua mavani?
Kuna kijungu cha kuaga bila moto jikoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye agenda hiyo nimemaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakuja katika agenda na mchango wangu wa Fungu 65 – Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu. Hapa nazungumzia vijana na ajira. Tatizo la ajira ni kubwa kwa dunia nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa Mwalimu tatizo la ajira lilikuwepo, wakati wa mzee Mwinyi tatizo la ajira lilikuwepo, wakati wa Benjamin Mkapa tatizo la ajira lilikuwepo, wakati wa Jakaya Kikwete tatizo la ajira lilikuwepo, wakati wa Magufuli tatizo la ajira lilikuwepo na sasa wakati wa mama Samia tatizo la ajira bado lipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Serikali yetu tukufu ilifanya utafiti na utafiti huo iliufanya kuangalia nguvukazi ya nchi ambapo tuna nguvukazi ya watu 23,536,000 na zaidi. Lakini ilivyofanya hapo iliangalia hali halisi ya soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti hiyo ilionesha kwamba asilimia takribani 80 ya nguvukazi ya Tanzania ujuzi wao uko

chini; asilimia 16.6 ya nguvukazi ya Tanzania ujuzi wao ni wa kiwango cha kati; asilimia 3.6 ujuzi wao ni wa kiwango cha juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi kwa kuwa ni nchi ya kiwango cha kati tulitakiwa asilimia ya kiwango cha juu iwe asilimia 12; asilimia 34 iwe ya kiwango cha kati na asilimia ya kiwango cha chini iwe 54 kwa kuwa tupo katika uchumi wa kiwango cha kati. Hii ilifanya ndiyo chimbuko la kuwa na programu ya kukuza ujuzi kwa ajili ya kupata ajira. Kwa bahati tukaweka hiyo programu, programu hiyo na *components* zake za kukuza ujuzi zikatajwa na iko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walikubaliana sekta binafsi na Serikali kwamba programu hii ambao ni Mradi Namba 6581 itasimamiwa na *SDL (Skills Development Levy),* kwamba *one-third* itatoka itakwenda kushughulikia tatizo la kukuza ujuzi kwa vijana. Na kukuza ujuzi kwa vijana maana yake tutapata tija kwenye bidhaa zetu na ajira zitazalishwa kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Skills Development Levy* iliyokusanywa kwa mwaka 2021/2022 ilikuwa bilioni 291, ambayo *one-third* yake ilikuwa bilioni 97, lakini kwa bahati utekelezaji wa programu hii ulivyokwenda, ilianza kuchangiwa kwa bilioni 15, tukaja bilioni 18 na sasa hivi tumeshuka tuko katika bilioni tisa. Tunajiuliza, je, tatizo la ajira kwa vijana liliisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa nataka niseme neno; na ninataka nitoe rai; Mwenyezi Mungu anasema kwenye *Quran* Tukufu *fama amali Musa illa dhuriyya.* Musa hajaaminiwa isipokuwa walibakia vijana watupu ndio waliomuamini Musa na niyo waliomfuata Musa. Lakini wazee wote waliogopa kwa sababu ya kumuogopa firauni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hawa vijana ambao sisi tunaanza kuwashushia hata hiyo pesa kwa ajili ya wao kupata ajira na kukuza ujuzi, tutakimbilia wapi? Serikali lazima itazame katika hili. *SDL* inatakiwa ipelekwe bilioni 97, sasa kama bilioni 97 haikupelekwa, je, hawa vijana tunawapeleka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo langu; *SDL* kama haijatoka kwa kiwango cha kutosha kama tulivyosema huku katika makubaliano, kwamba *one-third* ya *SDL* iende kwa ajili ya ajira na mafunzo kwa vijana ili kukuza ujuzi, hapa nina lengo la kuzuia shilingi kwa sababu vijana ni tatizo kubwa. Leo tutazame matatizo yote lakini bomu kubwa ni vijana. Sasa kama hatujawaangalia vijana tutaangalia kitu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema kukuza ujuzi kwa vijana, kama hawajakuziwa ujuzi wao ina maana kwamba bidhaa zetu na vijana tatizo hatutoweza kulipatia ufumbuzi. Hii naomba tuweke kwenye *Hansard,* nakuja kuzuia shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumza Mheshimiwa Mwijage kwamba kuna wazee ambao wamestaafu pensheni zao ni ndogo, malalamiko yao ni kwamba ile sheria iliyotungwa haifuatwi. Na maombi yao wanasema Serikali iunde *Task Force* kwa ajili ya kufuatilia tatizo la pensheni zao. Na wanaomba hii sheria basi, kwa zile changamoto zao, ikifuatwa hii sheria watakuwa wako sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika Jimbo langu la Jong'ombe. Niliahidiwa kupata skuli pale katika Shehia ya Kwalilatu kupitia *TASAF*. Lakini mpaka sasa hivi tunakwenda kumaliza bajeti hatujaona. Wananchi wamepita wamehojiwa, taratibu zimefanyika. Nilizungumza na Mheshimiwa Jenista wakati ule alisema atakuja yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali katika kipindi hiki ambacho kimebaki kwa kuwa jambo lilikuwepo katika mchakato, tunaomba tumalizie hili jambo ili kuweza kuwa-*accommodate* na kufanya lile jambo. Na mimi jamani mwenzenu nahitaji kura za kutoka kwa wananchi ili niweze kuja hapa. Kwa hiyo, jambo moja katika jimbo langu ni jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuzungumzia agenda yangu muhimu ile ya kwanza ya vijana. Endapo Serikali haitofanya, haito-*ringfence* watuambie mbinu gani watatumia, wata-*ringfence* lakini fedha *at least* zipatikane bilioni 36, vinginevyo Waheshimiwa Wabunge hakuna mtu ambaye hana tatizo la ajira katika jimbo lake. Tunafuatwa na wananchi. Nitaomba mje mniunge mkono wakati huo kwa sababu ya kuwasemea hawa vijana. Kama siyo hivyo ina maana kwamba tutawatelekeza vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa vijana wakiamua kufuata njia nyingine tutawafanya nini? Na ukimuona kijana kapata kitu sehemu nyingine mtakuja kusema vijana wanaharibika, lakini itakuwa kuharibika kwenu, kwa wenzenu watakuwa wametengemaa maana watakuwa wanawatumia wao. Sasa ili tuwatumie vijana wetu tuwajali katika ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Lakini pamoja na yote nitakuja kuzuia shilingi katika suala hili la *SDL.* Naunga mkono hoja; nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ali Hassan Omar King pia kwa kuzingatia muda vizuri. Nilimuita Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, wakati huo Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Dkt. Alice Kaijage, Mheshimiwa Tarimba Abbas na Mheshimiwa Salome Makamba wanajiandaa.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ili kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Bukene niweze kuchangia hotuba hii muhimu ya Ofisi ya Wairi Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia uhai na uzima ambao umetuwezesha kusimama hapa na kufanya jambo hili muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri; vilevile niwapongeze Wenyeviti wa Kamati za Bunge zote ambazo zinasimamia ofisi hii kwa kuwasilisha hotuba nzuri za taarifa za Kamati zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, kama ambavyo Wabunge wenzangu wamefanya, nitumie nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa fedha nyingi sana ambazo amezileta katika Jimbo la Bukene kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea fedha nyingi kwenye miradi ya maji, sasa hivi tunayatoa maji Nzega Mjini kuyafikisha Bukene, zaidi ya bilioni 24 na bilioni sita zimeshatoka; kuna fedha nyingi sana za miradi ya umeme, miradi ya barabara tunapasua barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee pia niipongeze Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, kwa mradi mkubwa sana wa mazingira ambao tumeupata pale kwenye Kata ya Sigili, Wilaya ya Nzega ambako jumla ya bilioni 2.5 zitatumika katika kujenga visima, maghala na mashine ambazo zitaongeza thamani ya mazao yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia; jambo la kwanza ambalo ninapenda kuongelea; niombe Ofisi ya Waziri Mkuu ifanye *coordination* kati ya Wizara ya Nishati na Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale jimboni kwangu kuna mradi mkubwa wa bomba la mafuta yanayotoka Uganda kwenda Chongoleani, Tanga. Na ndani ya mradi huo pale jimboni kwangu kuna mradi mkubwa sana wa kujenga *coating yard*. Yadi ambapo mabomba yote yatakayolazwa kutoka Uganda mpaka Tanga ndipo yatakapopakwa rangi maalum ili yatakapofukiwa chini yasioze. Ni mradi mkubwa mno wa zaidi ya bilioni 600; ni mradi mkubwa mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naiomba Ofisi ya Waziri Mkuu iwakutanishe Wizara ya Nishati na Ujenzi kwa sababu ilivyo sasa kila Wizara naona inafanya jambo lake kiutofauti. Wizara ya Nishati inaendelea kusimamia ujenzi wa yadi hii kubwa, ujenzi unaendelea vizuri. Lakini hata yadi hii ikikamilika hayo mabomba hayawezi kufika pale ili kupakwa hiyo rangi maalum kwa sababu hakuna barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara inayopita kwenye mradi huu ni barabara ya vumbi, ya changarawe, nyembamba, haina madaraja. Na mzigo unaopaswa kupitishwa kwenye barabara hiyo wa mabomba ni mzigo mzito, mkubwa sana. Mzigo wa mabomba zaidi ya tani 270,000, mabomba 86,000. Na kuna *special trucks* ambazo zimeshakodiwa, magari maalum zaidi ya 300 yatakuwa yanapishana kila siku. Kwa hiyo, barabara ilivyo sasa hivi huu mzigo hauwezi kupita na kufika pale *coating yard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sijaona kama Wizara ya Ujenzi inaona umuhimu huo wa kuishughulikia barabara hii kwa sababu tangu miaka ya fedha miwili iliyopita ilishafanyiwa upembuzi yakinifu, ilishafanyiwa usanifu wa kina

lakini miaka yote inapata fedha kidogo sana ambazo hazitoshi hata kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Meneja wa *TANROADS* Tabora ameshaandika barua kwa Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi kuomba kibali aruhusiwe kutangaza na Wizara impe fedha ili ujenzi uanze. Kwa hiyo, ninaona nishati wanafanya kazi kivyao na Wizara ya Ujenzi nao kwa upande wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Ofisi ya Waziri Mkuu iwakutanishe kutokana na umuhimu wa mradi huu basi hicho kipande cha barabara kutoka Nzega ambako lami inaishia kupita Itobo mpaka Sojo ambako ndiko *coating yard* ilipo kiweze kujengwa kwa kiwango cha lami ili kupitisha mzigo mkubwa huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu usalama wa chakula. Kabla ya msimu huu wa mavuno tulionao hapo nyuma tulipatwa na upungufu mkubwa wa chakula ambao ulisababisha bei ya mahindi kupanda sana, ilifika mpaka 22,000 mpaka 23,000 kwa debe, lakini niipongeze Serikali ilituletea mahindi kutoka *NFRA* ambayo yalikuja kupunguza makali ya bei kutoka 22,000 kwa debe mpaka 14,000 na ambayo ilisaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ili kuondokana na tatizo hili, uwekezaji kwenye miradi ya umwagiliaji haukwepeki. Ushauri wangu; ni lazima tuongeze fedha ili tuweze kujenga miradi ya umwagiliaji, tuisimamie ili tuweze kujinasua na suala hili la kila mara upungufu wa chakula kwa sababu mvua zenyewe kutokana na mabadiliko ya tabianchi haziaminiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwenye jimbo langu kwenye Kata ya Kahama Nhalanga kuna mradi wa umwagiliaji ambao Serikali ilitumia zaidi ya bilioni moja kuujenga. Lakini mradi huu kimsingi haufanyi kazi. Miundombinu ya mashambani imeharibika, tuta limepasuka

na bilioni moja zilishatumika lakini ile tija na tulichotegemea kupata hakipatikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ungeweza kumwagilia hekta 1,000, karibu ekari 2,500, tungeweza kupata zaidi ya tani tano za mpunga, lakini haufanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza kwamba sasa hivi Serikali imepeleka ma-*engineer* wa umwagiliaji kila wilaya ili skimu za umwagiliaji ziweze kusimamiwa. Kwa hiyo, napongeza hatua hii ya kuwekeza, lakini lazima tuwekeze kwenye miradi ya umwagiliaji ili tuondokane na tatizo la upungufu wa chakula wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwamba tumepata mradi mkubwa wa umwagiliaji kwenye Kata ya Sigili, Kijiji cha Lyamalagwa, Bonde la Mto Manonga ambako zaidi ya hekta 3,000, kama ekari 4,500, ambazo mkandarasi wa kujenga bwawa ameshapatikana na zaidi ya bilioni 11 zitatumika ili kujenga skimu kubwa ambayo tutaweza kumwagilia zaidi ya ekari 7,500 ambayo itatupatia mazao ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hayo ni maeneo mawili ambayo ninaomba kusisitiza na kushauri ili tuweze kuondokana na tatizo la upungufu wa chakula ambao unasababisha kupanda sana kwa bei ya chakula kama ambavyo tume-*experience* miezi miwili, mitatu iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia 100. Nashukuru sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zedi kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali. Wakati huo Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage anajiandaa.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, na nikuombe tu niende moja kwa moja kwenye hoja. Na hoja yangu itahusiana na maadili *(LGBTQ)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tuna Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Chombo hiki ni cha Kikatiba. Kimeanzishwa na kimetajwa katika Katiba, Ibara ya 131(1)(2).

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha kabisa ni kuona kwamba chombo hiki ambacho ndicho chenye haki ya kutupa taarifa za uhakika kimedharauliwa, hakifanyi kazi, kimekaa tu kinatoa taarifa ambazo zinamalizia huko. Kwa mujibu wa Katiba, naomba ninukuu, Ibara ya 131(3)(b) inasema;

(3) Kila mwaka wa fedha Tume itatayarisha na kuwasilisha kwa Waziri anayesimamia haki za binadamu taarifa kuhusu-

(a) shughuli za Tume katika mwaka uliotangulia;

(b) hali ya utekelezaji wa hifadhi ya haki za binadamu katika Jamhuri ya Muungano,

Na Waziri atawasilisha mbele ya Bunge kila taarifa iliyowasilishwa kwake na Tume mapema iwezekanavyo baada ya kuipokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu 2011 taarifa haijawasilishwa na sijui kama inafika kwa Waziri. Tume inatoa taarifa lakini taarifa ile inakaliwa, haiji. Maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba hali iliyokuwepo Tanzania kuhusu haki za binadamu ni mbaya kuliko tunavyofikiria lakini hatupati taarifa. Eti leo tunategemea taarifa kutoka kwa *NGO* tunategemea taarifa kutoka kwa mtu atuelezee habari ya *human right* katika nchi yetu? Haiwezekani. Sasa, kama hatuitaki Tume basi tuifute. Tume haina wafanyakazi, haina

bajeti, bajeti yake ndogo sana, haiwezi kufanya chochote, na tumeianzisha kikatiba kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kwanza ni kuvunja Katiba lakini pia kuvunja katiba ibara ya 18(2) kwa Tume kushindwa kutoa taarifa zinazoendelea kwa wananchi. Kwa wale wenye watoto nje ya nchi Amerika au Ulaya au Asia, kumlea mtoto nje ya nchi siku hizi ni bora na ni salama zaidi kuliko kumlea katika nchi yetu ya Tanzania. Hii ni kwa sababu watoto wa nje ya nchi wanaharibika, Ulaya na Amerika, sisi watoto tunawaharibu. *Style* ya maisha yetu ya kuishi, tutaishi na jamaa ndani ya nyumba huyu mjomba, kaka, shangazi, sijui nani, wale ndio wanaoharibu Watoto. Tume inaripoti kuhusu jambo hili na hizi ripoti hazitolewi kwa sababu wazee wenyewe wanaficha ripoti kwa sababu wanaona aibu, lakini hali ni mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu inashangaza, zamani ilikuwa kumtwaza mwanamke taabu sana, mpaka uandike barua, mwalimu aikamate, taabu sana. Siku hizi unapeleka simu unawekewa namba lakini zamani vitendo hivyo vilikuwa hakuna, leo vitendo hivyo vinatokea wapi? Na bado tume tumeitelekeza; hili sio jambo jema. Niombe Serikali kwamba, kwa hali ilivyo mbaya ni bora tuache taarifa ya *CAG* tusome taarifa ya Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili niseme kuhusu Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Tumeanzisha hiyo Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali lakini ipo chini ya Wizara. Tunashukuru Serikali imepeleka fedha kule kiwanda cha Dodoma, bilioni nane, vilevile tumepeleka kama bilioni sita kwa ajili ya kununua mashine. Sasa hawa watu lazima wawe wakala, lazima wajitegemee. Huwezi ukapeleka pesa ukaanzisha hiyo biashara halafu wakategemea *OC* kipuri kikiharibika wasubiri miezi mitatu wamemuandikia Katibu mkuu. Nafikiri tuuharakishe mchakato unaoendelea ili kumfanya huyu Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali awe wakala, na pia tumpe

mapato na watumishi ambao wanaweza kufanya hiyo kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana; wakati wa ziara ya Kamati tulivyokuwa tukienda kukagua miradi. Jengo la Msajiri wa Vyama vya Siasa ambaye anasajiri chama cha kisiasa kimoja kwa miaka mitano linajengwa kwa bilioni 20. Kwa hiyo jengo linajengwa kwa bilioni 20, kwani bilioni mbili haiwezi kujenga jengo? kwani bilioni tano hawezi? Jengo la TAKUKURU ni bilioni 24; tunaharibu fedha za Serikali badala ya kuziweka katika mambo ya maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda kile ambacho ni cha Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kinatumia bilioni nane tu, na mashine yake ni bilioni sita tu lakini ita-*generate fund* kwa bilioni 20 kwa mwaka. Lakini pia kama tutakiwezesha vizurini zaidi ya bilioni 40 hapo itafanya asilimia 55, lakini leo unachukua fedha unazipeleka kwa mtu anakaa na kiyoyozi anasajiri chama cha siasa, sijui anafanya nini, haiwezekani. Hatuwezi kutumia hivyo fedha za Serikali, fedha za Serikali lazima zitumiwe kwa utaratibu, kwa utaratibu huo hauelekei kama sisi ni nchi maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna majengo hapa yamejengwa kwa bilioni 100, tunayajua sasa haiwezekani. ingekuwa jengo hilo linajengwa ndani yake lina biashara hiyo sawa, lakini halifanyi biashara, jengo limekaa tu halafu nani ataliendesha? Halafu sie tupitishe bajeti hapa tukaliendeshe tena hilo jengo la bilioni 20 pamoja na *maintenance* yake, tupitishe hapa likafanye kazi? Haiwezekani hizo fedha sisi tuna haribu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ngwali kwa mchango wako. Sasa namwita Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage aweze kuchangia.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahante sana, na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya, lakini pia naungana na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayofanya ya kulitumikia Taifa letu la Tanzania. Pia nampongeza Waziri Mkuu pamoja na timu ya mawaziri katika Sekta ile pamoja na watendaji kwa kazi nzuri wanayofanya kwa Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachangia fungu 65, ilani ya Chama Cha Mapinduzi Ibara ya 168 imeendelea kutambua mchango muhimu sana wa wafanya kazi na vyama vya wafanyakazi na waajiri kwenye uchumi wa nchi yetu. Si hivyo tu, hata kwenye hotuba ya Waziri Mkuu ukurasa wa 65 pia imeeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hayo, haina ubishi kabisa kwamba vyama vya wafanyakazi ndivyo vinavyohusika kuwaunganisha na kuleta *harmony* kati ya waajiri na wafanya kazi. Kupitia mabaraza yao wanajadili mambo mbalimbali ambayo yanawagusa na ambayo yanawasumbua sana wafanyakazi; lakini pia ndiyo *forum* sahihi. Hatutegemei wafanyakazi wakose vikao waende kwenye waandishi wa habari na kwenye *platforms* za siasa zinaendelea sasa hivi kueleza mambo yao; wana mabaraza yao kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nazungumzia hayo? Fungu 65 ndipo mahala sahihi kuhusiana na mambo ya vyama vya wafanyakazi na wafanyakazi. Nashauri, watakapokuja watueleze, kwenye Fungu 65 mpaka sasa, kitengo cha wafanyakazi na vyama vya wafanyakazi kumefanyika nini na bajeti ijayo wanampango gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwa sababu idara ina Idara ya Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi ambaye ndiye anayehusika kwenda kufuatilia masuala mbalimbali na

utendaji wa vyama vya wafanyakazi kule pembezoni mikoani ambako kuna matawi ya wafanyakazi. Kwamba wanaendeshaje mambo yao kutokana na utaratibu na kanuni walizojiwekea. Kama Idara hii ya Msajiri wa Vyama vya Wafanyakazi itakuwa haina baketi itakwendaje kufanya shughuli hizo? Lazima tusikilize matataizo yao na tumuwezeshe Msajiri aende akafuatilie kwenye mikoa na pembezoni, kule ambako kuna matawi ya vyama vya wafanyakazi, akaangalie wanavyofanya kazi zao kulingana na taratibu walizojiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la wakala wa huduma za ajira nchini *(TaESA)*. Hili baraza linahusika na kuwaunganisha watafuta kazi na waajiri. Nipongeze sana Serikali, sasa hivi kupitia ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora imeshirikiana sasa hivi na Ofisi ya Waziri Mkuu kuanzisha Mfumo wa Taifa wa Kusimamia Ajira. Hii itasaidia kwa sababu mfumo huu utakuwa na taarifa za nafasi za kazi zote nchini na utakuwa na takwimu kamili za soko la ajira nchini. Kwa hivyo nipongeze Serikali kujua kwamba kuna umuhimu wa wao kuungana na Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi. Katika muunganiko huo *TaESA* inahusika na suala la usimamizi wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ukoje hapo? Kwamba hii *TaESA* ijulikane, *TaESA* iongezewe nguvu. Kama alivyosema mjumbe mwenzangu, kwenye *Skill Development Leavy* kwenye *SDL* iongezewe bajeti. Hii *TaESA* inahusika kutafuta ajira, inahusika kuwapeleka vijana kwenye mazoezi ya vitendo, lakini bajeti yake ni ndogo na pia haijulikani na haitoki. Watoto hawaifahamu na hata wazazi hawaifahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nipongeze kwamba sasa kuna ushirikiano kati ya ofisi ya utumishi na ajira lakini sasa *TaESA* Ifanye kazi iende ikatafute hizi nafasi, iende mikoani,

kwenye viwanda ikae na waajiri, itapata hizi nafasi kwa hiyo itasaidia kupata nafasi kwa ajili ya wananchi wetu.

Kuna Baraza la Uchumi, na hili baraza liko kwa mujibu wa Sheria. Tunabaraza lingine kwenye hii ofisi linaitwa *LESCO,* hili linaitwa Baraza la Uchumi na Jamii. Baraza hili linaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Waziri wa Kazi, inamshauri Waziri wa Kazi juu ya mambo mablimbali ikiwepo Sera ya Taifa ya Soko la Ajira, njia tofauti mbalimbali za kupunguza ukosefu wa ajira pamoja na pia kutoa takwimu za usimamizi wa sheria ya ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabaraza yote yapo kwenye ofisi, hatusikii kazi zake hatuoni ripoti yake tunakazana kutafuta ajira za vijana. Kama kuna mabaraza yapo kwa mujibu wa sheria yawezeshwe; kama ni bajeti ya *ESDL* iongezwe ili haya mabaraza kwa kusaidiana na juhudi mbalimbali za Rais mpaka analeta mashamba vijana walime basi hayo mabaraza yawe *active,* yaongezewe bajeti yatoke yajulikane yafanye kazi inayotakiwa kufanywa. Wanapokuja watuambie hayo mabaraza yamefanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo nipongeze Serikali kwa kuja na ongezeko la Mshahara wa kima cha chini hasa kwa sekta binafsi. Sensa ya mwaka jana imeonesha kabisa kuwa sekta binafsi ndiyo inayoongeza kuwa na watumishi wengi sana. Sheria ya Kazi inaonesha kwamba Bodi ya Ajira Sekta Binafsi inatakiwa iongezewe bajeti ili tunapopandisha safari hii iwe ndio mwanzo wa mchakato kwa sababu upandishaji wa kima cha chini umechelewa sana. Iwezeshwe, ianze mchakato mapema kwa sababu maisha kila mwaka yanabadilika, kwa hiyo ni lazima kima cha chini kipande kila mwaka. Kwa hiyo Bodi hii iwezeshwe, iongezewe bajeti ili ianze mapema mchakato wa kufatilia kima cha chini hasa cha watu wa sekta binafsi ndio wengi katika utumishi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada hayo nasema naunga mkono hoja ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nilimwita Mheshimiwa Tarimba Abbas wakati huo Mheshimiwa Salome Kamba anajiandaa.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Awali ya yote nipende kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri, hotuba ambayo inaonesha ni kwa jinsi gani Serikali yetu imepiga hatua katika kuleta maendeleo lakini vile vile kuweza kuwasaidia wananchi wake kupata uhuru wa kutosha wa kiuchumi na masuala mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na vile vile nisimame hapa kwa niaba ya Jimbo la Kinondoni na wananchi wa Jimbo la Kinondoni niweze kumshukuru sana na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa yale ambayo ametufanyia sisi wananchi wa Kinondoni. Kinondoni tumepata maendeleo makubwa sana ndani ya kipindi cha miaka miwili. Naamini wengi mlioko humu ndani katika Bunge hili mnaishi au mna ndugu pale Kinondoni; na kwa hali hiyo mnapita na mnaona ni jinsi gani Kinondoni imechangamka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano maeneo mawili au matatu. Kwa mfano kwenye Kata ya Kinondoni ambapo ndiyo kata iliyochukua jina la Jimbo na jina la Wilaya; kata ile katika miaka 60 ya uhuru wetu haijawahi kuwa na *secondary school* ya Serikali lakini safari hii tumepata *secondary school* ya Serikali ya kisasa na watoto wameshaanza kusoma. Vilevile pale hatujawahi kuwa na kituo cha afya wala *dispensary*. Kinondoni sasa hivi ina kituo cha afya cha kisasa ambacho kimejengwa na Serikali na kinapendeza na kina

huduma zote, nipende kuishukuru Serikali kwa ajili hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna barabara nyingi ambazo zimejengwa katika kata ile ikiwemo barabara ya *Best Bite* ambayo kwa miaka nenda miaka rudi ilikuwa ni kero sana. Pia nishukuru Serikali kwenye zile Bilioni moja ambazo Mheshimiwa Rais alizitoa kwa kila Mbunge kwa minajili ya kujenga barabara katika majimbo yetu mimi nimeipeleka kwenye kata moja ambayo ilikuwa haina barabara za lami hasa kata ya Ndugundi tumepata barabara mbili, Mkalamo moja na Mkalamo mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti,vile vile nishukuru Serikali kwa kuangalia suala la mafuriko katika Jimbo la Kinondoni. Mto Ng'ombe umekamilika, na hata mvua za juzi tulikuwa salama sana. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye tulikuwa naye kule kwenda kuangalia, na maelekezo aliyoyatoa yametekelezwa, hivyo hongera sana kwa Serikali kwa kutufanyia jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna suala la Mto Msimbazi, tumelizungumza sana. Napenda nitoe pongezi nyingine kwa Serikali kwamba sasa mradi ule wa kuboresha eneo lile la Bonde la Mto Msimbazi unakwenda kufanya kazi; na tayari tathmini zimefanyika na hivi ninavyozungumza jumla ya nyumba 2,592 zilifanyiwa tathimi na katika nyumba hizo 2,217 wamekubaliana tathmini zile. Isipokuwa nyumba 163 wenye hizo hawajakubaliana na tathmini.

Nilikuwa naiomba Serikali kwa utaratibu uliopo wa Kiserikali uendelee kufanya mazungumzo na wananchi hawa ili nyumba zao ziweze kufanyiwa upya marejeo ya tathmini ili waweze kupata tathmini ambayo inakubaliana na thamani ya nyumba zao ili mradi ule uweze ukaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yote haya kuna matatizo kidogo ambayo ningependa niyaseme. Kwa mfano kwenye Kata ya Kigogo tuna kituo cha afya kikubwa sana ambacho kina hudumia wananchi wa Ubungo na wananchi wa Ilala. Kituo kile kilipelekewa jokofu la kutunza maiti mwaka 2020; na jana wakati nazungumza kuuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya TAMISEMI nilikuwa naiomba Serikali iweze kufanya haraka kulipa fidia ili jingo la kuhifadhi mashine ile ya jokofu la maiti iweze kujengwa na Serikali ikasema na ikaagiza halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni waweze kutenga fedha za kujenga jengo la kuhifadhi jokofu la kutunzia maiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajabu ni kwamba kumbe wakati mimi namaliza kuzungumza lile jokofu limekwenda kuondolewa limepelekwa kwenye Hospitali ya Wilaya Mabwepande. Hiyo hali sikuipenda sana kwa sababu kumbe Waziri ana taarifa nyingine, TAMISEMI kwa maana ya watendaji wana taarifa nyingine, hili jambo si zuri na halioneshi kwamba Serikali ni moja na inafanya kazi kwa pamoja. Huyu anafanya maamuzi yake na huyu mwingine anafanya maamuzi yake, hawaambizani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili si jambo jema kwa utendaji wa Serikali ambayo ina sifa nzuri ya kuweza kuwatumikia wananchi wake. Nitaomba Mheshimiwa Waziri wa *TAMISEMI* au Naibu wake niende naye kwenye Kata ya Kigogo ili aweze kuona jinsi gani hali ile ambayo imefanyika sasa hivi inakwenda kuathiri wananchi. Hii ni hatari kwa sababu maelekezo mengi ambayo yanatolewa hapa Bungeni wananchi wanayachukulia kwa ukubwa wake lakini sasa kama Waziri anasema fedha zitengwe na wakati huo huo mamlaka nyingine zinakwenda kuondoa jokofu maana yake kama vile kuna *crush* kati ya Serikali kuu na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba na mimi nigusie suala hili ambalo linatula vichwa vyetu. Sisi Wabunge ili uwe Mbunge lazima ule kiapo; na katika kula kiapo lazima utashika ima Biblia takatifu ama *Quran* takatifu. Asubuhi kila tunapoanza shughuli za Bunge tunaomba dua na tunamtaja Mwenyezi Mungu hapa na tunamwomba atupe hekima kufanya maamuzi na kufanya mambo mengine. Lakini Mungu huyu tunamchukiza. Mungu huyo huyo ambaye tunamsema kwamba ndiye kiongozi ambaye anatuongoza sisi katika maisha yetu tunamchukiza. Tunamchukiza kivipi? Matendo tunayoyazungumza ya kiushoga ni matendo yanayo mchukuza Mungu. Tumesema kama Bunge; na wananchi huko nje na viongozi wa kidini wanalalamika. Leo asubuhi kwa Waziri wa Elimu kulikuwa na swali ambalo lilikuwa linahusiana na masuala haya ya watoto kuharibika wakiwa *boarding school,* na Mheshimiwa mbunge mmoja alisimama akaomba kwamba je, Serikali haioni uharaka na umuhimu wa kuleta sheria mahsusi? Waziri anajiuma uma anasema watalichukua hilo wazo watakwenda kulifanyia kazi, alah! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unachukua wazo ambalo vitu vinaumiza vichwa vya watu. Jambo hili si la leo, mwaka 1998 kulikuwepo na sheria ambayo ilitungwa *inasema Sexual Offenses (Special Provisions) Act, 1998* maana yake mambo haya yalikuwepo miaka mingi yanasumbua, yalikuwa ni madogo madogo. Hata hivyo Sheria ile haikuja *explicitly,* haiko kwa uwazi kabisa jinsi gani ya kuweza kupiga vita vitendo hivi, ingawa muda…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE.TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie maana yake hoja itakuwa ina-*hang*. Naomba kama haiwezekani kuleta sheria mpya hapa basi ifumuliwe Sheria ya *SOSPA* ya 1998 ili iweze ikakidhi mahitaji ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Baada ya Mheshimiwa Salome Makamba atafuata Mheshimiwa Innocent Seba Bilakwate, Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo na Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris pia watachangia.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwapongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri. Ukisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ukurasa wa 21 na 22, ningependa kujikita hasa kwenye kuboresha mazingira ya uwekezaji na kuboresha mazingira ya wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge mwenzangu Mheshimiwa Mwambe aliomba Mwongozo asubuhi, lakini napenda nikazie hapo kwenye suala zima la kuboresha mazingira ya biashara na mazingira ya wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimuundo na kimfumo Serikali imejipanga vizuri sana kuhakikisha inawalinda wafanyabiashara wanaoendelea kufanya kazi na kuwakuza wafanyabiashara wadogo waweze kuingia sokoni na kushindana kiushindani. Kimuundo Serikali imeweka Tume ya Ushindani wa Kibiashara ambapo mtu yeyote anapodhani kwamba hapendezwi au hafurahishwi na mwenendo wa biashara sokoni kwa washindani wake, anaweza kwenda kupeleka malalamiko au anaweza kwenda kufanyiwa tathimini. Kama hataridhika shauri lake litapelekwa kwenye Mahakama ya Ushindani wa Kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuna jambo ambalo kidogo linaendelea ambalo linaweza kuleta shida kubwa sana ya biashara ya saruji nchini. Mwaka 2022 Kampuni ya *Twiga Cement* iliomba kwenda kununua hisa ya kampuni ya *Tanga Cement*. Baada ya kuomba Tume ya Ushindani

ilikwenda kufanya tathimini kama sehemu ya majukumu yake. Kwa sababu moja kati ya sifa kubwa ya kuweza kununua hisa za kampuni nyingine ambayo mnafanya biashara inayofanana, hautakiwi kununua hisa kwa zaidi ya asilimia 34 ili usije ukalimiliki soko la biashara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tathmini ilipofanyika ya hisa za *Tanga Cement* kununuliwa na *Twiga Cement* ilionekana kuna uwezekano mkubwa baada ya kununua hisa zile, Kampuni ya *Twiga Cement* ingeweza kumiliki hisa zile zaidi ya asilimia 68. Pia Tume ikasema kwa hatari hiyo itaifanya Kampuni ya *Twiga Cement* kuwa kubwa iweze kumiliki lile soko, jambo ambalo lingeweza kuleta madhara kwenye upangaji wa bei kwa sababu yeye ndio mdau mkubwa kwenye eneo hilo. Ingeleta madhara makubwa kwenye upangaji wa bei, ingeleta madhara makubwa kwenye mfumuko wa bei lakini ingeleta gharama kubwa kwa mlaji ambao ni wanunuzi wa saruji yaani sisi wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maamuzi yale yalipotoka hawakuridhika nayo, wakaenda kwenye Mahakama. Mahakama ikakubaliana na maamuzi ya Tume wakasema Hapana, wasipewe kwa sababu watalimiliki soko la *cement* nchini, jambo ambalo linaweza likaleta madhara makubwa kwenye uchumi wa nchi hasa katika eneo la *cement*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Tume imesema, kama Mahakama imeamua, juzi tarehe 23 Februari hapa, Tume imetangaza kwamba *Twiga Cement* wataendelea kununua hisa za *Tanga Cement,* maamuzi hayo wanayapata wapi? Nguvu hiyo wanaitoa wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo madhara makubwa sana. Unajua mpaka sasa hivi tunapozungumza pamoja na viwanda vya *cement* kuwa vingi, bidhaa ya *cement* ina bei ya juu sana nchini. Kuna watu wananunua *cement* mpaka …

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa kutoka wapi.

**MHE. ELIBARIKI KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kingu hapa.

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Kingu utachangia muda si mrefu. Naomba u-*reserve* hiyo taarifa. Endelea Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Yapo madhara makubwa sana ya mmiliki mmoja kuwa na uwezo mkubwa wa kuamua bei, kuwa na uwezo mkubwa wa kupanga manunuzi na usafirishaji wa bidhaa ya *cement* hasa kwa wakati huu ambao nchi ndio inakwenda kujijenga kwenye maeneo ya viwanda, biashara na pesa nyingi za Serikali zinakwenda kwenye miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo inasimamia masuala haya ya uwekezaji, wajaribu ku- kulisimamia hili suala, kwa sababu mwisho wa siku mfumuko wa bei ukitokea kwenye *cement,* madhara ni yale yale ambayo tuliyaona kwenye sukari, kwenye mafuta ya kula na mambo mengine. Kwa hiyo ningeiomba sana Wizara itusaidie, ilimradi maamuzi yameshatolewa na Mahakama njia pekee ambayo *Twiga Cement* au haya makampuni yanaweza kufanya ili kumilikishana *share* ni kuomba marejeo ya maamuzi ya Mahakama ya Ushindani na sio kwenda kufanya ambavyo wanafanya. Kwa hiyo, naamini Serikali makini itakwenda kulisimamia hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nirudi kwangu Mkoa wa Shinyanga. Kitakwimu Mkoa wa Shinyanga unaongoza kwenye unyanyasaji wa kijinsia, mimba za utotoni na ndoa za utotoni. Ningeomba sana Ofisi ya Waziri Mkuu

waifanye Shinyanga kama kanda maalum kwa ajili ya kutekeleza jambo hili. Asilimia 59 ya watoto waliopo Shinyanga wanaolewa wakiwa na umri wa chini ya miaka 18 na sielewi ni kwa nini Serikali imeamua kutumia nguvu yake kwenda kulirudisha nyuma suala la ndoa za utotoni ambalo limekwishaamuliwa na Mahakama kwamba tuletewe humu tubadilishe sheria, eti sasa hivi wanaenda kukusanya maoni ya wadau. Hii inaonesha ni jinsi gani sisi hatuko *serious*. Walete Sheria hapa tubadilishe na kama wanadhani kuna utaratibu umekiukwa au umekosewa tutajadili humu Bungeni hili ndilo jumba la Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha asilimia 44 ya wanawake walioko Shinyanga wananyanyaswa ndani ya ndoa zao. Manyanyaso mengi na ukatili mwingi wa kijinsia sasa hivi uko kwenye ndoa. Mwanaume anampiga mke wake anasema yule nikimpelekea kitenge na kanga atakausha hawezi Kwenda kulalamika. Manyanyaso mengi yanatokea ndani ya ndoa, Shinyanga hali ni mbaya. Ndoa za utotoni zimekithiri, mimba za utotoni zimekithiri, unyanyasaji wa kijinsia na sio wanawake tu. Ripoti iliyotoka mwaka 2022, walioripoti unyanyasaji wa kijinsia 42,245 walikuwa ni wananwake na 5,774 walikuwa ni wanaume. Kwa hiyo unyanyasaji uko pande zote mbili, elimu inatakiwa itolewe, kuweka dawati la jinsia peke yake haitoshi. Tuweke *awareness* kwenye jamii, tutoe elimu na watu wachukuliwe hatua. Mila na desturi mbovu ndizo zinafanya wanawake na watoto washindwe kuripoti mambo haya ya unyanyasaji wa kijinsia na ukatili wa kijinsia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sana Serikali kama ambavyo kuna baadhi ya maeneo yamewekewa kanda maalum kwa sababu za kiusalama na Shinyanga iwekewe Kanda maalum kwa sababu ya unyanyasaji wa kijinsia. Kwa sababu ikitoka Shinyanga inafuata Tabora, ikitoka Tabora wanafuata wenzetu wa Mkoa wa Mara, unyanyasaji wa kijinsia kwa Kanda ya Ziwa hali ni mbaya sana na

inachagizwa na mila potofu, utamaduni mbovu, kutokuelewa ambapo wananchi wengi bado wako kwenye hii changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Salome Makamba. Nilimwita Mheshimiwa Innocent Seba Bilakwate aweze kuchangia.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia mpaka sasa kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Kyelwa. Kabla sijaanza kuchangia kwenye hotuba ya Waziri Mkuu nataka nisome neno la Mungu katika Zaburi 33:12; "Heri Taifa ambalo Bwana Mungu wao watu waliochaguliwa kuwa urithi wake."

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme neno hili Taifa la Tanzania ni Taifa Maalum. Inawezekana watu wasijue lakini Taifa hili Mungu ameliweka kwa ajili ya kusudi maalum. Ni lazima kama Watanzania tutambue kusudi hili ambalo Mungu ameliweka katika Taifa hili na tulilinde kwa nguvu zote na gharama zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Mataifa machache ambayo Mungu ameyachagua na ameyaweka kwa ajili ya kusudi maalum. Kwa hiyo ndugu zangu haya mambo ya haki za binadamu ya kuliondoa kusudi la Mungu katika Taifa letu niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, niwaombe sana Watanzania tupambane nalo kwa nguvu zote. Haiwezekani tukaileta laana katika Taifa hili ambalo Mungu ameliweka kusudi lake. Niombe sana viongozi wetu wa kitaifa hili jambo walichukulie *serious* na ikiwezekana pawepo na kipindi

maalum cha kutubu ili kuondoa dhambi hii katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongea hayo sasa nichangie hotuba ya Waziri Mkuu. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya. Watanzania wanajua kazi kubwa anayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais na aendelee hivyo hivyo, tunamtia moyo na naamini na Mungu atakuwa pamoja naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwaletea Watanzania fedha nyingi. Kila mahali Mheshimiwa Rais anakokwenda ameleta fedha na kwa kweli hakuna mahali ambapo hajagusa. Kwa hiyo, tunaendelea kumwombea Mheshimiwa Rais aendelee kuwatumikia Watanzania na naamini Watanzania wako pamoja naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la Vitambulisho vya *NIDA*. Ni haki ya Watanzania kupata vitambulisho vya *NIDA* kwa sababu ni muhimu, lakini jambo ambalo ni la kusikitisha, ni zaidi ya miaka 10 tangu waanze kutengeneza vitambulisho vya Taifa. Hata hivyo, katika maeneo mengi bado hatujaweza kuwafikia Watanzania wengi ili waweze kupata vitambulisho vya *NIDA*. Naamini vitambulisho hivi vya *NIDA* ni haki ya kila Mtanzania. Mtanzania ambaye hana kitambulisho hawezi kusajili simu yake, Mtanzania huyu hawezi hata kusajili biashara yoyote. Kwa hiyo, tunadumaza maendeleo ya Taifa. Hivyo, niiombe sana Serikali haya mambo ya kila siku wanakuja hapa na ngonjera za kutuambia sijui inaletwa mitambo gani, tuombe sasa waje na majibu yaliyo sahihi, Watanzania wapate vitambulisho ili tuondoe usumbufu uliopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile utaratibu wa kupata vitambulisho bado haujakaa vizuri. Kwa maeneo haya

ambayo yapo pembezoni kama Mkoa wa Kagera na maeneo mengine, Watanzania wanapata shida sana. Haiwezekani umeenda kumtambua Mtanzania, wewe Afisa uhamiaji uliyetoka Dar es Salaam bila kushirikisha Viongozi wa Vijiji na Vitongoji, wewe unaanza kutambua unasema huyu ni mhamiaji haramu kwa sababu ana pua ndefu, kwa sababu ni mrefu. Niombe sana tushirikishe jamii inayozunguka maeneo hayo ili tuweze kuwatambua wale ambao hawastahili ili Watanzania wanaostahili waweze kupewa Vitambulisho vya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine niongelee suala la umeme. Umeme ni maendeleo, umeme ni ajira, lakini pia umeme ni uchumi. Mheshimiwa Rais anapambana sana kuleta pesa kwa ajili ya kuwapa Watanzania umeme, lakini kasi ya kupeleka umeme ni ndogo. Mfano, upande wa Kyerwa, tuna vijiji 28 ambavyo bado havijapatiwa umeme, lakini vijiji hivi tayari Mkandarasi amekwishapewa. Niombe sana Serikali ifuatilie huyu Mkandarasi anayepeleka umeme Mkoa wa Kagera, kwa kweli *speed* yake ni ndogo. Haiwezekani ndani ya miaka miwili kwenye Wilaya ya Kyelwa ameshindwa hata vijiji vitatu, sasa hivi ni vijiji viwili tu. Kasi yake ni ndogo kwa kweli hairidhishi. Pesa ipo Serikali imetoa, lakini hawa wakandarasi wanaowapa wakati mwingine wawaangalie waone ni wakandarasi wa namna gani. Watanzania wanahitaji umeme kwa sababu ni muhimu sana. Kwa hiyo niombe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu hili aliangalie kama Msimamizi Mkuu wa Shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine niongelee kilimo. Serikali imeweka fedha nyingi kwenye kilimo na tunampongeza Mheshimiwa Waziri Bashe anafanya kazi nzuri. Tulishuhudia hapa wanagawa pikipiki za Maafisa Ugani, lakini niombe sana Mheshimiwa Waziri Bashe hili aliangalie Maafisa Ugani wake wanamwangusha. Hakuna kazi wanayoifanya. Hawa Maafisa Ugani kitu wanachokifanya kwa mfano Kyerwa, wanasubiri msimu wa kahawa, mkulima anaanza

kuvuna kahawa ndipo wanakuja kukagua kama ile kahawa imekomaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzoni wakati anaanza kulima, anapalilia, anahudumia hili zao hatumwoni Afisa Ugani lakini ukifika wakati wa kuvuna wanakuja kwa kasi. Wakati mwingine wanakuja kutafuta fedha kwa wakulima, kuwaibia. Kwa hiyo, niombe sana, ni lazima tuweke nguvu kubwa ili mkulima aweze kupata zao ambalo ni zuri na lenye tija. Kwa hiyo, niombe hili Mheshimiwa Bashe aliangalie Maafisa Ugani wake kwa kweli wanamwangusha hawafanyi kazi, wamekaa tu na hizo pikipiki walizowapa sijui wanazifanyia nini? Kwa hiyo niombe sana hili waliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilisemee ni suala la barabara. Barabara ni muhimu sana. Hizi barabara za Wilaya ya Kyerwa zimezungumziwa muda mrefu. Barabara ya Omurushaka kwenda mpaka Murongo, tenda imetangazwa mwaka 2022, Mkandarasi amekwishapatikana, lakini mpaka leo zaidi ya miezi sita hatujaona Mkandarasi. Tunaomba Mkandarasi aje asaini Mkataba, barabara hii ianze kujengwa kwani ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile barabara ya Mugakorongo kwenda mpaka Murongo, hii ni barabra muhimu, ni barabara inayounganisha Nchi ya Uganda na Tanzania. Ni lazima tufanye biashara na hawa wenzetu. Ukienda kwa wenzetu unaangalia ni kama Ulaya, lakini ukija huku kwetu ni kama uchochoro. Niombe sana kwa sababu barabara hii imeshatangazwa, tenda imeshafunguliwa, Mkandarasi apatikane na barabara hii ianze ili Wanakyerwa na wao waweze kujiona kama ni sehemu ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bilakwate. Nilimwita Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo aweze kuchangia.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia fursa hii kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Niwapongeze Serikali yetu ambayo iko chini ya Rais wetu Mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambazo zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tukiwa kwenye Kamati tulitembelea Mradi wa Ujenzi wa Meli ya Kisasa ya *MV* Mwanza Hapa Kazi tu. Katika maelezo tuliyopewa na Wakandarasi, tuliambiwa ujenzi wa meli unatumia chuma zaidi ya asilimia 60. Chuma chenyewe ambacho kinajenga meli yetu ya kisasa ambayo itaigharimu Serikali yetu zaidi ya shilingi bilioni 108 kinaagizwa kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia gharama ya ujenzi wa meli, bilioni 108, kama tungekuwa na mkakati wa dhati wa kuchimba chuma chetu cha Liganga na Mchuchuma ina maana zaidi ya shilingi bilioni 64 zingebaki hapa nchini, zingechochea uchumi na zingeongeza ajira. Niishauri Serikali yangu suala la kuchimba chuma cha Liganga na Mchuchuma nadhani kwa sasa hatuhitaji mjadala mpana zaidi, ni suala ambalo lazima tulifanye kama tunataka kujenga uchumi wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wa kanda ya Ziwa suala la meli ni suala la siasa ni suala la uchumi. Tunaishukuru Serikali kwa meli hiyo na tunamwombea Rais wetu na Mtendaji wetu Mkuu Waziri Mkuu wetu, wasukume kuhakikisha kwamba hiyo meli imekamilika na twende kuitumia kwa ajili ya uchumi wa kanda ya ziwa na Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma Hotuba ya Waziri Mkuu ameongelea huduma kwa wazee. Kuna wachangiaji wameongelea wazee ambao ni wastaafu lakini tuna wazee ambao walitumikia Taifa hili katika nyadhifa mbalimbali. Vile vile, tuna wazee kama baba yangu ambaye alikuwa mkulima akizalisha kahawa ikiuzwa na kuchangia pato la Taifa. Hao wazee ni wengi na kusema kweli nimesoma hotuba ya Waziri Mkuu amewaongelea, lakini tatizo kubwa la wazee wetu wanahitaji na wao kutambuliwa. Kwa kutambuliwa huko hawahitaji tuwatambue kwa maneno, wanataka na wenyewe watambuliwe kwa kupewa ka-*pension* hata kama ni kadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewasahau sana hawa wazee wetu, wanahangaika, wanateseka, tunataka yanayotendeka Zanzibar, kama Zanzibar wanaweza wakawapa *pension* hawa wazee ambao hawakuwa wafanyakazi wa Serikali, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na wazee wa Tanzania Bara tuwaangalie. Ni wazee ambao wametulea, wametumikia Taifa hili katika nyanja mbalimbali kilimo, uvuvi, ufugaji naomba tuwape heshima yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewasikiliza wachangiaji wengi hapa tangu hotuba ya Waziri Mkuu tuanze kuichangia wachangiaji wengi wameongelea migogoro ya ardhi kati ya Taasisi za Serikali na wanavijiji na wananchi kwa ujumla. Kama tutapata majanga mbele ya safari matatizo haya yatatokana na umiliki wa ardhi tusipochukua hatua leo. Wachangiaji leo asubuhi alianza Mheshimiwa Ezra, jana tulikuwa na Mheshimiwa hapa Ndugu yangu Mheshimiwa Kwezi anaongelea kwao Sikonge kule, kila sehemu kuna matatizo makubwa sana ya ardhi na matatizo mengi unakuta ni kati ya Taasisi ya Umma aidha Hifadhi ya Misitu au *NARCO* ni matatizo ambayo yanasababishwa moja kwa moja na Serikali yenyewe au Taasisi zake, matatizo ya namna

hiyo lazima tuchukue hatua za haraka sana kukabiliana nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana niliongelea suala la Mwisa hapa na Kaka yangu Mheshimiwa Mwijage ameongelea Rutoro, tunaongelea vijiji ambavyo vimesajiliwa kisheria, Taasisi ya Serikali inakuja kwenye hivyo vijiji kwa mantiki hiyo *NARCO* wanapima vitalu kwenye ardhi ya vijiji ambavyo vimesajiliwa kisheria na wanagawa hivyo vitalu wanamwachia mtu ambae amepewa kitalu kazi ya kuhamisha wananchi, hii haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatengeneza ukaburu mwingine, mwenye pesa mpishe na ukishakuwa kwenye vile vijiji mtu anakuja anakuhamisha hakuna chochote anachoondoka nacho. Hili tatizo lazima tutafute suluhu vinginevyo tutasabaisha matatizo makubwa kwa wananchi wetu na zaidi wananchi maskini, hawa ndiyo kazi kubwa ya Serikali ni kuwatetea na kuhakikisha kwamba wanaishi na wanapewa heshima kama wananchi wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwisa ambayo ipo Muleba, wakati naingia kwenye Ubunge niliambiwa ni hekta 133,000 ni eneo kubwa sana ambalo kwa Wilaya ya Muleba na Mkoa wa Kagera lile eneo ndilo linazalisha chakula cha kulisha Wilaya ya Muleba. Watu wakaja pale kwenye ardhi ya vijiji vya wananchi wakapima vitalu, sasa wanataka waondoe wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sasa ukiondoa wananchi hilo eneo kutokana na ukubwa wake, linapakana na Hifadhi ya Taifa ya Burigi-Chato na upande wa Magharibi kuna Ziwa Burigi lazima tuangalie na masuala ya ekolojia ya lile eneo, ukishawaondoa misitu itakatwa tutatengeneza jangwa lakini kikubwa zaidi lile eneo ndilo linalisha Wilaya ya Muleba na Mikoa Jirani, tutatengeneza baa la njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu na kuishauri lile eneo badala ya kupima vitalu twendeni tukalipime upya, tukatenge maeneo ya kilimo, tukatenge maeneo ya ufugaji tukatenge maeneo ya makazi ya wananchi, eneo ni kubwa hatuna haja ya kugombana gombana na watu hapa ni suala la kufanya matumizi bora ya ardhi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho lile eneo ni eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, siyo suala la sijui la mifugo Hapana! hatujawahi kufanya taratibu za kisheria za kuhaulisha lile eneo kutoka kwenye miliki ya Hamlashauri ya Wilaya ya Muleba kulileta kwenye Wizara nyingine yoyote Hapana! Hapa tunavyoongea naishukuru Serikali yangu wameshatupa mpaka na Hati za Vijiji vimesajiriwa na havijawahi kufutwa huyu *NARCO* anatoka wapi? Mamlaka kapewa na nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa tumekuwa tukicheza na namba, leo hekta 130, kesho hekta 76 leo naambiwa ni hekta 43 hizi nyingine zimeenda wapi? Ndiyo maana naishauri Serikali tukapime lile eneo upya tujue lina ukubwa kiasi gani tukapange matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho. Sasa hivi tupo kwenye mfumo wa mavuno ya kahawa Kagera, nashukuru Waziri mkuu amefanya kazi nzuri na natumaini ataendelea kutufanyia kazi nzuri na nimeongea naye juzi hapa, tunaomba sasa msimu unapoanza wakulima wapewe ili vyama vya msingi vianze kununua kahawa yetu mapema, Mheshimiwa Bashe naona ameniangalia pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kukimbiana wakulima eti kahawa ni magendo, katika nchi ya Tanzania kati ya Kata na Kata naomba mwaka huu nitafurahi nisipo lisikia. Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Bashe uliniambia, ulisema kahawa ni mali mkulima siyo mali ya Serikali, inakuwa mali ya Serikali pale

ambapo imenunuliwa kutoka kwa mkulima imeingizwa kwenye maghala itakuwa mali ya Serikali. Sikubaliani na magendo ya kutorosha kahawa kuipeleka nje ya nchi kwa sababu tutakuwa tunakosa kodi, lakini biashara ndogondogo za humo kwa humo kati ya Kijiji na Kijiji, Kata na Kata tuwaruhusu wakulima wakauze kahawa yao.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana tunaendelea na kazi ya kusafirisha abiria wetu Mkoa wa Kagera. Niliongea mwaka jana na nalirudia na litakuwa la mwisho na nitaendelea kulisema kwamba Uwanja wa Ndege wa Mkajunguti ni suala ambalo haliepukiki kwa sasa kutokana na wingi wa abiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi niliongelea suala la kiwanda cha Kahawa cha *TANICA,* kiwanda hiki kina miliki kati ya Serikali na Vyama vya Msingi, lakini kile kiwanda hakiwezi kuzalisha kwa uwezo wake na Kagera tunazalisha kahawa, kile kiwanda ndiyo kiwanda pekee ambacho kinaweza kutusaidia ku-*process* kahawa inayozalishwa Kagera ninakuomba Serikali itupatie mtaji wa kutosha ili kiwanda hiki kiweze kuzalisha *at full capacity,* sasa hivi kinazalisha *under five percent* sasa kiwanda gani hiki?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kahawa ipo tunakimbizana na wauza kahawa, sasa hivi wanapeleka Uganda sijui wapi? Ni kwa sababu tumeshindwa kuingiza mtaji katika kile kiwanda. Serikali inaweza ikanunua zile hisa ambazo haijanunua mpaka leo ni Bilioni 8.6 ni hela ndogo! Mheshimiwa Bashe una hela nyingi na hicho kiwanda kipo chini ya Wizara yako, hebu tupeni hiyo hela tukaiongeze mtaji, tunanunulie teknolojia mpya tuweze kuzalisha, itakusaidia wewe na itatusaidia vijana wetu ambao mnawapa mtaji ili waweze kuzalisha lakini itaajiri vijana wetu na kuongeza pesa ya kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga hoja mkono na niwatakie mfungo mwema. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Kikoyo kwa mchango wako. Nilimuita Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris wakati huo Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga pamoja na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga wajiandae.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu. Nitumie nafasi hii pia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kuweza kusimama nikiwa na afya tele kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu katika uwakilishi wangu kwa wananchi wangu waliopo katika Jimbo la Morogoro Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kukupongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yako nzuri ambayo umeitoa hapa Bungeni ikionesha yale ambayo yalifanyika katika kipindi kilichopita lakini mwelekeo wa Wizara yako katika kuyafanyia yale yanayotakiwa kufanywa na Serikali katika mwaka huu wa fedha unaokuja. Nitumie nafasi hii vilevile kumpongeza Mama yetu Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika kuwaletea maendeleo Watanzania. Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano ni mashahidi, mambo ambayo yanafanyika katika Majimbo yetu ni historia ambayo kwa kweli kila Mbunge anashangaa maana ndani ya miaka miwili kuna mambo makubwa ambayo yamefanyika. Tuna kila sababu ya kumpongeza, kumpa moyo lakini kuwa sambamba na yeye katika kufanya yale ambayo anayahitaji yafanyike kwa maendeleo ya Taifa hili la Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuchangia kwenye suala la barabara. Ninaipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi chini ya Rais Samia Suluhu Hassan

kwa kazi kubwa ambayo ameifanya katika ujenzi wa barabara ya Bigwa - Kisaki. Barabara ya Bigwa - Kisaki ni barabara muhimu ambayo inakwenda kwenye Hifadhi ya Mwalimu Nyerere pia inakwenda kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere. Toka tumepata uhuru ilikuwa ni historia lakini kwa mwaka huuu wa fedha Serikali yetu imetenga fedha kujenga kwa kiwango cha lami kilometa 78, *tender* hiyo ilitangazwa tarehe 20 Januari na juzi tarehe 5 Aprili tenda imefunguliwa wako Wakandarasi ambao wanachujwa ili kazi ianze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kila sababu ya kuipongeza Serikali lakini kubwa zaidi niiombe Serikali hasa Wizara ya Ujenzi na *TANROADS* waharakaishe mchakato wa kupata Mkandarasi ili kazi ianze mara moja na Watanzania ambao wako kule Morogoro Kusini, Morogoro Kusini Mashariki na Wilaya ya Morogoro na wao waone matunda ya uhuru kwa kuweza kupita kwenye barabara ya lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile niishauri Serikali yangu na kuiomba Serikali tufanye upembuzi yakinifu wa barabara ya Ngerengere kwenda Mvua na Mvua kwenda Kisaki ili nayo ijengwe kwa kiwango cha lami, kwa sababu barabara zote hizi ni muhimu, ni barabara ambazo zinakwenda kwenye Hifadhi ya Mwalimu Nyerere na Bwawa la Mwalimu Nyerere, tukiweza kukamilisha kufika huko kwa kiwango cha lami tuna uhakika watalii watakwenda, tutaongeza pesa nyingi za kigeni kwenye Serikali ambazo zitasaidia kuleta maendeleo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la barabara niipongeze Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi kikubwa ambayo wameifanya katika kuleta fedha za maendeleo katika upasuaji wa barabara kwenye eneo la *TARURA*. Katika mwaka wa fedha uliokwisha tumepata takribani bilioni 4.13 katika utengenezaji wa barabara kazi inaendelea. Ombi langu kwa Serikali kiuhalisia jiografia ya Jimbo la Morogoro Kusini ni Jimbo ambalo liko milimani fedha hii ambayo

imekwenda imetosheleza kwa kiasi lakini bado kuna uhitaji mkubwa, ninaiomba Serikali yangu ikiwezekana katika bajeti inayokuja hii kupitia TAMISEMI*, TARURA* waongezewe bajeti, ikiwezekana ifike hata bilioni saba tuweze kwenda kupasua barabara za milimani kama vile Singisa, Kasanga, Kolero, Bwakila Juu, Kibogwa ili barabara zifikike maendeleo yapatikane kwa urahisi. Vilevile ninaomba Serikali kuna bajeti tumeomba ombi maalum la billioni moja kwa ajili ya barabara ya Bwakila Juu - Dakawa niombe Serikali itusaidie fedha hizo ili walau tuweze kufanikisha katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwenye suala la elimu tumefanya kazi kubwa sana. Kwa mara ya kwanza nadhani Wabunge mtakuwa ni mashahidi miaka yote kila tunapofika mwishoni mwa mwaka huwa tunakuwa na *operation* maalum kwa ajili ya kuwachangisha wazazi ili watoto waende shule *form one* inapofunguliwa, ndani ya miaka miwili hii chini ya Mama Samia Suluhu Hassan hakuna mzazi ambae amebughudhiwa. Madarasa yalipelekwa na watoto wote walianza kwa mara ya kwanza wote hakukuwa na walioingia awamu ya kwanza, hakukutokea na walioingia awamu ya pili wote waliingia kwa awamu moja, tuna kila sababu ya kumpongeza Mama katika haya na tupo nyuma yake tunamuunga mkono katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali ni kwamba pamoja na mafanikio haya bado kuna changamoto, bado maboma mengi ya nguvu za wananchi ambayo yamejengwa yanahitaji kumaliziwa. Vilevile bado kuna uhitaji wa vyumba vya madarasa, ninaiomba Serikali yangu ihakikishe kwamba mambo haya yanafanyika ili watoto wetu waweze kusoma kwa nafasi na kuweza kupata elimu iliyo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika maeneo ya pembezoni kama vile kwangu Jimboni Kata ya Kolero, Kata

ya Kasanga, Kata ya Kibogwa, Kata ya Singisa na Bwakila Juu, kuna uhitaji mkubwa wa mabweni kutoka katikati ya Kata kwenye shule ya sekondari mpaka kwenda kwenye vijiji kuna mwenda ambao unatumika pengine zaidi ya masaa matatu, manne watoto wetu wanashindwa kwenda na kurudi, matokeo yake nini? Wanakwenda kujipangisha kwenye vijumba ambavyo hakuna ulinzi wa watoto. Kama hivi tunavyopiga kelele maadili na nini, kwa hiyo ninaiomba Serikali ihakikishe kwamba inatutengea mabweni walau mawili mawili kwenye kila shule za sekondari katika bajeti ili watoto wetu wapate utulivu wa kusoma na kukaa katika usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala afya Serikali imefanya kazi kubwa. Ninaipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, kwenye Wilaya yangu hospitali ya Wilaya tumekamilisha, tuna kila sababu ya kupongeza katika hili. Pia Vituo vya Afya Sita vimekamiliaka, maboma Kumi yamemalizwa ya zahanati ambayo ilikuwa nguvu za wananchi zilikuwa zimetumika kulikuwa kuna uhitaji wa Serikali kuongeza, tuna kila sababu ya kupongeza Serikali katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna changamoto ambayo ninaiomba Serikali yangu ya vifaatiba vya upasuaji,majengo ya *OPD* kwa Kituo cha Afya cha Kisemu, Kisaki, na Mikese, vilevile Watumishi bado ni wachache, kuna hela ambazo tuliahidiwa Halmashauri ya Morogoro Vijijini milioni 500 kwa ajili ya vifaatiba kwenye Hospitali ya Wilaya, milioni 300 kwa ajili ya vifaatiba kwenye vituo hivyo nilivyovitaja vya afya na shilingi milioni 150 kwa ajili ya zahanati. Ninaiomba Serikali tuleteeni fedha hizo tukamilishe haya yanayotakiwa kupata ili Watanzania dhamira ya Serikali ya kuwapatia afya inayostahili ikamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kwenye suala la utawala…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimuita Mheshimiwa Hassan Mtenga.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninakushukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Rais wetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya hasa ukilinganisha kwenye Jimbo langu la Mtwara Mjini iko miradi ya mfano ya mabilioni ya shilingi ambayo yanaendelea sasa hivi kufanyika, ni vema nikamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimshukuru Makamu wa Rais Mheshimiwa Isdory Mpango, nimshukuru Waziri Mkuu na hapa nigande kidogo niseme kwamba, Waziri Mkuu nakushukuru sana kwa mambo mengi ambayo umekuwa unanishauri, unanisaidia kwenye Jimbo langu kwa kweli nakutakia kila la kheri Mwenyezi Mungu akubaliki sana. Pia kwenye shughuli ya Mwenge Mheshimiwa Waziri Mkuu umetutendea haki Wananchi wa Mtwara, kwa hiyo tunakupa pongezi la Wanamtwara wamenipa salamu tukuambie kwamba wanakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo zaidi ya matatu ya kuzungumza. Jambo la kwanza tunazungumza uchumi ndani ya nchi yetu, tunapozungumza uchumi ndani ya nchi yetu hatuwezi kuwa na uchumi ambao ni bora kama hatutakuwa na viwanda ndani ya nchi. Nimeona nilizungumze hili tukiangalia *zone* ya Mtwara na Lindi ni watu ambao tunazalisha au tuna maeneo mengi ya madini lakini madini haya yana uwezo wa kutengeneza *gypsum* yana

uwezo wa kutengeneza zana za aina nyingi za ujenzi. Ninaishauri Serikali muda sasa umefika kwa sababu *material* haya tusifike mahala tukawa tunayatumia vibaya, *material* haya kama tungefika sehemu tukawaleta wawekezaji wakaweka viwanda, nadhani tungepiga hatua kiuchumi na hata vijana wetu wangepata ajira za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo ambalo mara nyingi sana nimekuwa nazungumza kwenye Bunge hili lako Tukufu, inawezekana ninaeleweka au nisieleweke hata hivyo Wabunge wanzangu naomba kwa hili mni-*support*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtwara tulikuwa na mpango wa *Mtwara Corridor* na hii *Mtwara corridor package* yake tunazungumza bandari, tunazungumza *airport*, tunazungumza na reli ya Liganga na Mchuchuma, Mbamba *Bay*. Nimesikiliza taarifa hapa na ripoti ya Waziri Mkuu sijasikia masuala ya Reli ya Mtwara *Mbamba Bay*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tumefika eneo Serikali tumewekeza bilioni 157 kwenye Bandari ya Mtwara na ninadhani uwekezaji ule umewekezwa kwa ajili ya kufungua njia na fursa za kiuchumi, ni vyema sasa nikaishauri Serikali kwamba mpango wa kutujengea reli bado ubaki palepale na jitihada ziongezeke ili reli tupate ya Mtwara Mbamba *Bay*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la ujenzi wa daraja, kwanza ninaishukuru Serikali mlitujengea daraja kule Mtambaswala, tunachozungumza kuhusu daraja na Mto Ruvuma tunazungumza *mileage* na hasa kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtwara Mjini kuna kiwanda cha Dangote kiwanda hiki kinapeleka *cement* mpaka Katavi, lakini kiwanda hiki hakina uwezo wa kupeleka *cement* Pemba, Mozambique na maeneo mengine kwa sababu ya

*milage*. Hoja yetu Wanamtwara tunasema mtufungulie daraja pale Kilambo, kutoka Mtwara Mjini mpaka unaingia Kilambo ni kilometa 70, ukitoka Kilambo mpaka unaingia Mocimboa da Praia Wilaya ya kwanza ya Mozambique pana kilometa 56. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mmoja tu, leo Waziri wa Uchukuzi alitembelea kwenye Bandari ya Mtwara akakuta kuna bomba nyingi ambazo zinakwenda Mozambique ambazo zile bomba ni za watu ambao wanakwenda kushughulika na masuala ya gesi Mozambique, lakini bandari yao ambayo wanaona ni karibu kuitumia ni Bandari ya Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bomba zile ni mwaka wa pili sasa zipo bandarini hazina uwezo wa kwenda *Mozambique*, kwa sababu njia ambayo ipo ambayo tungeweza kuitumia, *mileage* zinawakataa na gharama ni kubwa sana. Sasa naomba, leo tunaizungumzia Dangote kama Dangote, mfanyabiashara mmoja mkubwa sana. *Cement* mfuko mmoja *TRA* wanachukua zaidi ya shilingi 3,000, lakini *cement* ya *Mozambique* mfuko mmoja kwa hela ya kwetu ni shilingi 35,000 kwa hela ya Tanzania. Dangote anasema kama daraja hili litapitika, nitauza *cement* kwa shilingi 16,000. Tunakwenda sasa kufanya biashara kubwa na *TRA* ya Mtwara kiujumla itakuwa imepata mapato ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme suala hili halihitaji kuwepo na profesa, halihitaji mtu awe na *degree* kwenye ufahamu wa suala hili. Tumsaidie Rais. Rais wetu sasa halali usiku na mchana anahaingaika kuona ni jinsi gani Tanzania ataifikisha pale wanapohitaji Watanzania. Tunakaa humu tunahangaika na ushuru wa *PP*, ushuru sijui wa mbaazi, wakati *item* tunazo wenyewe za kuzitengeneza tukapata fedha kwenye Serikali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuliotembea tumekwenda India juzi juzi, tumeona kule sekta binafsi wanatengeneza madaraja, nchi inafunguka, wanatengeneza reli, nchi zinafunguka, hapa tunaogopa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitu vingine kwa kweli hata kuvisema vinaleta simanzi ndani ya Bunge letu hili. Mtwara ni sehemu ya Tanzania, lakini mfano mmoja, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwezi mmoja na nusu uliopita alikuwa anakwenda Lindi, wananchi wa Mtwara wamemsubiri kuanzia saa 2:00 alivyopita pale mpaka saa 10:00 wako juani, wanamsubiri Rais wao kwa mapenzi makubwa. Sasa hili siyo kwamba ni suala la Mbunge, maana leo kuna hoja zinaongelewa, suala hili ni la Mbunge. Suala hili siyo la Mbunge, ni la kitaifa. Tunapozungumzia kufungua mipaka, tunazungumzia fursa za nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili mimi nilitaka nilizungumze kwa mapana na marefu sana. Tunaomba wenye mamlaka mtusaidie. Mimi nimekwenda mbali zaidi, tumewasiliana na wenzetu wa *Mozambique,* sisi ndio majirani, wanasema sisi tuko tayari, ni suala la Waziri wa Fedha, Waziri wa Uchukuzi, sawa bwana, tuangalie ni mpango gani tunaweza tukaenda tukamaliza hii fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya mambo ni ya msingi sana, lakini kuna suala moja la mwisho nalotaka niliseme…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mtenga, na muda wako umeisha. *(Makofi)*

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimwita Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, wakati huo Mheshimiwa Zuena Bushiri, Mheshimiwa Elibariki Kingu, na Mheshimiwa Dorothy Kilave wanajiandaa.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri sana ambayo ameiwasilisha ndani ya Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala zima la tathmini zinazofanywa na baadhi ya watendaji kwa vitisho kwa wananchi wetu. Hivi karibuni, mwaka jana 2022 kwenye suala hili la ujenzi wa Reli ya *SGR*, *route* tatu katika Mkoa wetu wa Tabora. Jana niliuliza hapa swali la nyongeza kuhusiana na malipo yao, lakini wakati naliuliza nilisema, pamoja na fedha kidogo ambayo wameambiwa watalipwa lakini bado fedha hii imecheleweshwa kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona leo nilizungumze jambo hili ili liweze kuwekwa sawa. Watendaji hawa walipofika kufanya tathmini ya maeneo ya wananchi wetu hususan katika Manispaa ya Tabora, Eneo la Ndevelwa, watu hawa wamepimiwa maeneo yao, *square* mita zilizopatikana eti kila *square* mita moja Shilingi 800. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia ya sasa, nchi yetu hii sasa kuna ardhi unaweza kununua *square* mita kwa Shilingi 800? Hawa watu wana hati, wamesajiliwa, wanajulikana, ni maeneo ambayo ni mapya, hawakukataa kupisha mradi huu kwa sababu ya uzalendo wao. Walisema mradi huu upitishwe, tunahitaji maendeleo ya Wana-Tabora lakini walipwe stahiki zao sahihi. Kwa akili ya kawaida haiwezekani, mtu mwenye *square* mita 500 anakwenda kulipa shilingi 400,000 wakati leo ukiigusa ardhi Tabora Mjini, huna milioni mbili hupati eneo la kujenga nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu unaenda kumlipa shilingi 400,000 aipeleke wapi? Kwa nini tunataka kuifanya Serikali ionekane haijali wananchi wake, na hasa kwa kipindi hiki ambacho Mama Samia anaongoza ambaye ni mwanamke mwenzetu? Hatutaki jambo hilo litokee, lakini naomba niliseme, tena nalisema kwa machungu makubwa na kwa ukali. Haiwezekani, na kwenye nchi hii na kwenye Taifa hili kuwalipa watu shilingi 800 kwa *square* mita moja, haiwezekani Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Ofisi ya Waziri Mkuu, jambo hili Mheshimiwa Waziri Jenista na watu wako, tunaomba mwasaidie wananchi wetu ni masikini. Haiwezekani, nendeni mkaone mjue. Tunaumia sisi viongozi wao. Unamlipa mtu shilingi 800! Cha kusikitisha, ninao mfano mmoja hapa, kuna mtu mmoja kalipwa shilingi 350 kwa *square* mita moja. Huyu mwananchi ana *square* mita 4,643. Huo ni ukubwa wa eneo lake. Malipo alioyoandikiwa kulipwa, bado hawajalipwa maana yake, hapa nazungumza ni zaidi ya mwaka sasa umepita bado malipo hayo hawajalipwa, atalipwa shilingi 1,639,050. Hayo ni malipo ya fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye kila *square* mita moja ukipiga hesabu na humu ndani kuna wanamahesabu, kila *square* mita moja ni Shilingi 350/=. Jamani, sisi watu wa Tabora ni wapole sana, ni wastaarabu, ni wakarimu, lakini msichukulie *advantage* upole wetu na ustaarabu wetu kutufanyia haya. Yanaumiza! Hivi leo maeneo haya yangekuwa ni yetu sisi viongozi, tungekubali kweli kulipwa kiasi hiki! Mtu ana hati tayari, mtu ana kila kitu tayari ameshaweka pale, anasubiri mji upangwe ili aweze kufanya maendeleo yake kwenye eneo lake! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi umepita mkubwa tumekubali, lakini leo inakuwa ni dhahama sasa! Badala ya raha ya kusema kwamba nataka mradi upite, wananchi wananung'unika, wanasikitika, tutapata wapi baraka? Hii ni

dhuluma, siyo haki. Ni lazima Serikali iangalie jambo hili jamani. Hata kama haliwezekani, liangalieni jambo hili mwasaidie hawa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Mwakibete amelifuatilia jambo hili angalau hiyo *amount* ndogo ambayo wameandikiwa, Mheshimiwa Mwakibete ameisimamia angalau walipwe kwanza, kama kuna mambo mengine yatafuata. Waheshimiwa Waziri ninyi ni viongozi wenzetu, ni wazazi, mna ndugu, mna jamaa, na marafiki, kwa fedha hii tunaomba watusaidie tafadhali watu hawa waweze kulipwa stahiki zao kwa mujibu wa eneo na maeneo yao. Shilingi 800/= haiwezi kutosha. Yaani kwa kweli naongea kwa uchungu mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusiana na hili suala zima la shule kongwe. Hili suala la shule kongwe limekuwa linazungumzwa tu juu juu. Sisi wananchi wa Tabora tunazo shule maarufu kongwe Tabora Mjini pale. Kuna Shule ya *Tabora Boys*, kuna Shule ya *Tabora Girls*. Shule hizi zimetoa watu maarufu na wengine wamo humu ndani. Wengine ni viongozi wakubwa kwenye Taifa hili, lakini kizuri zaidi, Shule ya *Tabora Boys* Baba wa Taifa, amesoma pale. Ukiona shule zile na hali iliyopo ni aibu hata kusema shule hii amesoma Baba wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Serikali inatuambia tutoe fedha za mapato ya ndani kwenda kufanya ukarabati wa shule hizi, jamani mnatuonea! Hebu saidieni shule hizi za kihistoria ziweze kuwa shule bora. Unapofika pale Tabora, unasema naenda *Tabora Boys*, hilo geti lenyewe linavyokuitikia, aibu! Halina hata mvuto! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo kwenye Kamati ya *LAAC,* tumepita juzi pale. Tunashukuru wafadhili wametusaidia kutengeneza mabweni, wameyakarabati. Tumeingia mpaka

chumba cha Baba wa Taifa alicholala, tumekiona, lakini nenda kwenye bwalo, nenda kwenye majengo mengine, ni aibu! Shule ya *Tabora Girls* kuna watoto wetu wa kike, hata *fence* tu haina. Wanaume wakware wanapita pale na magari yao kujionesha, kufanyaje, wanawakonyeza watoto wetu, wanawaharabia masomo yao. Wajengewe angalau *fence* pale kwanza ili watoto wetu waweze kusoma kwa amani na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa dakika chache ulizonipatia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Zuena Bushiri.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nami kunipatia nafasi nichangie hotuba hii ya Bajeti ya Waziri Mkuu. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya katika Taifa hili na kutuletea fedha nyingi sana kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee Mkoa waa Kilimanjaro. Mkoa wa Kilimanjaro tumepata Shilingi bilioni 620.224 katika miradi 717. Tunampongeza sana Mama, tunaipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Naomba nifafanue miradi hii. Afya tumepata shilingi bilioni 45, elimu tumepata shilingi bilioni 17.21, ujenzi tumepata shilingi bilioni 126, nishati tumepata shilingi bilioni 21.59, maji tumepata shilingi bilioni 358.43, uchumi tumepata shilingi bilioni 17.63, ardhi tumepata shilingi bilioni 11.3, utawala tumepata shilingi bilioni 3.97. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa fedha hizi ambazo tumezipata kwa kuwa haijawahi

kutokea, ni jambo la kihistoria. Baada ya pongezi hizi na fedha hizi ambazo tumezipata, nitajikita katika sekta ya afya.

MHeshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya kazi kubwa sana katika sekta ya afya, tumejenga zahanati, tumejenga vituo vya afya, tumejenga hospitali za wilaya, za mikoa na za rufaa. Hata hivyo, bado tuna changamoto ambazo hospitali hizi zinaikabili. Kwanza kabisa tuna changamoto ya watumishi, hasa katika ngazi za kata katika zahanati. Ni ukweli usiopingika kwamba tunao watumishi wachache sana hasa katika sehemu za vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna changamoto ya nyumba za watumishi. Unakuta daktari amehamishiwa zahanati fulani, lakini anatumia kilometa kama moja na nusu kutembea kila siku kufika katika kituo chake cha kazi. Naiomba Serikali iliangalie hili kwa kina kirefu, kwa mapana yake ili madaktari hawa waweze kufanya kazi vizuri na kuwahudumia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika Hospitali ya Rufaa ya Mawenzi. Nilisimama tena hapa kuongelea kuhusu Hospitali hii ya Mawenzi ambayo ni Hospitali ya Mkoa. Nashukuru Serikali kwa kuwa imefanya kazi kubwa sana katika jengo la mama na mtoto, linaendelea vizuri na kazi inaendelea. Pia, naishukuru Serikali kwa Shilingi bilioni 1.5 ambayo wametupatia kwa ajili ya ujenzi wa wodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba Hospitali hii ya Mawenzi ni hospitali ambayo imejengwa kipindi cha mkoloni, majengo yake yamechoka sana na hayana hadhi ya kuitwa Hospitali ya Mkoa. Naiomba Serikali ijitahidi kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya wodi zilizoko pale ili angalau ziweze kujengwa zifanane na hadhi ya Hospitali ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine niongelee changamoto iliyopo katika Hospitali ya Mawenzi ambayo ni jengo la kuhifadhia maiti *(Mortuary)*. Kama nilivyotangulia kusema kwamba majengo mengi yalijengwa kipindi cha mkoloni. Jengo hili kwanza ni dogo, lakini pia ni la zamani, hata majokofu yaliopo pale yamechoka. Hospitali ile ya Mawenzi ni ya Mkoa. Tunazo wilaya saba katika Mkoa wa Kilimanjaro, wote wanaitegemea ile hospitali, lakini yanapotokea matatizo ya watu kufariki, nasikitika sana kwa sababu hata hospitali ile inazidiwa kiasi kwamba miili ile ya marehemu itafutiwe nafasi kupelekwa kwenye Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya *KCMC*, jambo ambalo unakuta sasa nyingine hata kule *KCMC* kumejaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, naamini ni Serikali Sikivu, iangalie Mkoa wa Kilimajaro na ile Hospitali ya Mawenzi ili iweze kutusaidia sehemu hii ya *mortuary*. Kwanza tujengewe *mortuary* kubwa ambayo itakuwa na hadhi ya mkoa na itakayokuwa na majokofu mengi na imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia baada ya kuchangia kuhusu Hospitali ya Mawenzi kwa maana ya afya, naomba nije katika ukatili dhidi ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mwanamke na ninaposema suala la mtoto, niseme wote ni wazazi, Wabunge wenzangu wanaume msije mkasema lakini wanaume sisi; wanawake inatugusa zaidi. Inatugusa kwa ile amini tuliyokula ya kukaa na watoto tumboni miezi tisa na kuwalea mpaka watakapofika hatua ambayo wanajitambua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ukatili wa watoto kwa kweli limekithiri sana hapa nchini. Mimi kama Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Kilimanjaro, nilifanya ziara katika Mkoa mzima wa Kilimanjaro nikiambatana na watumishi wa Dawati la Kijinsia katika Wilaya zote. Nasikitika mambo ambayo

tulikuwa hatutegemei kwamba yanaweza kufanyika yanafanyika katika Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba kama Wabunge wote hatutakuwa na sauti moja, tukashikana, suala hili hatutaweza kulimaliza. Ninasema hivyo kwa sababu gani? Kumekuwa na utamaduni katika baadhi ya maeneo; niiseme Kilimanjaro. Baadhi ya watumishi wamekutana na changamoto ambayo mimi binafsi imeniwia ngumu. Nasema hivyo kwa sababu wanasema, baada ya kukutana na hoja kama hizo watoto wamefanyiwa ukatili, wanapokwenda kufuatilia, unakuta kwamba wale wazazi wanakutana wenyewe, wanayaongea wenyewe na zile kesi kule mahakamani hatimaye zinafutwa. Naiomba Serikali, kesi kama hizi zikipelekwa pale zifanyiwe uharaka ili ziishe haraka ili watu wasipotoshe Ushahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani kidogo, mimi ni Mpare nimeolewa na Mchaga, ni waume zangu, lakini wana utamaduni ambao mimi binafsi siupendi. Kule Uchagani unapofanya jambo ambalo linakuuma sana au ni zito, kuna jani moja linaitwa *sale*. Ukiiongea na watumishi wale, dawati la jinsia watakwambia tatizo hilo. Wanapokuta mambo yamekuwa siyo mazuri, linatumika jani la *sale* kwenda kuomba msamaha ili mambo yaishe. Wakati huo tayari watoto wameshaathirika. Nawaomba ndugu zangu tusitumie vitu vya mila kuharibu vizazi vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisemea hili kwa sababu haiingii akilini uletewe sare wakati mtoto wako amelawitiwa, ni jambo la kusikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee pia…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Elibariki Kingu wakati huo Mheshimiwa Dorothy Kilave anajiandaa.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nakwenda kuzungumza mambo mawili tu na mambo haya mawili nayokwenda kuzungumza yapo katika *level* ya kitaifa kwa lengo la kuisaidia Serikali na kuwasaidia walipakodi ambao ni Wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 7 Desemba, 2020, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kiongozi wetu Kassim Majaliwa Majaliwa kwa uzalendo kwa kutanguliza maslahi mapana ya Taifa alitoa maelekezo kwa kuangalia namna gani Watanzania walipita katika msuko msuko mkubwa ambao ulipelekea kupanda kwa bei kubwa ya bidhaa katika Taifa letu ikiwemo bidhaa ya *cement* na bidhaa zingine. Tarehe 7 Desemba Waziri Mkuu alitoa maagizo ya kufanyika kwa *study* ambayo ingeweza kuleta majibu katika Taifa letu kwa nini Watanzania wamepata *burden* kubwa katika sekta ya ujenzi kwa sababu ya kupanda kwa bei ya *cement* katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikupe taarifa; *Fair Competition Act* Na. 8 ya mwaka 2003 *section 5(1)* imeeleza namna gani kampuni inaweza kuwa na *market share* katika Taifa letu katika uwekezaji wa aina yoyote katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikupe taarifa hata ninapozungumza hapa, aliyekuwa Waziri wa wakati huo *Professor* Kitila Mkumbo; ninakupongeza kwa sababu wewe pia ulitanguliza mbele maslahi ya nchi na nina imani hata

mwalimu wangu aliyenifundisha *Mzumbe University* Mwalimu Dkt. Ashatu akipewa na yeye maelezo mazuri atakwenda kuyatanguliza maslahi mbele ya nchi, wataweza kuzishauri mamlaka za nchi kuhakikisha ya kwamba maslahi ya Watanzania, maslahi ya walipakodi yanalindwa dhidi ya ma-*cartel* ya kijambazi yanayochukua nafasi katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikwambie, *study* iliyofanywa na vijana wazalendo wa Kitanzania waliosomeshwa na kodi za walalahoi wa Kitanzania. *Study* imeonyesha miunganiko ambayo *Twiga Cement* waliokuwa wanataka kumnunua *Tanga Cement* jambo la kwanza. *Study* zinaonyesha ilikuwa inakwenda ku-*violate Fair Competition Act* Na. 8 ya mwaka 2003 *section 5(1)* iliyopitishwa na Bunge hili tukufu kwa ajili ya kumlinda mwananchi mlalahoi kule mtaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunapozungumza *study* imeonyesha gharama ya kutengeneza na kuzalisha mfuko mmoja wa *cement* kwenye taifa hili la Tanzania *it is only 5,700 Tshs.* Gharama ya kuzalisha mfuko mmoja wa *cement* ni shilingi 5,700. Kampuni ikiachwa ikauza kwa faida, bei ya *cement* kwenye Taifa letu hakuna namna bei ya *cement* inaweza ikazidi shilingi 8,700 na shilingi 9,000 lakini nini kinafanyika? Makampuni haya ya uzalishaji wa *cement study* zinaonyesha yanafanya kitu kinaitwa *cartels* zilizozungumzwa katika *Fair Competition Act* ambayo imepitishwa na Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nikupe taarifa, *cartel* hizi tunazozizungumza nataka niwaambieni na ndiyo maana Wabunge nataka niwashawishi. Mna kazi kubwa sana kumwombea Mheshimiwa Rais na Waziri Mkuu huyu na Mawaziri ili wawe na moyo wa kizalendo wa kufanya maamuzi ya kizalendo. Mambo haya wanapambana na watu matajiri wakubwa, watu wenye fedha, vita hii bila

kumtanguliza Mungu taifa hili Watanzania watakuwa wanageuka kushoto wanapigwa, wanageuka kulia wanapigwa mamiradi ya Serikali Mheshimiwa Rais juzi amelalamika anasema *Engineer estimates* zinakuwa kubwa. Miongoni mwa vyanzo vinavyosababisha nchi yetu inapata hasara ni kwenye *study* kama hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninapozungumza, Umoja wa Wazalisha *Cement* wa Afrika Mashariki kwa *study* wamegundulika wanakaa vikao, wanafanya *market allocation,* wanapanga bei za *cement* na ninataka nikwambie hata Bunge hili kuna wakati tunakuja tunapitisha vitu hapa maskini ya Mungu bila kuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninapozungumza, *research* inaonyesha ukuaji wa Sekta ya Ujenzi umekua kwa 13% lakini nenda kwenye viwanda, uzalishaji wa *cement* umeongezeka *only* kwa 3% na hiyo *percent* ninayoizungumza ya 3% kwa 13% ambayo sekta inakua; viwanda vimezalisha 3% lakini *capacity* yake vinatakiwa vizalishe 50% na tulichokifanya kibaya zaidi tumekwenda tukapandisha bei ya *importation* ya *cement* kutoka 25% mpaka 35%. Tunamlinda nani wakati wazalishaji wa ndani *only* wanazalisha 3% ya *maximum capacity* ya uzalishaji wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya yanaumiza sana kwa mtu yeyote mzalendo anaelipenda Taifa lake hawezi kunyamaza akaacha kuzungumza mambo haya yanayofanyika kwenye Taifa hili. Hapa tunapozungumza, *cement* inauzwa shilingi 18,000. *Study* zimefanywa na watoto wetu wa Kitanzania waliosoma kwa kodi zetu. *Study* inaonyesha zote hizi zimefanyika na ni ma-*cartel. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hapa ukimuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu hii ripoti toka taarifa imesemekana ripoti ifanyike, hii ripoti haijawahi kuwekwa hadharani. *It has never been published in the public,* umma uweze kuona

namna gani viwanda vya *cement* vimetengeneza ma-*cartel* kwa kushirikiana na wasambazaji, kwa kushirikiana na wafanyabiashara kuwaibia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme neno moja, kama Bwana Mungu wetu aishivyo, Wabunge wazalendo hatutanyamazishwa kusema mambo yanayowaumiza Watanzania, mambo yanayoumiza watu wetu katika sekta nzima ya uzalishaji na hii inasababisha Serikali yetu inatekeleza *grand project*. Miradi ya *SGR,* miradi ya barabara, miradi ya ujenzi, gharama za ujenzi zinakuwa kubwa, nani wa kulihurumia hili taifa na kuwa na ujasiri wa kuyasema haya na ku-*risk* maisha yake? Nani wa kuwa na huo ujasiri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazungumza hapa ninajua hayo ma-*cartel* kule yananisikiliza. Yataanza kutengeneza hata njama, wanafanya hata njama wakati mwingine ku-*silence* kila sauti itakayosimama kuwatetea Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazungumza hapa *study* imefanywa na hawa vijana na ninakuomba Waziri wangu Mkuu Kassim Majaliwa kwa uzalendo ule ule ulioufanya kaka yangu ya kuagiza *study* ifanyike, tumia uzalendo ule ule tena itisha ripoti hii mtakuja kuniambia Serikali tukiamua kuwa *serious* haifiki mwezi wa sita hapa, bei ya saruji inapaswa kuwa chini ya shilingi 9,000 kuwasaidia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ninaomba nizungumze. Tumezungumza hapa kuhusiana na mambo ya kulinda maadili ya Taifa. Nchi hii haiwezi kuwa na *prosperity* kama tutaacha kulinda tunu za maadili ya kitaifa hili. Hii nchi yetu ni nchi iliyopata uhuru na sababu kubwa ya Mwalimu Nyerere kupigania uhuru wa Taifa hili ilikuwa taifa liwe huru liweze kulinda misingi yake iliyopelekea Taifa hili kuheshimiwa nyakati zote toka Taifa hili limepata uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa wito, Bunge letu kama chombo cha kutunga sheria na kusimamia Serikali ninatoa wito kwa mahakama zetu za Taifa hili, ninatoa wito kwa viongozi wa dini zote. Katika Biblia katika imani yangu, neno la Mungu linasema; "Mungu wetu huwa hadhihakiwi." Pia neno la Mungu katika kitabu kitabu kitakatifu Biblia inasema, "Mungu wetu huwa siyo Mungu wa Kujaribiwa kwa sababu yeye ni Mungu mwenye uwezo na mamlaka."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa wito kwa Serikali, kwa sababu hata haya ma-*NGO* tunayoyaona ambayo yanasababisha kuharibu maadili ya watoto ukiangalia yamesajiliwa na Serikali yetu hii hii ambayo tunazungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawezaje tukasema tunalinda hizi haki za watoto kama tutashindwa Serikali kuhakikisha kwamba tunajenga *platform* na mazingira ambayo yatampa Mungu heshima na tukampa Mungu wetu utukufu ili Taifa letu liendelee kubarikiwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa wito kwa Serikali, ninawaomba sana lindeni vizazi vyetu, walindeni watoto wetu wa Kitanzania kwa kuhakikisha kwamba jambo lolote ambalo litakuja ku-*contravene* na misingi ya Taifa hili inakwenda kudhibitiwa kwa maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kama utaniruhusu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, ahsante sana kwa mchango wako. Sasa naomba nimuite Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi aweze kuchangia.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyenipa afya na nguvu kuweza kuchangia katika Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nimpongeze Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri iliyosheheni, iliyojaa matumaini makubwa sana ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika Jimbo la Lushoto tumepata fedha nyingi sana za miradi. Mradi wa maji mpaka mabilioni ya fedha, mradi wa barabara tumepata mabilioni ya fedha. Mradi wa afya tumepata mabilioni ya fedha, elimu tumepata mabilioni ya fedha na miradi chungu nzima tumepata mabilioni ya fedha. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende katika kuchangia sasa baada ya pongezi hizo. Lushoto kuna barabara kuu moja tu ambayo inaingia Lushoto. Barabara hiyo inaanzia Mombo kupanda Soni hadi Lushoto Mjini ambayo ni kilometa 32. Barabara ile ni nyembamba sana na kila wakati naiongelea barabara hiyo katika Bunge lako tukufu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike hatua sasa maneno haya au uchangiaji wangu huu ufike mwisho. Barabara hii ni nyembamba na inapelekea hata wafanyabiashara wa Lushoto vitu vinapanda bei kwa sababu gari inayoruhusiwa kupita katika barabara ile ni tani 10 tu siyo zaidi ya hapo.

Barabara hii hata Waziri Mkuu amepita na ameiona kwa hiyo niombe sasa katika bajeti hii, barabara ile itengewe fedha angalau itengenezwe hata kwa kilometa tano tano ili Wananchi wa Lushoto waondokane na adha hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo tuna barabara yetu mbadala namshukuru Rais wetu ametupa fedha za barabara ile ambayo inaanzia Dochi kupitia Ngulwi hadi Mombo ambayo ni kilometa 36 lakini bado fedha zile hazitoshi. Inatakiwa iongezwe fedha kwa sababu barabara hii ikitengenezwa itakuwa barabara mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, barabara hii naomba iende itoke *TARURA* iende *TANROADS* kwa sababu gani? Kwa sababu *TARURA* hawana mafungu ya dharura. Kwa hiyo, niombe sasa barabara hii itoke mwaka huu iweze kwenda *TANROADS* na Wananchi Lushoto waweze kupata barabara mbadala hata ile ya Soni – Mombo ikipata dharura basi wana barabara mbadala ya kupita kupeleka mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo niishukuru Serikali inatengeneza Barabara ya kutoka Magamba kwenda Mlola. Barabara ile inatengewa kila mwaka kilometa moja ambayo inagawanywa nusu kilometa kuelekea Mlalo na nusu kilometa kuelekea Mlola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sasa Serikali yako tukufu kwenye Bunge hili la Bajeti itengewe hata angalau kilometa 10 ili barabara iweze kwisha haraka wananchi wangu wa Jimbo la Lushoto au Wilaya ya Lushoto waweze kupata manufaa na barabara ile kwa sababu barabara ile ni ya kiuchumi na ukanda ule una mazao mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye suala la afya, niendelee kuipongeza Serikali inayoongozwa na Mama Samia Suluhu Hassan kwa kutupa vituo vya afya zaidi ya viwili

katika Jimbo la Lushoto lakini vituo hivyo viko Tarafa ya Mlola tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali niendelee kuipongeza lakini sasa bado kuna changamoto ya vituo vitatu vya afya. Mfano Kituo cha Afya Gare, tangia mwaka 2015 naongelea kituo kile cha afya lakini mpaka leo bado hakijatengewa fedha. Sambamba na hayo kuna Kituo cha Afya Kwai bado nacho hakijatengewa fedha. Sambamba na hayo bado kuna Kituo cha Afya Makanya nacho bado hakijatengewa fedha. Niiombe Serikali sasa awamu hii vituo hivi viweze kutengewa fedha ili viweze kufanya kazi na wananchi wangu waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye suala la elimu, niendelee kuipongeza Serikali inayoongozwa na Mama Samia Suluhu Hassan kwani fedha za *booster* zimefika na zimefanya mambo makubwa sana lakini bado kuna changamoto, Wilaya ya Lushoto ina shule nyingi sana. Shule za msingi za Wilaya ya Lushoto ni sawa sawa na Sekondari sawa sawa na Mkoa wa Katavi tena huenda zinazidi. Kwa hiyo, niiombe sasa Serikali iangalie kwa jicho la huruma shule za msingi na sekondari katika Wilaya ya Lushoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo kuna shule ambazo zina hadhi hata ya kuwa na kidato cha tano na cha sita. Mfano Shule ya Sekondari Masange Juu, naomba hii ipandishwe hadhi nayo iwe na kidato cha tano na cha sita. Lakini nayo Sekondari ya Magamba nayo iwe na kidato cha tano na cha sita kwani shule hizi watoto wanakaa mbali sana kwa hiyo, zikiwa shule za bweni naamini kabisa kuwa zitasaidia watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia lingine ni suala la kilimo, Lushoto wakulima wengi ni wa mboga mboga na matunda lakini Mheshimiwa Bashe sijawahi kumsikia kwamba anatoa ruzuku kwenye mboga mboga na matunda wakati mboga

mboga hizi na matunda ndiyo zinachangia pato kubwa la halmashauri. Kwa hiyo, niiombe sasa nayo bajeti hii ya mboga mboga na matunda basi ziingizwe kwenye bajeti nayo ipate pembejeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo kuna suala la *VETA*. Namshukuru Rais ametupa fedha zaidi ya Shilingi bilioni 2.6 kwa ajili ya Chuo cha *VETA* na chuo kile kimeisha lakini wananchi wanauliza; je, ni lini chuo kile kinafunguliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, suala la mwisho ni kumwomba Mheshimiwa Bashe, nilimwomba chakula cha bei nafuu lakini Mheshimiwa Bashe viongozi wako au wataalamu wako mpaka leo hawajaniletea chakula kile. Nikuombe Mheshimiwa Bashe hebu lione hilo sasa Lushoto tuweze kuletewa chakula cha bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Dorothy Kilave aweze kuchangia kwa muda huu uliobaki.

**MHE DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nashukuru kwa kuniona pia niweze kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyeweza kunisimamisha hapa niweze kuongea na kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri yenye mashiko ambayo mengi yamesemwa mule ndani na mengi yanaonekana yakifanyika kwa yale machache basi ninaamini kama Bunge tutaweza kuyafanyia kazi yaweze kuendelea kufanya kazi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa wangu Mama Samia kwa kazi nzuri ambayo ameifanya na anaendelea kuifanya, amekuwa ni mama bora na amekuwa ni mama ambaye hakika mimi amenikosha sana kuifanya demokrasia sasa inafanya kazi nzuri kwa ajili ya mustakabali mzima wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama Samia ameweza kuleta fedha nyingi sana kwenye Jimbo letu la Temeke naweza kusema kwamba ni mabilioni nikianza kutaja moja moja hapa; kwa kweli ninasema inawezekana ni upendeleo mkubwa kwa sababu ni jimbo la mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeweza kujenga mambo mengi, shule za sekondari na kama siku zote tunavyolalamika kwamba tuna watoto wengi kwenye jimbo letu lakini sasa hivi hakuna mtoto anayebaki kuanza shule darasa la kwanza au shule ya awali. Kwa hiyo, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri hii ambayo anaendelea kuifanya na ninaamini bado ataendelea kuifanya kwa miaka inayokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sasa katika Jimbo langu la Temeke. Jimbo langu la Temeke hasa upande wa eneo la Kurasini. Kurasini imekuwa kama ni eneo ambalo la uwekezaji lakini yapo mambo ambayo kidogo hayafurahishi. Tumekuwa na eneo lile *DAWASA* ambalo wanakwenda kumwaga maji taka, watu wako pale ambao eneo lile sasa hivi limekuwa kwa kweli ni kero kwa eneo letu la Jimbo la Temeke hasa upande wa Kurasini. Wameweza kulipa fidia kidogo sana na watu bado hawajaondoka kwa sababu hawajamaliziwa fidia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana Serikali waliangalie hili tena upya. *DAWASA* naamini wanalifahamu vizuri na walishapelekana mpaka mahakamani lakini

walivyoambiwa kwamba wamalizie wale watu mpaka sasa hawajaweza kumaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sio eneo hilo tu Kurasini kama ninavyosema katika Jimbo letu la Temeke ni eneo la uwekezaji. Wako hawa ndugu zetu wa eneo la *EPZ* wana eneo kubwa sana ambalo sasa hivi limekaa wazi halifanyiwi kazi. Lakini wako wananchi waliopewa fedha ambazo kuanzia mwaka 2015 wamelipwa mpaka sasa 2023 bado mapunjo yao hayajakuwa sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe Serikali yangu Serikali sikivu waangalie sasa wananchi hawa kwenye mapunjo haya waweze kufidiwa ili waweze kuondoka katika maeneo hayo hasa lile eneo la *DAWASA* kwa sababu ni kero, kwa sababu hata *DAWASA* wenyewe sasa hivi hawalitengenezi hawalifanyii kazi yoyote nzuri ili wananchi wale waweze kukaa mahali salama. Kwa hiyo, niombe sasa Serikali iweze kuwalipa waweze kuondoka kwa kadri ambavyo afya zao siyo nzuri kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba yapo maeneo mengine ambayo tunatamani sisi kama Jimbo la Temeke tuweze kupatiwa hasa lile eneo la *EPZ* hawajalifanyia kazi mpaka sasa, sisi wenyewe tunalitamani kama Jimbo la Temeke au Halmashauri yetu ya Temeke tuweze kufanyia kazi. Zaidi ya hayo niombe basi Serikali kama inaweza kuifanyia kazi kwa mapema kuweka uwekezaji pale ninaamini vijana wetu wa Jimbo la Temeke na hasa halmashauri yetu watapata ajira kuliko linavyokaa wazi hivi bila kufanyiwa kazi yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa niombe Waziri wa Maji pamoja na Waziri wa Ardhi tuweze kwenda pamoja jimboni tukawasikilize wananchi hawa jinsi gani wanavyolalamika ili tutoe msimamo sasa au Serikali itoe namna gani ya kuweza kuwaondoa wale watu pale kwa

fedha ambazo zimebaki ili wananchi wale waende kukaa sehemu zingine nae neo lile Serikali iweze kuendelea kwa mustakabali wanaoweza kuufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba wananchi wangu wa Jimbo la Temeke wamenituma nimwambie Mheshimiwa Rais tumeweza kuomba na maombi haya tunaomba sana sana Wananchi wa Temeke Mungu azidi kumpa hekima, maono, mafunuo ili aweze kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa jinsi anavyoendelea kuiongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho niombe pia kwamba Jimbo letu la Temeke na Wananchi wangu wa Temeke wamenituma na kusema sisi kama wana Temeke tunalaani vitendo vya ubakaji, ushoga, usagaji na mambo mengine yote yanayofanana na hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa *session* yetu ya asubuhi tutaendelea baadaye naomba kabla sijahitimisha niwataje watakaoanza kuchangia. Ataanza kuchangia Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, akifuatiwa na Mheshimiwa Janeth Maurice Massaburi, na kisha Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan na Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika. Naahirisha shughuli za Bunge mpaka leo saa kumi jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10:00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**12 APRILI, 2023**

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na hoja iliyopo mbele yetu, hoja ya Makadirio na Mapato na Matumizi kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Hapa ninayo orodha ya wachangiaji wa jioni. Tutaanza na Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo atafatiwa na Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Maimuna Pathan ajiandae.

**MHE DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu, lakini nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nitumie nafasi hii kukupongeza wewe kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge hili; tuna imani kabisa ni mtu sahihi kwa nafasi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kumshukuru Rais wetu Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayofanya. Hivi navyoongea kuna baadhi ya vijiji vyangu ambavyo vilikuwa vinaitwa vijiji vya giza; kwa mfano kama pale Changarawe Kata ya Masanze leo hii wamewasha umeme. Pamoja na hayo ndani ya wiki wanaenda kuwasha umeme katika Kijiji cha Ilakala katika Kata ya Muhenga, kule wedo katika Kata ya Kisanga na maeneo mengine ya Jimbo la Mikumi. Zaidi ya vijiji 20 vinaenda kuwasha umeme ndani ya mwezi huu, ni jambo kubwa sana kwetu na kwa niaba ya wananchi wa Mikumi tunaipongeza Serikali ya Rais wetu mama yetu Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kumpongeza Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayofanya akiwa kama mratibu mkuu wa shughuli za Serikali ndani ya Bunge. Nimesikiliza hotuba yake ya bajeti; na niseme tu kwamba nafarijika kuona kwamba miradi ya kimkakati inaendelea, na kule Morogoro ukiondoa Bwawa la Mwalimu Nyerere tuna mradi mwingine mkubwa wa reli ya mwendokasi *(Standard Gauge Railway - SGR)* ambayo kipande cha kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro kimeshakamilika kwa asilimia 97 na kipande cha Morogoro kuja Makutupora kimeshakamilika kwa asilimia 92.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa ya Ofisi ya Waziri Mkuu ni kuratibu shughuli za Serikali na hasa kupambana na umaskini na pia kuhakikisha nchi yetu inafikia kwenye uchumi wa viwanda, ndilo jukumu lake kubwa. Katika hilo tunaona kuna *activities* mbalimbali ambazo zinaendelea lakini kubwa kuliko yote ni uratibu wa kuangalia ni jinsi gani sekta mbalimbali ndani ya Serikali zinawasiliana na zinafanya kazi pamoja ili rasilimali chache ambazo tunazo zitumike kwa tija na ufanisi kwa ajili ya maendeleo ya wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masikini hana anasa ya kutapanya rasilimali chache ambazo anazo; na ndiyo maana suala la uratibu *(coordination)* ni suala la muhimu kuliko yote kwa sababu tukifeli hapo tumefeli pakubwa. Kwa hiyo jukumu la uratibu Ofisi ya Waziri Mkuu ni jukumu kubwa ambalo wanapaswa kulibeba kwa uzito mkubwa. Kufanana na hayo ni TAMISEMI, ambao nao kwa sababu wanagusa sekta nyingi wanapaswa kufanya kazi kwa karibu sana na Ofisi ya Waziri Mkuu katika kuratibu sekta mbalimbali, iwe uvuvi, kilimo, barabara, afya, elimu hata pia usalama katika ngazi ya vijiji, kata, tarafa, wilaya na mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikupatie taarifa ya kusikitisha; sekta ya uratibu ambayo ndiyo roho ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilivunjwa, sababu ya kuvunjwa kwa kitengo hiki

ama idara kamili ambayo ilikuwa inasimamia uratibu wa viwanda, kielimu, uvuvi, ushirika, mazingira, kila kitu ambacho nakizungumza ambacho hakina idara kilikuwa kinaratibiwa kwenye idara ya uratibu wa sekta lakini hakipo. Sasa jukumu la Ofisi ya Waziri Mkuu kwa maana ya kushirikiana kwa karibu na TAMISEMI katika kuhakikisha kwamba wanaenda kuboresha maisha kwa wananchi wetu, idara hii ya uratibu ni muhimu mno katika usimamizi wa shughuli mbalimbali za uzalishaji mali pamoja na pia kupambana na umaskini katika ngazi za chini kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo rai yangu kwa Serikali iangalie sababu za kuvunja idara ya uratibu wa sekta ndani ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Je, sababu hizo zina mashiko na athari yake ni nini kuondoa ile idara? kwa hiyo ni muhimu kuangalia upya uamuzi huo wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia suala la kupambana na umaskini, umaskini si pepo ambalo litaondoka kwa kulikemea ama kwa kunena kwa lugha. Umaskini ni hali ambayo unaweza ukapambana kwa maarifa. Unapopoteza maarifa maana yake umepoteza silaha muhimu sana katika kupambana na umaskini. Ndiyo maana tunasema kwamba suala la uratibu wa sekta mbalimbali kuona jinsi gani tunatumia rasilimali chache ni muhimu mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ambazo tumewekeza kwenye reli ya mwendokasi ni nyingi sana. Vituo ambavyo vinaenda kusimama kwenye mwendokasi pale Kilosa ni vituo ambavyo uwekezaji wake ni mkubwa mno. Najaribu kufikiria, tumejipangaje kuona kwamba uwekezaji huu mkubwa unaenda kulipa? Kwa sababu nikiangalia basi la kutoka Kilombero kuja Kilosa la *freedom* linabeba abiria 20 mpaka 30 hawawezi kwenda kutumia kituo hiki ama stesheni hii ya mwendokasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia abiria wanaotoka Dar es Salaam kuja kilosa sioni nani ambaye anaenda kutumia kituo hiki cha *SGR* kwa maana ya treni ya mwendokasi. Lakini nikijaribu kuangalia ajali za mabasi na malori ambazo zinatokea, ukitoka Dar es Salaam mpaka Morogoro ukitoka Morogoro mpaka Mikumi ajali ni nyingi mno. Mara nyingine tunasingizia tu mwendokasi wa madereva, lakini mwendokasi wa madereva si mwarobaini wa sababu za ajali za barabarani. Wembamba wa barabara, wingi wa magari, ubovu wa barabara ni maeneo muhimu ya kuyaangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa reli hii ya mwendokasi unaweza sana kutusaidia kupunguza ajali pia kupunguza safari za abiria wetu kutoka Dar es Saalam kwenda mikoa ya Kusini, kama tunaweza tukaitumia station hii pale Kilosa kwa umuhimu. Kwa mfano *TRC* inaweza ikawa na makubaliano na wenye mabasi ambayo yanaenda Ruvuma, Songwe, Iringa, Mbeya, Njombe na mikoa mingine ya nyanda za juu kusini wakakata tiketi moja kutoka Dar es Salaam mpaka Mbeya lakini akifika pale Kilosa akaingia kwenye mabasi kwenda Mbeya, Songwe, Njombe. Kipande cha mwendo wa masaa sita tunaweza tukampunguzia huyu abiria saa moja na nusu. Kwa kufanya hivyo tunakuwa tume-*save* muda, kwa kufanya hivyo tunakuwa tumepunguza *stress* ya barabara na foleni barabarani, tukapunguza ajali tukapunguza mwendo lakini tukaongeza ufanisi, kwa maana ya uchumi wa mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linawezekana na tunaweza tukajifunza kwenye nchi za wenzetu jinsi mifumo ya usafiri, kwa maana ya treni za umma na mabasi binafsi yanaweza kuratibiwa katika kurahisisha safari za wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo malori yetu ni mengi sana ukiangalia na barabara zetu. Kuna umuhimu wa kujenga bandari kavu Kilosa. Ujenzi wa bandari hii kavu

itakuwa na mantiki kwa sababu itaenda kuongeza ufanisi wa kituo ambacho kiko pale Kilosa kwa maana ya *station* ya pale Kilosa. Hili likifanyika nafkiri uwekezaji huu mkubwa unaweza kwenda kuwa na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, linalofanana na hilo, kuna bilioni 571 zinawekezwa pale kwenye Kiwanda cha Sukari Ilovo. Tunajiuliza tunaenda kusafirisha vipi zile malighafi, kwa sababu reli ya kutoka Kilosa kwenda kwenye kiwanda kile cha sukari ilishakufa, na sioni jitihada zozote za kwenda kufufua reli ile? Ufufuaji wa reli ile unaenda kuimarisha uzalishaji katika kiwanda kile kinaenda kupunguza gharama ya uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa ile ambayo itakuwa *affordable* kwa mwananchi mmoja mmoja na; kwa maana hiyo inaenda kuleta tija ya uwekezaji mkubwa, ambao Serikali inafanya kwenye kiwanda kile cha Ilovo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji huu mkubwa wa reli sio tu kwamba unaenda kurahisisha maisha ya wananchi tu lakini pia hata utalii kwenye mbuga ya Mikumi. Mtalii anapofika Kilosa anapaswa kusafiri kilomita 100 kwenye barabara ya vumbi kufika Mikumi kuingia getini. Tumeshauri hapa si mara moja si mara mbili, kwamba inagharimu nini Serikali kufungua geti lingine upande wa Kiangali, kwa maana ya Kilosa, Mtalii atakaposhuka na treni ya mwendo kasi pale atembee kilomita 20 aingie getini afanye utalii wake? Hilo tukilifanya maana yake tutaupambanua uchumi wa mji wa Kilosa na vilevile tunaenda kuongeza tija ya reli hii ambayo uwekezaji wake ni mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha barabara barabara ya vumbi kutoka Kilosa mpaka Mikumi ndiyo ambayo tunategemea kuchukua watalii wetu ambao wanashuka kwenye mwendokasi ilia pate nafasi ya kuingia ndani ya mbuga yetu. Kwa kweli kwa hili ndiyo maana nasema kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu inapaswa kusimamia jukumu lake la kuratibu; *TARURA* kusimamia jukumu lake,

kusimamia Wizara ya Maliasili na Utalii pia hata viwanda na biashara, kwa kufanya hivyo huu uwekezaji ambao tunaendelea kuwekeza kwenye mabwawa kwa ajili ya umeme, kwenye usafiri kwa *(SGR)* unaweza kwenda kuwa na tija kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sitendei haki kuchangia bila kuzungumzia changamoto za wananchi wetu hasa mipaka kati ya hifadhi, kwa maana ya *TFS* na vijiji vya kule Mdalasela kwa maana ya Kata ya Mikumi lakini kule Ulaya na baadhi ya maeneo ya Zombo, Nzitokwiva unasimamiwa na *TFS* ambao kila siku wanahamisha mipaka. Wakati umefika sasa tunategemea Serikali kuja kutuonesha mipaka ili wananchi watendewe haki ili waendeshe shughuli zao za kiuchumi kwa uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto kubwa ya wakulima na wafugaji katika Wilaya ya Kilosa. Bado tumeona jitihada za Waziri Mkuu, alikuja kusimamia changamoto ambazo tunazo, lakini hilo halitoshi; tunaomba Serikali itekeleze yale yote ambayo Waziri Mkuu alielekeza akiwa kwenye ziara yake kule Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MWENYEKITI**: Ahsante sana, Mheshimiwa Cecil Mwambe atafatiwa na Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Maimuna Pathan ajiandae.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nishukuru sana kwanza kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia mchana huu kwenye hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa namna anavyoipigania nchi yetu na kupambana ili kuweza kuiweka kwenye mstari ulionyooka, hasa kwenye kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati pamoja na kutoa huduma stahiki kwa

wananchi, kuboresha masuala ya afya, miundombinu ya elimu pamoja na masuala ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pia pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri pia kwa namna ambavyo anatusimamia sisi kama Wabunge na anavyotuunganisha na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hapa ndani wote tuko kama Wabunge na ukitupima kwa madaraja Wabunge sisi wote tunafanana, ni daraja moja kwa sababu tumetokea huko chini kwa wananchi. Wajibu wetu wa kwanza kabisa ni kuismamia Serikali, na wajibu wa pili ni kuishauri Serikali pale tunapoona haifanyi kile ambacho sisi kama Wabunge au wananchi wetu wametuelekeza Serikali ikifanye. Wakati tunafanya mambo haya tunatakiwa kuangalia kuhusu uzalendo wetu na uwajibikaji wetu kwa Taifa kama namba moja lakini kwa wapiga kura na sehemu ya tatu tunatakiwa kuwajibika kwa chama chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo pamoja na haya yote nitahakikisha kwanza ninalilinda Taifa langu kabla ya chama changu. Nitahakikisha ninawalinda wapiga kura wangu kabla ya chama changu halafu baadaye nitakilinda chama changu dhidi ya haya yote niliyoyataja hapo juu na ndipo nitapata ustawi sahihi na kuweza kuwasimamia na kuwaongoza watu wetu. Nayasema hayo, nataka nishauri Bunge lako na ikiwezekana lishawishike kwamba, kwa kadiri mambo yanavyokwenda tuna haja ya kubadilisha kanuni ili ripoti ya CAG ifanyiwe kazi na Bunge kabla hatujapitisha bajeti nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu zangu za msingi mojawapo kubwa ni kwamba, bajeti hii tunayokwenda kuipitisha ndiyo ile ambayo inalalamikiwa kwamba hapo nyuma pamefanyika ubadhirifu na kuna watu bado wataendelea kupelekewa fedha za Serikali wakiwa bado

madarakani. Simaanishi kwamba tuijadili hii bajeti kwa sasa hivi, lakini kwa nia ya kubadilisha kanuni badala ya kusubiri mpaka mwezi wa kumi na moja ambayo itakuwa ni takriban miezi sita toka pesa mpya zilipopelekwa kwenye wizara tofauti ambazo nyingi zinalalamikiwa, watendaji wanalalamikiwa. Tumemsikia Mheshimiwa Rais naye akitaja baadhi ya watu kwamba wanalalamikiwa kwenye haya mambo. Kwa hiyo kimsingi ilitakiwa watu hawa kwanza wawajibike kabla hatujawapelekea pesa zingine ambazo inawezekana wakaenda kuzitumia kwa mtindo ule ule, kwa sababu watajua kwamba itakapofika Mwezi Novemba sisi kama Bunge tutajadili tutaweza kuondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tubadilishe kidogo mtindo wa ufanyaji wetu wa kazi hasa inapokuja ripoti nzito kama hizi, kwa sababu kuna haja ya kujadili ripoti ya *CAG* na kuona mapungufu kabla hatujafanya *location* ya pesa zingine kwenye maeneo yale yale ambayo tayari kuna matobo makubwa ya matumizi mabaya ya pesa za wananchi. Ndio wale tuliosema tunawalinda, tunalinda Taifa lakini baadaye tunajilinda sisi wenyewe na tunataka tuone chama chetu kinaendelea kuongoza nchi hii, lakini haya lazima tuyasimamie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nilipata nafasi ya kuuliza swali hapa asubuhi; nilikuwa naongea kuhusu barabara ya Nachingwea Masasi. Nakumbuka hapa Waziri wa Fedha alimpa taarifa Mbunge mwenzangu ambaye tunapakana kwenye eneo la mpaka wa Nachingwea. Kwamba mradi wa utekelezaji wa barabara kati ya Masasi na Nachingwea utatekelezwa hivi karibuni. Majibu ya Waziri kama umefatilia vizuri na kuyasikia hapa leo naye amesema upande wao wameshamaliza na taarifa hizi zimekwenda Wizara ya Fedha, ili sasa waweze kutengewa fedha ya utekelezaji wa mradi huu, lakini kimsingi hakuna kinachoendelea mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama watu wa Masasi, Nachingwea na huko hatujaona *mobilization* inafanyika pale, kwa hiyo tafsiri yake hilo jambo haliwezi kufanyika siku za karibuni. Wilaya ya Nachingwea ni wilaya ambayo inafanana karibia sawasawa kabisa na umri wa uhuru wa nchi yetu, haijawahi kupata barabara ya lami, haijawahi kuunganishwa na sehemu nyingine yoyote yenye lami. Ndiyo maana sisi tunapokaa hapa tunaongea tunashauriana tunaambiana kwamba tunataka Serikali ifanye haya mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali ipo, majibu haya sisi tunayapokea na hii sio mara ya kwanza basi watueleze kama inashindikana sisi tumezoea kufanya michango kwenye baadhi ya maeneo. Tunachanga ili kujenga madarasa kuisaidia Serikali na sasa hivi nataka watuambie ili tukaweze kufanya michango sisi watu wa Mtwara, Lindi na Nachingwea tuweze kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati ikiwemo pamoja na barabara ya Mtwara, Mnivata-Newala, ambayo nayo ahadi zimekuwa nyingi. Newala- Masasi haijatekelezwa, hatuoni nini pale kinachoendelea pamoja na kwamba hivi karibuni wamelipa fidia lakini hii ya Nachingwea – Masasi ndio tatizo kabisa siku zote tunapewa majibu haya yanayofanana. Kwa hiyo tunaomba Serikali watuambie kama haipo kwenye bajeti yake inashindikana kwa sababu hatujui kilichofata hapo mbele basi sisi kama wananchi wa maeneo haya tuchangishane kwa kukata kwenye mazao yetu ya kilimo pamoja na korosho shilingi 20 ili tukajenge hiyo barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongelea kipande cha kilometa 42, Masasi-Nachingwea, lakini Wilaya ya Nachingwea ina zaidi ya umri wa miaka 60. Kwa hiyo Serikali kama hata ingeamua kujenga kilometa moja moja toka wakati huo, sasa hivi wangekuwa wameshaenda mbali zaidi ya Nachingwea na wanakaribia kufika Liwale. Kwa hiyo tutakapotoka hapa tutakwenda kuwashauri watu wetu kama inawezekana basi tuchangishane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba, Mheshimiwa Waziri wakati anawasilisha mpango wake alisema kwamba uchumi wetu unayumbayumba na kwamba inawezekana uchumi ukatoka kwenye asilimia 4.2 kwenda asilimia 3.9. Sababu zinazotajwa katika haya mambo ya kupanda kwa bei za vitu na mengine, ni pamoja na vita ya Ukraine pamoja na Russia pia na yale masuala ya *covid*. Sasa sisi kama Taifa mpango wetu ni nini? Tunayo miradi yetu mikubwa ya kimkakati tunayo suala la Liganga na Mchuchuma, suala la reli ya kusini, suala la Bandari ya Mtwara, tunayo haya mambo ya gesi ambayo hayatumiki ipasavyo tungeweza kuachana na sababu hizi ndogondogo za kiuchumi kwa sababu kama vita itaendelea kwa miaka 20 manake uchumi wetu bado utaendelea kudorora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nataka niombe, kwa sababu tuna taarifa za *CAG, CAG* akakague; na Mheshimiwa Mwenyekiti utaniongoza kuna hili suala la *ETS* tumelalamikia muda mwingi hapa kwamba ndiyo kati ya vitu ambavyo vinaongeza *inflation* kwenye bei za bidhaa mbalimbali. *CAG* sasa akakague na kuona kama tender hii ya *ETS* bei zilizopo na athari zilizopo kwenye soko atuletee taarifa hapa sisi kama Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka pia *CAG* akakague na kuangalia Mfuko wa Pembejeo. Ukija Mtwara kwenye zao letu la korosho kuna Mfuko wa Pembejeo wa Pamoja. Mfuko huu umeshafanya kazi zaidi ya miaka mitatu, lakini pia haupo kisheria, ndiyo tunataka *CAG* akakague atuletee hapa taarifa, kama Mfuko bado unatufaa sisi au kama haufai basi uondolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tunataka kufanyiwa *review* kwa *export levy,* kodi inayotozwa kwenye masuala ya korosho. Pafanyiwe *review* pia katika tozo mbalimbali ambazo zinatozwa kwenye korosho, hela ya korosho kila mara inaanguka, wakulima wanapata hasara, makampuni

yanapata hasara, uchumi wa maeneo yetu unadorora kwa sababu tunategemea zaidi zao la korosho, lakini watu wanashindwa kuja kununua kwa sababu ya tozo zilizopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata sisi ziara ya kwenda kwenye nchi wanakozalisha korosho, nchi ambako wanatumia mfumo kama wa kwetu. Sisi Tanzania peke yake ndiyo tuna hizi kodi hapa tunazozitaja. Sasa ni wakati wa kuona kama ni kweli kodi hizi zinastahili ama kodi hizi hazistahili ili tuweze kwenda sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo linaumiza sana wananchi ni masuala ya fidia kwenye maeneo mbalimbali. Kwenye Jimbo la Ndanda tuna mgogoro mkubwa sana na wa siku nyingi wa eneo kati ya Jeshi la Magereza pamoja na wananchi kwenye Kata ya Namajani kwenye Vijiji vya Ngalole pamoja na Chiroro na maeneo hayo. Toka mwaka 2012 Mahakama ilitoa *award* kwa wananchi na kuwaambia kwamba eneo lile lirudishwe kwa wananchi, Serikali haijafanya hivyo, magereza haijafanya hivyo. Katika bajeti hizi zote sijaona popote ambapo imetengwa fedha ya kwenda kuwapa wale wananchi fidia zao ili waweze kuachia hayo maeneo. Kwa hiyo kama Serikali imeshindwa, tutakapokuwa tunamaliza Bunge na tunakwenda kwenye Wizara ya Ardhi, watueleze ili tukawambie wananchi sasa wakalime kwenye yale maeneo yao, waachane na huu mpango wa Serikali kwa sababu hautaweza kutekelezeka karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la fidia pia. Barabara inayotokaa Nanganga inakwenda Ruangwa nyumbani kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, inakwenda pia na kuunganisha na Wilaya ya Nachingwea. Palibomolewa pale majumba ya wananchi wa kawaida, palibomolewa misikiti, lakini pamoja na Ofisi yetu ya Chama cha Mapinduzi, hakuna fidia iliyolipwa mpaka sasa hivi na wananchi wanapouliza

Serikalini wanasema fungu la fidia lilikuwa halijaandaliwa. Tunaka tutakapokuwa tuna *wind-up* haya mambo basi tuweze kupata majibu ya pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nisisitize kwenye yale niliyoyasema kwamba kwa vyovyote vile tunahitaji uchunguzi wa kina wa kuona kama Mfuko huu wa Pembejeo unaosimamia Mikoa ya Mtwara, Lindi na maeneo yote wanayolima korosho bado uko *viable* na kwamba *CAG* akaukague tupate taarifa hapa kwa sababu itakuja ndani ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kama hayo niliyoyasema, kwa hiyo, naomba nisisitize kufanyike ukaguzi ili wananchi waweze kupata majibu na sisi kama Bunge tubadilishe Kanuni, tujadili taarifa ya *CAG* kabla hatujatenga pesa kwa bajeti inayofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Janeth Masaburi, atafuatiwa na Mheshimiwa Maimuna Pathan na Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, ajiandae.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kabla siajaanza kuchangia naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye amenipa kibali cha kuweza kusimama hapa katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie kumshukuru Mungu, kwa sababu kabla sijaanza kazi hii ya ubunge tulikula kiapo kwa kutumia Biblia na wenzangu Waislam, ndugu zangu walitumia *Quran* Tukufu. Kwa hiyo tunapokwenda kufanya kazi kwa kumtumia Mwenyezi Mungu, twende kufanya kazi kwa kumheshimu na kumwogopa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya yeye na wasaidizi wake Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri wote, Watendaji wote wa Serikali pamoja na Wabunge, wamefanya kazi kubwa sana kwa kuhakikisha kazi na maendeleo yanaendelea katika nchi yetu. Mheshimiwa Rais, aliahidi kwamba atafanya kazi na *slogan* yake ni "Kazi Iendelee" baada ya kurithi kazi aliyoiacha marehemu Dkt. John Magufuli. Mheshimiwa Rais, aliahidi ukweli na amefanya kazi, amepambana sana, tumetembelea miradi mingi, tumeona mambo makubwa yanayofanyika, Mama amefanya kazi kubwa sana tena ya kijasiri. Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa wananchi, tunaomba tumuunge mkono Mheshimiwa Rais, ana nia njema sana katika nchi hii. Tumpe nguvu, tumwombee kwa Mwenyezi Mungu, aweze kutimiza ahadi zake alizoahidi kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amani na usalama katika ngazi ya familia. Suala la maadili na malezi ya watoto wetu yanashabihiana na amani na usalama katika ngazi ya familia. Sisi wazazi na walezi tulitetereka katika kulea watoto, tumeachia wadada wa kazi kulea watoto, tumeachia watoto majirani kutunza watoto sisi tunahangaika na kutafuta pesa. Matokeo yake watoto wamejilea wenyewe, watoto wetu wamebakwa, watoto wamelatiwa, watoto wamejifunza tabia tofauti kinyume na maadili, sasa tunalia, tufanye nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile mfumo wa elimu yetu hauko sawa katika kulea watoto au kufundisha watoto kuanzia ngazi ya shule za awali. Serikali iwekeze kwenye shule za awali kwa kuweka walezi wazuri ambao watamtengeneza mtoto, huyu mtoto ambaye anakuja kuwa kiongozi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tukumbuke kisa cha Sodoma na Gomora. Naomba kunukuu hii Sodoma na Gomora kitabu cha Biblia utasoma mwanzo 19, mstari wa 23 – 26 inasema, nanukuu: "Jua lilipokuwa limechomoza juu ya nchi ya Lutu alipoingia Sowayi ndipo bwana akanyesha juu ya Sodoma na juu ya Gomora kiberiti na moto toka mbinguni kwa bwana, akaangusha miji hiyo ya bonde lote na wote waliokaa katika miji hiyo na yote yaliyomea katika nchi ile lakini mkewe Lutu akatazama nyuma yake akawa nguzo ya chumvi." mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna wake wengi wa Lutu katika nchi hii ambao wanataka tugeuke nguzo ya chumvi ambao wanatetea suala la ushoga, lakini tunasema alipo shoga kuna basha, lakini wanaoonekana wengi hapa ni mashoga, mabasha wako wapi? Basha huwezi kumtambua kirahisi na mabasha ndiyo wenye pesa. Namuunga mkono dada yangu Dkt. Thea anasema waasiwe, tunasema kabla hajaasiwa na kukuhumiwa kwanza wachapwe viboko hadharani, kama nilivyoona kule Wahindi na kama nilivyo waona Waganda na wale Wamasai walivyo mchapa yule mtu aliyewasaliti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo nawakumbusha tena kuna habari za gharika kuu, uwasi wa mwanadamu kwa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu alinyesha mvua siku 40 usiku na mchana akaifuta ile nchi yote chini ya uongozi wa Nabii wake Nuhu. Hiki kitu kinachoongelewa siyo mzaha, tumeongelea miradi mingi inafanyika katika nchi hii, matrilioni ya fedha yanatumika katika nchi hii, tuna madini, tuna maziwa, tuna bahari, tuna rasilimali nyingi katika nchi hii. Nchi hii ilipendelewa na Mwenyezi Mungu, lakini tuwekeze kwa watoto waadilifu. Haya tunayosema kuna majizi, wala rushwa, yote inatokana na ukosefu wa malezi tangu mtoto mdogo. Mtoto mdogo kuanzia kuzaliwa mpaka miaka sita anaiga kila kitu. Ukimtengeneza ataiga kitu kizuri, usipomtengeneza ataiga kitu kibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende Serikali tukawekeze kwenye malezi ya watoto. China wamewekeza kwenye malezi ya watoto wao, Singapore wamewekeza kwenye malezi, kuna nchi zimejifungia kutengeneza kizazi kitakachoweza kushika nchi. Tunaweza kukataa ndoa za jinsia moja maana yake unakataa uumbaji wa Mwenyezi Mungu, zaeni mkaongezeke, watu wanazuia watu wasizaliane, wingi wa watu ni tishio, China wako wengi wanatisha dunia, India inatisha dunia kwa sababu ya wingi wa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuja kudanganywa na uzazi wa mpango. Ule ni uongo wa kutuzuia tusizae ili tuendelee kuwa dhaifu. Ahadi ya Mwenyezi Mungu, ni kuzaa, utazaaje unatengeneza wanaume kuwa wanawake? Sisi wanawake ambao tunashika mimba miezi tisa unaambiwa umezaa mtoto gani? Wa kiume, zamani ulikuwa unaulizwa umezaa mtoto gani? Mwanajeshi, leo unaenda kutoa litoto linakuwa nyoronyoro, litoto langu kama lile mimi naweza kulipoteza tu, siwezi kuona vitu vya namna hiyo, haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kuwa na mtoto msenge halafu bado namchekeachekea, nitahama hata kama mji, kama nipo Dar es Salaam nitahama, siwezi kukaa na mtoto msenge. Tunaongea kwa lugha laini laini inakera sana, inanikera, inaniudhi na nawapongeza Viongozi wa Dini wameongelea kwa nguvu sana. Nampongeza Waziri Nape nimemwona juzi ameongea, lakini kila Mbunge sauti yako ni sauti ya Mungu, usiposema utahukumiwa na Mwenyezi Mungu, utakuwa umemsaliti Mwenyezi Mungu, kuungana na wale watu wa Sodoma na Gomora. Hatuwezi kufanya kazi kubwa katika kuendeleza nchi hii tukaanza kufumbia macho masuala haya. *(Makofi)*

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issa J. Mtemvu, taarifa.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mzungumzaji anaendelea kuzungumza vizuri. Kwenye eneo la maadili hilo nilitaka nimkumbushe tu, si tu wazazi kule nyumbani, si tu Serikali kutengeneza mifumo ambayo itatuwezesha kujifungia ndani na kutengeneza msingi mzuri wa malezi kwa Watoto, lakini inasemekana hata ndani ya Bunge kuna hao unaowazungumza, hata ndani ya Bunge inasemekana, kwa hiyo Mheshimiwa Mwenyekiti, sina uhakika yanasemwa tu kwa hiyo ndiyo maana tunapata ugumu wa kulea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issa unachangia hiyo taarifa na kuzungumza. Mheshimiwa Janeth Masaburi, taarifa unaipokea?

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Hii taarifa naipokea. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa sababu nitakuwa mwongo mbele za Mwenyezi Mungu. Wenye tabia hiyo waache, tunawajua, wengine viongozi, hatutaki kusema sana, tunamwogopa Mungu si mwanadamu, haya ya dunia ni ya kupita tu. Leo niko hapa kwenye hiki kiti kesho sipo na kesho nipo labda nimekufa, lakini Mungu apewe sifa yake, Mungu ahidimiwe Mungu ndiye mwenye kutukuzwa na Mungu ndiye mwenye kuogopwa. Sisi wanadamu siyo kitu, tuko duniani kesho tunapita lakini kizazi lazima tukiendeleze kwa sababu ni ahadi ya Mwenyezi Mungu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutasifia ndiyo lakini kwa nini watu wanafanya hivyo na hizo *NGO* kubwa naona zina…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana, muda wako umekwisha, tunakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Namwita Mheshimiwa Maimuna Pathan, atafuatiwa na Mheshimiwa Deodatus Mwanyika na Mheshimiwa Kunti S. Majala ajiandae.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuongelea Bajeti ya Waziri Mkuu. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia uhai wake na pia tunamshukuru sana Rais wetu Mama Samia Suluhu kwa miradi ambayo ametuletea pesa nyingi katika nchi yetu na miradi hiyo inaendelea. Tunampongeza sana na tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Waziri Mkuu, tumeiona iko vizuri sana. Tunashukuru imekwenda vizuri na waliofanya kazi, kwa kweli wamechakata wamefanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina nyongeza ya mambo ya msingi sana yanayoendelea, lakini hayana matokeo mazuri. Naongea kwa masikitiko makubwa sana na maumivu makubwa sana kutoka moyoni mwangu. Wananchi wa Mkoa wa Lindi Wilaya ya Liwale na Wilaya ya Nachingwea wanavyouawa na wanyama tembo. Ukienda kwenye mashamba ya wananchi wale utatoa machozi, utalia njaa itakayotokea sasa hivi ni kubwa mno. Tuna vijiji vingi ukienda maeneo yanaitwa Nditi, Namapwiya, Ngumichile, Mbute, Nyambi, Mwandila, Matekwe, Majonanga na ukienda Liwale; Kibutuka, Mkutano, Lilombe na Kilangala inasikitisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ni mbaya wamepelekwa Askari Wanyamapori wachache. Hivi kwa hali ya kawaida kwenye shamba wakiingia tembo hamsini kwa mara moja hawa askari wetu wawili, watatu wataweza kufanya ile kazi

kweli? Wataweza kweli? Hali ni mbaya. Mwisho juzi kuamkia jana kuna kijana amefariki ameuawa na tembo mchana kweupe katika maeneo ya Mwinyichile saa tisa mchana, amejitoa nyumbani akasema akaangalie shamba lake kama limebakia mahindi kidogo au alizeti, amefika kule yeye ndiye wamemfanya chakula inasikitisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitegemea ingetokea hali ya dharura, ya tahadhari ya haraka ya kupeleka helikopta, lakini tumelizungumzia sana. Haijapelekwa helikopta kufukuza wanyama wale mpaka leo lakini angeuawa ndovu mmoja ingeenda helikopta na maaskari pale kwenda kuwaletea vurugu wananchi, inasikitisha sana hii hali, inasikitisha mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najiuliza na wananchi wa kule wanajiuliza ndovu na binadamu nani ni muhimu? Inafikia wakati wanasema mtapigiwa kura na ndovu, siyo kwamba wanaongea vile kwa kutulaghai ni hatua na uchungu waliokuwa nao. *(Makofi)*

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahya Mhata, taarifa.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la tembo kwa kweli ni la hatari sana. Hata Jimboni kwangu tembo ni tatizo, kwa hiyo namuunga mkono kabisa mzungumzaji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Maimuna taarifa unaipokea?

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea taarifa. Hali ni mbaya. *(Makofi)*

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, nimeona kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mzungumzaji pia kwamba kule kwetu Arumeru Mashariki, Kijiji cha Kilinga, tembo wamehamia kwenye nyumba za wananchi. Hali ni mbaya sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitegemea sisi wananchi wa Mkoa wa Lindi hali ya dharura ingetokea, kwa sababu ndovu wanaoingia kwenye shamba moja ni zaidi ya Hamsini, wanapelekwa askari wawili, watatu wanashindwa wanakimbia na wao wanaondoka. Wabunge wenzangu na viongozi mbalimbali wameripoti hicho kitu mara chungu nzima, tulitegemea wangeleta helikopta kufukuza wale wanyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali iko tofauti. Tunajiuliza wangeuawa ndovu wawili pale pangetulia vile, wananchi wetu wangepona kweli? Inasikitisha sana. Tunaomba…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine, kuna wahanga wananchi wetu wa Wilaya ya Kilwa Masoko na wa Nachingwea kulikuwa na upanuzi wa viwanja vya ndege, walitwaliwa maeneo yao, ni siku nyingi, lakini mpaka sasa hivi hawajawapa pesa zao. Hiyo hali inakatisha tamaa na inarudisha maendeleo. Pia kuna barabara hii ya Masasi – Nachingwea – Liwale. Hii Barabara tangu 2015 kila siku tunaambiwa ipo kwenye upembuzi yakinifu, kila siku tuaambiwa inajengwa, kwani hii keki ya Taifa na sisi pia hatuitaki? Tugawane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba na sisi barabara ile ni ya muhimu ni ya kimkakati ile barabara itengenezwe. Jamani ikinyesha mvua dakika kumi tu, huwezi kupita ile barabara.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna, endelea na mchango wako.

**MHE MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba mtuangalie kwa jicho la huruma. Kuna akinamama, kuna vitu vingi, kilimo kikubwa kule kinaendelea, lakini hatuna barabara, lami hatuijui kule kwetu. Watu wanazaliwa mpaka wanakufa. Tunaomba watusaidie tuwekewe lami barabara ile, kila siku tunapigwa danadana na maelekezo, lakini ilani haitekelezeki, ni kwa nini hii huku tu? Tunaomba watusaidie barabara itengenezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna migogoro ya wafugaji na wakulima. Hali ni mbaya, kuna watu wanauawa, tuna uhakika na tuna uthibitisho watu wameuawa na wafugaji. Tunaomba watusaidie, hali ni mbaya ni mbaya sana, kwa hiyo hakuna amani, hakujatulia watusaidie wenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaomba malambo kwa ajili ya mifugo, Mheshimiwa Dkt. Samia, aliahidi yafufuliwe yatengenezwe tunaomba tusaidiwe kwa Mkoa wa Lindi, hakuna kabisa malambo hali ni mbaya. Pia tunaomba na *scheme* za umwagiliaji kwa sababu kilimo cha sasa hivi mvua haziaminiki. Mabadiliko ya hali ya hewa ni kila siku, tunaomba tusaidiwe tupate na *scheme* za umwagiliaji ili vijana wetu waweze kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mikoa ya Kusini karanga na alizeti zinastawi sana lakini wananchi wa kule

wanashindwa kulima vizuri kwa sababu hawana mbegu nzuri. Tunaomba Serikali sikivu ilete mbegu na wataalam kule wa kuweza kuwaelewesha wale ndugu zetu kilimo cha karanga na alizeti. Pale Nachingwea kuna maeneo yalikuwa yanaitwa *farm* one mpaka *farm* 17, yale maeneo yalikuwa maeneo mazuri sana kwa ukulima wa karanga. Zilikuwa zinatoka karanga nzuri sana lakini sasa hivi watu wakilima hakuna, tunaomba Serikali yetu sikivu itusaidie tupate mbegu nzuri na tupate na Wagani waweze kuwaelimisha watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deodatus Mwanyika atafuatiwa na Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota ajiandae.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Kama wenzangu walivyosema nianze kwanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Amiri Jeshi Mkuu, Samia Suluhu Hassan, kwa mambo yote ambayo Wananjombe na hasa katika Jimbo langu tumeyaona yakija katika maeneo yetu. Tumekuwa na miradi mikubwa ya maji, kero ya maji ilikuwa ni kero kubwa sana katika Halmashauri ya Njombe lakini sasa tunayo miradi mikubwa miwili inayoendelea Mkandarasi anakwenda vizuri. Afya kwa mara ya kwanza wananchi wa Njombe sasa wamepata *CT scan* na wanaweza wakaacha kufunga safari kwenda Mikoa ya jirani kwa ajili ya kupata huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa barabara kwa kweli tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais tunayo barabara ya Itoni kwenda mpaka mpakani na Ludewa ambayo ilikuwa ni changamoto kubwa sana. Barabara hiyo sasa Mkandarasi yupo *site*, bilioni 95 zimekuwa *allocated* na ina kilometa 55. Baada ya kusema hayo niende kwenye kuchangia lakini

nimshukuru sana sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa hotuba yake aliyoitoa hapa Bungeni na Wasaidizi wake wote waliohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchangia mambo kama matatu ama manne kama muda utaniruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza kabisa ni kilimo na mifugo. Kwenye kilimo, Jimbo la Njombe lina mazao mbalimbali lakini zao la kimkakati linalotambuliwa Kitaifa ni zao la chai, nami napenda kuliongelea zao hili kwa kuanza kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu lakini kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe. Kilio kikubwa kilikuwa ni bei na wananchi walikuwa wanalalamika sana kuhusiana na bei ya chai na nililiongea hapa, baada ya vikao vya wadau, Serikali ikiongozwa na Mheshimiwa Bashe, wameweza kufikia mahali ambapo hata kama siyo pale ambapo wananchi walipataka angalau sasa hivi bei ya kilo ya chai ilikuwa inauzwa shilingi 314 kwa kilo, imefika 366 kwa kilo. Walipenda sana ingefika 400 lakini uhalisia ndiyo huo, kwa hiyo tushukuru kwa hicho kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema wananchi hawa, wakulima hawa wanaweza wakapata hata hiyo shilingi 400 kwa sababu ukiweza kulima kwa ubora kuna malipo yanaitwa *bonus payment,* ukiweza kulima ukapata ubora ambao ni asilimia 68 unapata *bonus payment* ya Shilingi 90 kwa kila kilo. Ukilima ukapata ubora wa asilimia 75 unapata *bonus* ya karibu shilingi 112 kwa kila kilo, kwa hiyo uwezekano wa kufika 400 inawezekana, sasa ni nini ambacho kinaweza kikafanyika na Serikali na nitoe ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa hapa ni umwagiliaji, Serikali iliongeza bajeti ya kilimo hapa na sehemu kubwa ya bajeti hiyo ilikwenda kwenye maeneo ya umwagiliaji, lakini kwa masikitiko makubwa sana wakulima wa chai kwenye miradi ya umwagiliaji bado hawajaingizwa,

hakuna kinachoendelea kwa wakulima wa chai kwenye upande wa umwagiliaji. Ninaomba Serikali iweze kuhakikisha kwamba hata wakulima wa chai wanaingizwa kwenye miradi. Miradi hii imeendelea kuwa kwenye *scheme* nyingine tu lakini kwa wakulima wa chai hakuna

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunacho Kiwanda cha Chai pale kina–*process* chai kinaitwa Kabambe. Kiwanda kile kina *capacity* Kubwa lakini kinatishiwa kufungwa kwa sababu uwezo wa kuki-*feed* kiwanda ni mdogo. Wakulima wa chai wamejitahidi walipoweza kufika lakini bado hawawezi kufikisha na jambo linalozuia ukiacha suala la umwagiliaji ni suala la miundombinu wezeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Serikali ilikubali kutoa fedha kutusaidia kwa upande wa barabara, lakini kwa masikitiko makubwa nipende kusema tuna tatizo kubwa sana la ujenzi wa barabara ambazo ziko chini ya *TARURA*. *TARURA* inatakiwa ijipange vizuri kuweza kusimamia Wakandarasi wajenge hizi barabara haswa za maeneo wezeshi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jinginje ninapenda kiliongelea kwenye mifugo ni kiwanda cha maziwa ambacho kipo katika Mji wa Njombe. Ninaongea kwa masikitiko makubwa sana kwenye kiwanda hiki, ni kiwanda pekee ukiacha viwanda vya *avocado* au parachichi kiwanda pekee ambacho kinakusanya maziwa, kiwanda hiki kilipata mkopo wa Benki ya Kilimo - *TADB* lakini kiwanda hiki kimefungwa kimesimama, niliomba hapa msaada wa Serikali uweze kuingilia mpaka leo haijaweza! Ninasikitishwa sana na *ethical behavior* na *integrity* ya *TADB* kwenye kushughulikia suala la kiwanda hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba wananchi wafugaji wana-*own* asilimia 30 ya kiwanda hiki, ungetegemea *TADB* wao wana jukumu la ku-*promote* na kusaidia wafugaji na wakulima, kwa hiyo wangeingia katika

*scheme* ya kuasaidia hata kama wamekopa na kwamba fedha hazijarudishwa. Wananchi hawa kwanza *TADB* wao wenyewe wako *responsible* kwa *default* kwa kiasi kikubwa kwa sababu hawakutoa fedha kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TADB* walichofanya kwa masikitiko makubwa, wamechukua madalali kwenda kuuza kile kiwanda na siku zote wanapeleka madalali karibu na sikukuu wakati watu hawapo, wameuza eneo la shamba lakini wameuza *warehouse* kwa milioni 500, kwenye kiwanda ambacho thamani yake ni bilioni 2.6 hii hakiubaliki na tunaomba Serikali iingilie kunusuru maisha ya wakulima hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana tu nimesikia tena hapa baada ya kuuza jingo, *TADB* wamekwenda tena na dalali mwingine wanataka kuuza mashine! Nadhani *TADB* ilianzishwa kwa minajiri ya kuwasaidia wafugaji, wakulima ili waweze kujikomboa. Wakulima na wafugaji 1,000 wa sekta hii ya maziwa watakwisha maisha yao kabisa iwapo Serikali haitasaidia, siyo kwamba hawawezi kulipa hilo deni, mkakati wa kilipa hilo deni upo lakini *TADB* wana-*interest* na ndiyo maana nimesema *ethical behavior* ya *TADB* lazima iangaliwe, nina uhakika *CAG* ni eneo ambalo anatakiwa akaliangalie.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo jingine napenda niliongelee ni eneo la usafiri wa anga. Mji wa Njombe kwa kweli tuna uhitaji mkubwa sana wa kuwa na kiwanja cha ndege. Napenda kuiomba sana Serikali iweze katika bajeti inayokuja iweze kuona hata kama hatutaweza kupata ujenzi wa kiwanja cha ndege *upgrade* ambayo inafanyika sehemu nyingine lakini kwa kuanzia angalau fedha ziwe *allocated* tuweze kuona eneo hili kubwa la uchumi linapata huduma ya usafiri wa anga wa uhakika. Tuna Wawekezaji wengi kwenye maeneo mengi, wangependa kuja katika kuwekeza katika Mkoa huu wa Njombe na Mji wa Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipitisha sheria hapa ya Uwekezaji. Mimi napenda kuiongelea Sheria ya Uwekezaji wa harakaharaka. Wakati tunaongea hapa tuliiomba sana Serikali na ninashukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu ameongelea kwamba Serikali itaendelea kuangalia kuboresha mazingira ya biashara, pia itaendelea kuangalia sera zake kwa nia ya kuboresha. Moja ya maeneo ambayo tuliomba na ninaomba liendelee kuangaliwa kwa haraka ni kuangalia uwezekano wa kuona ni namna gani viwanda katika nchi yetu vinaweza vikapelekwa kwenye maeneo mengine kwa kuweka *incentive scheme,* tunaliomba hilo na tunaomba Serikali iendelee kuliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili watu wengi hatuliangalii kwa umakini, ni lazima tufanye mambo kwa mkakati tunaagiza ndege ya mizigo, hiyo ndege ya mizigo haitakuwa *economical* kama itakuwa inakwenda kuchukua mizigo tu ambayo ni ya kilimo na kupeleka sokoni. Inatakiwa iwe na mizigo mingine inayopeleka maeneo hayo na mizigo hiyo ukianzisha viiwanda na shughuli nyingine za kiuchumi ndipo unaweza kuifanya hii ndege iweze ku-*add* value katika maeneo yetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa sekunde 30 malizia mchango wako.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapo na naunga mkono hoja.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanyika, Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mheshimiwa Jumanne Kishimba, ajiandae.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nami nafasi niweze kutoa

mchango wangu kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru hotuba ya Waziri Mkuu ukurasa wa 42 mpaka 43 umezungumzia suala la ardhi kama mtaji, pili kutokana na ardhi tuliyonayo kuwekuwa na migogoro mingi hali kadhalika nayo ameizungumzia kwamba sasa tunakwenda kwenye suala zima la utatuzi wa migogoro ili ardhi yetu iweze kutumika kama mtaji kwa maana kwenye sekta ya kilimo, sekta ya mifugo, sekta ya maliasili na sekta nyingine zote kwa sababu ardhi ndiyo kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya maneno mazuri yaliyoandikwa kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, yamekuwa yakiandikwa kila hotuba ya kwake ya Waziri Mkuu lakini pia na ya kisekta kwenye Wizara zake husika. Tumekuwa tukizungumza suala zima la migogoro ya ardhi, Serikali imekuwa bado haituelewi, sijajua changamoto ni nini haswa, wanaona raha hiyo migogoro kuendelea kuwepo hapa nchini, ama kuna kitu wananufaika nacho kutokana na hii migogoro, sijaelewa! Wakija wataniambia kwa nini Serikali haitaki kutatua migogoro ya ardhi ya kiutawala lakini na migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji, migogoro ya ardhi baina ya maliasili pamoja na watumiaji wengine wa ardhi?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Chemba mgogoro baina ya maliasili pamoja na wananchi. Pori la Swagaswaga tumelizungumza, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili, Waziri wa TAMISEMI, Mifugo, Maji, kadhaa Mawaziri Nane walienda kwenye Pori la Swagaswaga, wakaenda wakazungumza na wananchi wakawaeleza hali halisi iliyoko pale. Wale wananchi wameanza kuishi pale kabla ya uhuru, wameishi pale kabla ya Serikali kwenda kuanzisha hifadhi, wameishi pale kabla hata ya uanzishwaji wa vijiji miaka ya 1970 huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Serikali hiyo hiyo imejenga shule, imejenga zahanati, ni wapiga kura wanapiga kura pale, Serikali inawatambua, leo wakigeuka upande wa pili wa shilingi wanaambiwa ni wavamizi, mmevamia eneo la hifadhi, watu wanapigwa, watu wanauawa, watu wanafanyiwa manyanyaso ya kila aina, mpaka ubakaji unafanyika kwenye Hifadhi ya Swagaswaga. Hiki kitu siyo sawa!*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Mawaziri Nane imekwenda imepeleka wataalam, wamepeleka wataalam pale! Wataalam wameenda wamepima, kwa nini Serikali inakuwa na kigugumizi cha kutoa tamko la suala zima la wananchi wa Pori la Swagawaga kuendelea na maeneo yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu wamelima mmeenda kufyeka mahindi ya wananchi wangu, kwa sababu gani za msingi? yaani mtu mmemuacha anaenda analima, anapanda, mazao yanaota, yanakua, mnaenda mnafyeka siyo laana hiyo? Siyo laana hiyo?

**MBUNGE FULANI:** Ni laana!

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini mvua inyeshe? Kama Mwenyezi Mungu anatuletea mvua ya bure hatuilipii tunalima, tunapanda, mnaenda mnafyeka eti kisa hifadhi! Hivi tusipokuwepo leo hifadhi zitakuwa zina thamani gani? Tusipokuwepo binadamu hifadhi zitakuwa na thamani gani?*(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti kuna taarifa kutoka kwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wana muda wa kujibu wangetulia tu.

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge anayeongea hivi sasa, kwamba sisi kama binadamu na hata viumbe waliopo hapa duniani tuna-*balance* kwa *eco-system*. Tusingeweza kuishi peke yetu bila kuwepo na wanyama, kuwepo na mimea, kuwepo na hifadhi, kuwepo na rasilimali zote zilizopo hapa nchini. Kwa hiyo, nataka kumpa taarifa kwamba hifadhi ni za muhimu asizione kama ni kitu ambacho hakihitajiki hapa duniani au hapa Tanzania.

Mhehsimiwa Mwenyekiti, pili nampa taarifa pia kwamba athibitishe kama kuna watu wameuawa, watu wamebaka, vinginevyo aondoe hii kauli.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kunti, taarifa hii unaipokea?

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yeye ni Shahidi alikwenda Swagaswaga, mmefika pale mmeambiwa kwani mnachoficha ni nini? Hivi watu wale wananawake wanapoumia wewe unanufaika na nini? Lakini suala la kwamba eti tuna-*balance* tunahitaji, sawa tunaitaji tumepewa Mwenyezi Mungu ametupa hizi rasilimali ziweze kutusaidia na kutunufaisha watu wote sote, hawa wanyama wanufaike na sisi binadamu tuweze kunufaika. Leo kwa nini mnaona thamani ya mnyama kuliko binadamu? Kwa nini mnaweka thamani ya mnyama ni kubwa kuliko binadamu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Wizara wakija kuhitimisha waniambie mgogoro wa Swagaswaga unaisha lini Wilaya ya Chemba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la misafara ya Viongozi. Viongozi wetu tunawaheshimu na tunawapenda na tunajua changamoto kubwa wanazo kwa majukumu yao wanayoyafanya. Hivi kweli tunasema muda ni mali, wakati ni mali, kusimamisha wananchi zaidi ya masaa matatu barabarani, Kiongozi hajatoka atokako, tuna wagonjwa, tuna watu wanatakiwa kwenda kutekeleza wajibu na majukumu yao mbalimbali. Mimi ninaomba Viongozi wetu wanaosaidia hususan wa Wizara ya Mambo ya Ndani, Polisi biashara ya kusimamisha wananchi mabasi sijui magari mengine na wananchi wengine watumiaji wa barabara kwa ajili ya viongozi wetu wanapopita waende kwa sababu wana mawasiliano. Wawe wanawasiliana kwa kadri muda unavyosogea wawe wanawaacha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Waziri Mkuu alikuwa natatoka nyumbani kwake kuanzia Saa Mbili na Dakika Kumi na Saba magari yamesimamishwa foleni imefika mpaka Nzuguni. Tunapandisha uchumi huo? Uchumi unapanda? Kusimamisha, sasa hiyo ni moja lakini je, fikiria hapa alikuwa anatoka hapo Mlimwa, kama Waziri Mkuu ameamua kutumia leo magari kutoka Dar es Salaam mpaka aje afike hapa Dodoma wananchi watasimama kwa muda gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana hivi vitu vingine hebu tuwe tunaenda na wakati na kwa safari ndefu niombe Viongozi wetu Wakuu watumie ndege waache kutumia magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye suala zima la maadili.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Kuna taarifa Mheshimiwa Kunti.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja.

**MWENYEKITI:** Kuna taarifa Mheshimiwa Kunti. Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**T A A R I F A**

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Wewe utakuja kujibu lakini.*(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Hapana Mheshimiwa Kunti si ungekaa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge, tunafahamu wote kwamba utaratibu wa utendaji kazi wa viongozi wetu umewekwa kwa mujibu wa taratibu mbalimbali ambazo zinasimamia pia heshima ya viongozi wetu hapa nchini.

Kwa hiyo, suala la namna ya ku–*control* hilo ni la watendaji ambao wako chini ya mamlaka zinazohusika. Kwa hiyo, nadhani ingekuwa ni bora tu kwa Mheshimiwa Mbunge kutoa ushauri kwa mamlaka zinazohusika badala ya kuhusianisha na utendaji kazi wa Viongozi wetu ambao umewekwa kwa utaratibu unaozingatia heshima ya Viongozi wetu pia hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tukiliweka hivyo litakuwa na *logic* nzuri zaidi kuliko kuendelea kusema Waziri Mkuu, kiongozi fulani. Tuende katika utaratibu ambao ni wa

usimamizi wa kiusalama na mambo mengine. Pia ni *practice* ambayo ipo katika ulimwengu mzima, *practice* ambayo imekuwa ikitumika katika kutoa heshima kwa Viongozi wetu na kuzingatia utaratibu ambao unatumika katika uendeshaji wa shughuli za viongozi na Serikali katika ulimwengu mzima.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti taarifa unaipokea.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mwongozo wa Spika.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako. Tunajua kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, taarifa kuna muda maalum na imekuwa tabia ya Bunge hili Mawaziri kutumia muda wa Wabunge vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko kwenye kuchangia Bajeti kama wanataka kujibu, wasubiri kwa muda wao wa Kikanuni wa kujibu watapewa nafasi. Kama taarifa hatukatai lakini waende *specific* kwenye hoja na watumie muda wa Kiti vizuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti malizia mchango wako.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Bunge ni kuishauri Serikali, ndiyo tuko na wananchi kule chini, tunaona adha za wananchi, tunawashauri. Mkiona inafaa tekelezeni, mkiona haifai basi *to hell* haina shida.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu maadili katika jamii yetu. Nilikuwa najiuliza kwa sauti nawaza, nikawa nasema hivi Serikali ina kila uongozi kule chini, kwenye Mtaa tuna Viongozi, kwenye Kata tuna Viongozi, kwenye Wilaya tuna Viongozi, kwenye Mkoa mpaka Taifa, hawa watu wanaosagana, hawa watu wanao sijui mwanaume anaenda

anamngonokea mwanaume mwenzie, halafu ukiangalia hivi hii inaingiaje akilini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu wako kwenye mitandao tunawaona, wanajisifu, Serikali mpo. Wanadhalilisha Taifa letu, mmekaa kimya. Baraka, tukiona Wamachinga wako pale *One Way,* tunapeleka mgambo na polisi kwenda kuwachapa, wasagaji na wanaofanyana mambo ya ajabu ya kudhalilisha Taifa mmekaa kimya, hamsemi la heri wala la shari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Mama Massaburi anachangia, Mheshimiwa Mtemvu akasema na Wabunge tupo. Sasa nikawa nashindwa kushangaa, ndiyo maana hatuchukui hatua kwa sababu na sisi Wabunge tunafanyiwa haya maneno! Kama mimi Kunti nahusika, nafanywa na mwanamke mwenzangu; nafanywe na mwanamke mwenzangu? Inakuwaje? *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kunti, muda wako umeisha.

**MHE. KUNTI Y. MAJALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ichukuliwe hatua. Biashara ya wanawake kufanyana na wanaume kufanyana wenyewe kwa wenyewe, ikome katika Taifa letu. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, atafuatiwa na Mheshimiwa Jumanne Kishimba na Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, ajiandae.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ambayo ipo Mezani pako ambayo ni hoja ya Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nami nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya kwa Watanzania ambayo ni kazi tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya, lakini kwa kutuletea hotuba ambayo ina matumaini kwa Watanzania. Amegusa kila sekta. Pia tunamwona Waziri Mkuu jinsi anavyohangaika kuisimamia Serikali, tunamwona anavyosimamia miradi mbalimbali ya Serikali, na anavyofanya ziara kufuatilia maagizo ya viongozi wengine. Kwa hiyo, tunampongeza sana Waziri Mkuu kwa kazi tukufu anayoifanya. Tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu ampe afya njema, aendelee kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza pia Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Profesa Ndalichako kwa kazi nzuri anayoifanya, pamoja na Naibu Waziri. Kipekee nawapongeza kwa jinsi walivyoratibu shughuli za Mwenge katika Mkoa wetu wa Mtwara. Wametoa usaidizi wa kutosha na shughuli zilifana. Nachukua nafasi hii kumpongeza Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Mheshimiwa Kanali Abbas kwa jinsi alivyosimamia zoezi hili, na uzinduzi ulifanyika kwa kufana sana. Nampongeza yeye pamoja na Kamati mbalimbali ambazo zimehusika katika shughuli ile ya Mbio za Mwenge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utaanza kujikita kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu, Ukurasa wa 30 ambao unazungumzia kwamba, Serikali itaendelea kuratibu upatikanaji wa pembejeo, viuatilifu na mbegu. Kipekee naipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa kazi kubwa ambayo inaifanya katika kuwekeza katika tasnia ya korosho. Tumeona kwa muda wa miaka mitatu mfululizo Serikali ikitoa

pembejeo bure kwa wakulima wa korosho. Tunaendelea kuishukuru Serikali na mwaka huu kuna mikataba yenye thamani ya shilingi bilioni 340 ambayo imetolewa. Nina matumaini pembejeo hizi zitafika kwa wakati na wakulima wa korosho watanufaika na pembejeo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri ufuatao: Pamoja na uwekezaji huu ambao umefanywa kwenye tasnia ya korosho, bado kuna anguko la uzalishaji wa korosho katika nchi yetu. Msimu wa mwaka 2017/2018 Tanzania tulifikisha tani 320,000, lakini kwa masikitiko makubwa msimu huu uliopita uzalishaji umepungua hadi tani 160,000 pamoja na uwekezaji mkubwa uliofanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiuliza Bodi ya Korosho, hawana majibu ya uhakika, ukiuliza *TARI* Naliendele, hawana majibu ya kutosheleza. Napendekeza iundwe tume huru ya kufuatilia nini kimeikumba tasnia ya korosho mpaka kukawa na anguko kubwa kiasi hiki? Kwa sababu haiwezekani mikoa ya uzalishaji wa zao la korosho imeongezeka, Serikali inawekeza vya kutosha, lakini tumetoka kwenye tani 340,000 hadi tani 120,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ndogo tu, *Ivory Coast,* kila mwaka wanaongeza zaidi ya tani 100,000 na mwaka huu wamefikisha tani 1,000,000. Malengo ya Bodi ya Korosho mwaka huu ilikuwa ni kufikisha tani 400,000, lakini tumeishia kupata tani 160,000. Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi inasema tutakapofika msimu wa 2025 tufikishe tani 700,000. Kwa anguko hili tuna kazi kubwa sana ya kufanya ili kufikia malengo ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba uunde tume huru ili kuchunguza nini kimejiri? Ninapendekeza tupate wataalamu kutoka nje; kuna wataalam kutoka *SUA;* tusiendelee kuwatumia wale wale wa *TARI* na wa Bodi ya Korosho kwa sababu watatuletea majibu yale yale ambayo

tumeyazoea. Tupate timu mpya, ikiwezekana twende hata nchi nyingine tuchukue wajumbe, kwa mfano, *Ivory Coast* ambao wamezalisha vizuri. Msumbiji wanafanya vizuri, tuchukue uzoefu kutoka huko, kwa sababu, tukileta *TARI* au watu wa Bodi ya Korosho watatupa majibu yaleyale ambayo kila mwaka bado uzalishaji unapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza hadidu za rejea ya tume hiyo vile vile iangalie mfumo wetu wa uagizaji na udhibiti wa pembejeo. Kuna malalamiko kwamba pembejeo ambazo zinaingia kwenye tasnia ya korosho hazina ubora unaotakiwa. Kwa hiyo, Tume hii tutaipa na kazi hiyo, waangalie; je, hizi pembejeo ambazo zinaingia kwenye tasnia ya korosho zina ubora unaotakiwa? Zinatoa matokeo ambayo tunayatarajia? Kwa sababu haiwezekani tukaambiwa kuna mabadiliko ya tabia ya nchi wakati Mtwara na Msumbiji tunapakana na Mto Ruvuma; Msumbiji wanafanya vizuri, lakini Mtwara haifanyi vizuri. Kuna kitu ambacho hakiko vizuri katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili utajikita katika kuifungua Mtwara. Naipongeza Serikali kwa kazi kubwa sana ambayo imeifanya katika kuufungua Mkoa wetu wa Mtwara. Kuna uwekezaji mkubwa kwenye Bandari yetu ya Mtwara, kuna uwekezaji mkubwa katika kiwanja cha ndege na maboresho katika barabara, lakini kuna kazi ambayo ninatakiwa ifanyike ili Mtwara yetu iweze kufunguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ya Mnivata – Newala – Tandahimba mpaka *Mbamba Bay,* kipande cha kilometa 160. Tumekuwa tukibadilisha tarehe ya kuanza utekelezaji. Tulikutana na Katibu Mkuu akatuambia Machi tutaanza utekelezaji, lakini jana tumesikia jibu hapa kwamba ni mpaka Juni. Changamoto ni nini? Hii barabara ianze kujengwa. Barabara hii ni kiunganishi kizuri na kitakamilisha *Mtwara Corridor* ambayo itafungua mikoa ya Mtwara,

Ruvuma, Njombe mpaka *Mbamba Bay*. Kwa hiyo, naomba huo mchakato wa ununuzi uendeshwe haraka, ili barabara hii iweze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ya Masasi – Nachingwea, ni ya muda mrefu, kwa nini haitengewi fedha za kutosha ikajengwa? Vilevile kuna suala ambalo ukichukua vitabu vya bajeti miaka mitano, tutakuwa tunazungumzia reli kutoka Mtwara hadi *Mbamba Bay* na Tawi la Mchuchuma na Liganga. Kila mwaka tunataja, lakini utekelezaji haupo. Naomba Serikali yangu sikivu tuanze kuutekelea huu mradi. Mradi huu kama nilivyosema, utaifungua mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Njombe na hivyo tutafungua ushoroba wa kusini.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chikota kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kuchauka.

**T A A R I F A**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwongezee taarifa Mheshimiwa anayeongea. Ametaja *Mtwara Corridor;* kwa ufahamu wangu, naona *Mtwara Corridor* imeshakufa. Kwa sababu, *Mtwara Corridor* ilitegemewa kuifungua, kama *route* aliyoisema; lakini kwa miaka saba niliyokaa Bunge hili sijawahi kuona mradi wa barabara Mtwara wala barabara Lindi, zaidi ya barabara iliyotajwa Mnivata, kila mwaka inatajwa, na hii barabara ya Nachingwea – Masasi. Hakuna barabara yoyote Mkoa wa Lindi iliyotekelezwa kwa muda wa miaka saba yote niliyokaa hapa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chikota, taarifa unaipokea?

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea. Niongezee kwamba, ile barabara inaitwa barabara ya Masasi – Nachingwea mpaka Liwale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna mradi wa maji kutoka Mto Ruvuma kupeleka maji Mtwara Manispaa. Mradi huu ni mkubwa na mradi huu una mwaka wa saba sasa. Kwenye kitabu cha Wizara kunabadilika maneno tu, tunatafuta fedha, tunafanya usanifu, tunafanya mazungumzo. Mradi huu ni muhimu sana kwa Manispaa ya Mtwara. Mradi huu siyo kwa Manispaa ya Mtwara tu, utanufaisha Wilaya ya Mtwara, lakini vilevile na Halmashauri ya Mji wa Nanyamba kwa sababu, chanzo cha maji kipo Maembechini; lakini wananchi wamesitisha kufanya shughuli zao za maendeleo kwa kupisha mradi huu. Fidia haijalipwa bado, lakini vilevile hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba mradi huu ambao ni muhimu kwa upatikanaji wa maji kwa uwekezaji wa Mji wa Mtwara, kwa sababu, hata Kiwanda cha Dangote kina mahitaji makubwa sana ya maji. Mradi huu ukitekelezwa, basi hata na Kiwanda cha Dangote kitapata maji ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mradi huu utekelezwe na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jumanne Kishimba, atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, na Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, ajiandae.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nami nampongeza Mheshimiwa Rais, Waziri Mkuu na Mawaziri na watumishi wote wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaliongea kidogo suala la *CAG,* lakini siyo kwa tarakimu. Suala hili la *CAG* linatupa wakati mgumu sana na sioni kama kuna uwezekano tutakwenda labda miaka 10 wizi hautaisha. Labda tutafute namna ambayo ni nyepesi kidogo. Kwa nini *CAG* anakagua baada ya tukio? Kwa nini *CAG* asianze kabla ya mradi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yangu ni kawaida mbwa huwa anabweka wakati kuna mwizi ili mwenye mali atoke, lakini mbwa akibweka baada ya kuibiwa, kuna uwezekano kwamba mbwa hakuwepo kwenye eneo lile. Kwa hiyo, tumwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama itakupendeza, tuwe na Wizara ya Matumizi na Wizara ya Kero. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, anayetayarisha mradi ni Katibu Mkuu na watumishi wake kwenye Wizara au sisi Halmashauri. Tunashauriana kwa sababu ya pesa zilizopo, tunaamua tufanye mradi. Hapa kwenye mradi, anachoangalia *CAG* ni kile kilichotoka nje ya ule mradi, lakini asilimia 80 ya miradi ile haina mahitaji yoyote kwenye jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano wa masoko yetu. Ni kweli, soko la ghorofa unatarajia kweli ujenge soko la ghorofa uweke nyanya watu wakanunue na umetumia shilingi bilioni 30; haiwezekani! Yaani tubishe, yaani tuone kabisa, tunaona soko la kawaida liko mahali pale, unaweka soko la shilingi bilioni 40 kwenda kuweka nyanya na samaki, watu watafuata kweli kwenda kununua? Kama kungekuwa na Wizara ya matumizi, huu mradi ungepelekwa kwao, wakauangalia kwamba huu mradi; je, unafaa? Kama wanaona unafaa, wampelekee na *CAG* na TAKUKURU wauangalie ndiyo uje Bungeni. Ingekuwa muda huu tunazozana fedha hazijaenda, lakini sasa hivi tunazozana pesa zimekwenda, tena tunaidhinisha bajeti nyingine. Tutafanyaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunaiona miradi yetu asilimia kubwa haina faida kwa wananchi, badala yake tena inakuwa kero. Leo unabebwa kutoka hapa unaambiwa huwezi kuteremka na basi hapa na mvua inanyesha, lazima uende mwisho kwenye stendi ya Nane Nane. Umetoka Bahi, ni shilingi 5,000 kuja hapa. Ukiteremshiwa Nane Nane kurudi tena huku, ni shilingi 10,000. Huyu mwananchi tunamwadhibu kwa sababu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo utatengeneza mradi; huo mradi wako ulichukua hela zetu, ukatengeneza mradi mbaya, halafu leo unatuadhibu sisi tena wenye hela. Tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu alifikirie kwa mapana sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nimemuunganisha Waziri wa Matumizi na Waziri wa Kero? Nafikiri mmeona hoja hapo ya Mheshimiwa Kunti ilivyokuwa. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri Mkuu, inatupa wakati mgumu sana sisi kukabiliana na Mawaziri kwenye matatizo ya hoja, lakini kama kuna Waziri wa Kero, sisi tutapeleka kero zetu kwake yeye, yeye ndio atazipeleka kwa Waziri Mkuu. Maana yeye hahusiani na kitu chochote, ni kama Waziri asiye na Wizara Maalum. Itatusaidia sana. Kuna kero nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunalia ajira. Leo daktari anamaliza *University Muhimbili,* anakuja hana kazi, lakini haruhusiwi hata kufungua *kiosk* kuchoma watu sindano, lakini Mmasai anatembeza dawa na ana kibali cha Wizara ya Afya. Sasa tunafanyaje? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu umechukua milioni yake 40, baadae ukamfunga pingu, haruhusiwi tena kuuza dawa, lakini mtu ambaye hakusoma, anatembeza dawa. Samahani ndugu zangu Wamasai kama mpo. Anatembeza dawa, tena

anakwambia inatibu magonjwa 40, unakuja saa ngapi? Sasa unafanyaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima twende upya. Mabadiliko ni makubwa sana duniani. Lazima tufungue vitu vingi sana, kero ni nyingi mno. Leo wote humu ni mashahidi. Tunapanda ndege kutoka hapa Dodoma kwenda Dar es Salaam, hapa unasachiwa, unafika Dar es Salaam unasachiwa tena. Je, ulipakia abiria huko angani? Nani alipanda angani? Sasa tutamwambia nani? Hakuna wa kumwambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaenda barabara yetu ya mwendokasi. Mwendokasi unaona ziko nne, upande huu kuna daladala zaidi ya 100, lakini haziruhusiwi kuhamia huku, lakini huku hakuna watu, lakini nao si wanalipa deni hilo hilo! Mvua inanyesha, wamo mle kwenye daladala wameshika mkono, kwa nini wasiruhusiwe watu wa daladala wakatumia hii kwa muda mpaka tutakapopata mabasi? Maana hawa na wenyewe si wanalipa deni. Je, ikitokea mwenye funguo za ofisi yuko kwenye daladala, wewe wa mwendokasi ukawahi, faida ya mwendokasi itakuwepo? Si utakuwa mlangoni! Haitawezekana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, najaribu sana kufafanua kwamba, akiwepo Waziri wa Kero na Waziri wa Matumizi, sasa hivi ndiyo ungekuwa muda wetu kubanana kwamba, mradi huu tumeukubali uende, mradi huu bwana kama unataka kuuza nyanya kwa shilingi bilioni 20 hatutaki. Katengeneze banda la shilingi bilioni tatu, wanunuzi wa nyanya watanunua. Kwa hiyo, tunge-*save* sana. Huu mvutano wote usingekuwepo. Nafikiri mnafahamu kesi ya *CAG* ilivyowahi kuleta matatizo mengi mno kwenye Serikali. Mengi mno!

Mheshimiwa Mwenyekiti na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hiyo, tukuombe ulifikirie kwa makini sana. Pia bado

najiuliza, Serikali imeamua kurudi kwenye biashara. Kilichoifanya ikatoka miaka ya 1980 na miaka ya 1990 kimebadilika? Watu wa miaka ya 1990 na 1980, na hawa wala *blue band* wa leo, kama wale walishindwa waliokuwa wanakula mihogo, hawa wala *blue band* wataweza biashara? Kweli tumeamua kurudi kwenye biashara? Kweli tutaweza? Kwa haya matatizo tu yaliyotokea haya ya wizi, tunarudi kwenye biashara tena za gharama kweli, tutaweza kuziendesha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukiwaona matajiri, asilimia 80 hakuna mzima. Mwingine ana *gout,* mwingine ana *pressure,* yaani kutwa nzima makoti yamejaa vidonge: Je, itawezekana kweli! Au kwa kuwa, Serikalini ninyi mnastaafu miaka 60, mnataka kumtelekezea nani huo mzigo? Maana mzigo huo ulishatelekezwa miaka ya 1990, tukauza na viwanda, tukasema jamani tunatoka, sisi tunarudi kwenye kodi, lakini *immediate* tunaenda moja kwa moja tena kwenye biashara. Kabla hatujaanza biashara, nusu ya hela imeibiwa. Sasa hiyo biashara tutaianzaje? Nani atatuletea hela? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hiyo, tunaomba sana hili suala la *CAG* tubadilishe huu utaratibu ili tujadili hela kabla ya wizi wenyewe. Baada ya hapo, nakushukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kishimba. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo la wageni wa Mheshimiwa Mbunge. Wako wageni 55 wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, Mbunge, ambao ni wanafunzi wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, atafuatiwa na Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, na Mheshimiwa Venant Daud Protas, ajiandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa kuchangia Hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza, nianze kwa kukupongeza wewe binafsi kwa kuendelea kukalia Kiti na kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, niipongeze sana Serikali yetu ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Makamu wa Rais na Mawaziri wote, kwa kazi inayoendelea kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Pwani napenda kushukuru sana kwa miradi mbalimbali iliyotekelezwa ndani ya Mkoa wetu wa Pwani kwa kipindi hiki cha miaka miwili tangu Mheshimiwa Rais Samia ameingia madarakani. Tumeshudia mwaka ulioishia Juni, 2022, Mkoa wetu ulipokea fedha za ziada zaidi ya bilioni 20 kwa ajili ya miradi mbalimbali ukiwemo ujenzi wa madarasa, ujenzi wa vituo vya afya, miradi ya maji n.k. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mwaka huu wa fedha unaoendelea mpaka sasa licha ya kwamba tumeshapokea bajeti ya zaidi ya asilimia 75 ya pesa za miradi ya maendeleo. Lakini tumepokea pia nje ya bajeti zaidi ya bilioni 10.6 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ukiwemo ujenzi wa madarasa 341. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuja na pesa za kumalizia miradi iliyokuwa inatekelezwa na Mradi wa *EP4R* ambapo jana nilipita Bagamoyo nikakuta pesa, milioni 100, Shule ya Sekondari Kingani kwa ajili ya kumalizia bwalo, na miradi hiyo ilikuwa mingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pesa hizo, niombe Serikali inapopanga miradi hii ya maendeleo, hususan ujenzi wa madarasa na vituo vya afya ambako unatoa pesa za kiwango cha aina moja, niishauri Serikali iangalie maeneo kwa mfano ya visiwa, hayafanani. Kwa hiyo, unatoa pesa kwa maeneo yanayolingana kwa kiwango kimoja lakini yapo maeneo ambayo miundombinu siyo rahisi kufikika, na hapa narejea Visiwa vya Mafia, Mkuranga na Kibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa Mkuu wa Wilaya pale Rufiji anajua mazingira. Leo ukitenga pesa inayofanana na Kata za Mbuchi, Kiongoroni, Salale na maeneo mengine kwa kweli pesa hizi zinakuwa hazitoshi na inasababisha halmashauri zetu kutumia pesa ya ziada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, niseme pia nina ushauri. Nimeisoma Hotuba ya Waziri Mkuu katika ukurasa wa 66, masuala mazima ya uwezeshaji wa wananchi. Hapa niombe kuishauri Serikali, ina mifuko zaidi ya 63 ya kuwezesha wananchi ambayo ipo katika Wizara mbalimbali, ifike wakati sasa ile mifuko iunganishe. Pengine iwe chini ya Waziri Mkuu au moja kwa moja Ofisi ya Mheshimiwa Rais ili wananchi wengi, hususan wanawake, wapate kuelewa fursa zinazotokana na mifuko hii ili waweze kufaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ushauri huo, napenda kuipongeza Serikali, katika Mkoa wetu wa Pwani kwa mara ya kwanza wamekuja na Mji wa Viwanda, eneo la viwanda, Kongani ya Viwanda Kwala. Na uwekezaji mkubwa uliofanyika pale na namna ambavyo imeweza kuweka mpango mkakati mzuri mji ule utakuwa wa mfano wa kuigwa na utazalisha ajira 100,000 ambazo ni rasmi na nyingine zaidi ya 300,000 zisizokuwa rasmi; kwa hiyo, naishukuru Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapa pia naomba niikumbushe Serikali pia eneo la ujenzi wa viwanda Bagamoyo na eneo la ujenzi wa bandari Serikali bahati nzuri imekuja na mpango mzuri tu wa kutumia sekta binafsi na Serikali yenyewe kujenga bandari na hili eneo la viwanda lakini naomba niikumbushe ulipaji wa fidia wa maeneo hayo, wananchi wetu wa Bagamoyo wamesubiri muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hapa tumeona Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Angellah Kairuki, ametangaza nafasi za kazi. Niishukuru sana Serikali kwa kuendelea kutoa ajira kwa vijana wetu; nafasi zaidi ya 20,000. Na naishukuru kwa sababu imekuwa na kawaida tangu Rais Dkt. Samia ameingia madarakani kila mwaka amekuwa akitoa kibali kwa ajili ya nafasi za kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri; kuna vijana wengi wanajitolea, walimu na sekta ya afya, na imewahi kusemwa hapa Bungeni kwamba zikitokea hizi ajira vijana wale hawafikiriwi kabisa. Kama sasa hivi anakubalika kujitolea kwa nini inapotangazwa ajira rasmi aonekane hana sifa? Na nimeona tangazo na vigezo, Serikali iseme neno. Na Mheshimiwa Spika alitoa maelekezo kuwa Serikali iseme neno kwa vijana wanaojitolea ambao leo sasa neema imeshatangazwa, taratibu zake zikoje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masuala ya miundombinu niishukuru sana Serikali kipekee kwa ujenzi wa Daraja la Mbuchi. Daraja hili Mheshimiwa Waziri Mkuu amefika na hata wananchi wa Mbuchi wamesema waziwazi, kwa ukombozi kupitia daraja lile kwa kweli hawana namna, ni kumuunga mkono Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sijitendei haki kama sitachangia suala zima la maadili. Tumeona namna gani Wabunge na hata viongozi wa dini na wananchi mbalimbali wamekuwa wakilisemea. Tumeona ongezeko la vitendo vya ubakaji na kulawiti kwa watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka jana tu, 2022, matukio zaidi ya 12,000 kulinganisha na matukio 11,000 yaliyotokea mwaka wa fedha uliopita. Pamoja na adhabu mbalimbali wanazopewa, kifungo cha miaka 30, niiombe Serikali kwa kuwa matukio yanaongezeka, iandae mdahalo wa Kitaifa tujue tatizo ni nini hasa na iangalie hii sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeisoma hotuba ya Waziri Mkuu, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na mambo mazuri aliyosema juu ya ulinzi wa watoto, ningefurahi kama angegusa walau hata mapitio ya sheria, walau hata mapitio ya kufanya mdahalo kujua chanzo ni nini. Kwa nini kuna ongezeko kubwa la matukio haya; nini kimebadilika sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana tu tumesoma baba mzazi amembaka mtoto wa mwaka mmoja Iringa huko; hili siyo jambo la kawaida. Na matukio yamekuwa yakiongezeka mara kwa mara. Kwa hiyo, niiombe Serikali, na niunge mkono, inaonekana adhabu ya miaka 30 haitoshi, adhabu iwe kuhasiwa tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nimpongeze Mkuu wetu wa Wilaya ya Bagamoyo, yeye ametoa kabisa maelekezo; hakuna Mtendaji wa Kijiji wala wa Kata wa kutoa barua ya kudhamini wanaofanya matendo haya ya ubakaji. Yale makosa yanadhaminiwa lakini tukiweka msingi huo wa kutodhamini, kwa nini adhaminiwe. Mtoto ameharibika! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Bagamoyo ndani ya wiki tatu tu watoto zaidi ya watano wamebakwa na kulawitiwa na wamelazwa katika Hospitali yetu ya Bagamoyo. Na zaidi ya kesi 10 ziko mahakamani kwa kipindi kifupi tu. Kwa hiyo, napenda kusema hali ni mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa Ripoti ya *CAG;* na mimi naunga mkono kubadilisha kanuni. Kwa sababu kuna vikundi mbalimbali vimeshajadili, vimeshatoa hukumu, vimeshatoa maelekezo kabla Serikali haijapata nafasi na *CAG* kuja kwenye Kamati za Bunge. Itakapofika Novemba nachelea kusema tutakuja kufanya nini. Kwa sababu Watanzania wameshaaminishwa vya kuaminishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa Mkaguzi wa Hesabu Ofisi ya *CAG* na utaratibu huu wa *CAG* ulianza tangu 2007, hivihivi anawasilisha taarifa kwa Mheshimiwa Rais baadaye anakuja Bungeni inawasilishwa anakutana na Wenyeviti wa Kamati, wanazungumza, taarifa inakuwa *public* inaendelea kujadiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama tutaacha msingi wa kila mtu atakayeona inafaa anajadili na kutoa hukumu na kujumlisha hasara zilizopatikana bila utaratibu mahususi kwa kweli Mwenyekiti tutakuwa hatulitendei haki Bunge. Zinatajwa hasara mbalimbali wakati nyingine pengine siyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri tupate fursa na sisi kama Wabunge, kwa sababu ndio tuliokasimiwa kwa niaba ya wananchi, tuijadili ripoti ili iwe rasmi kuliko ilivyo sasa; vyama vya siasa vimejadili, wananchi mbalimbali wamejadili, wameshatoa hukumu zao wakati pengine hali ilivyo sivyo inavyoafsiriwa kwenye taarifa za *CAG.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nimalizie taarifa ile pia nayo ni ya kitaalam. Niwaombe Watanzania, siyo kila hoja ni ufisadi, tutatishana bure.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Subira.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** …lakini tuipe nafasi ili ufafanuzi utolewe. Naunga mkono bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu; nampongeza sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Subira. Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, atafuatiwa na Mheshimiwa Venant Daud Protas, Mheshimiwa Haji Amour Haji ajiandae.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kuweza kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nitumie fursa hii kuwapa pole sana wananchi wa Jimbo la Kijini pamoja na wananchi wa Jimbo la Nungwi, hasa katika Vijiji vya Kidoti, Tazari na Kilimani kutokana na athari za upepo mkali ulioharibu nyumba na mali zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali yangu tukufu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuona namna ya kuweza kuwafariji wananchi wale waliopata majanga yale ikizingatiwa kwamba upepo ule ni miongoni mwa athari za mabadiliko ya tabia nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, mchango wangu ninapenda kuuelekeza moja kwa moja katika suala zima la maadili, mila, sinka na taratibu za Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, duniani muda huu tuliokuwa nao nchi zote zimeweza kugawika katika makundi mawili; zipo nchi zinaokubaliana na masuala ya ushoga, ndoa za jinsia moja, lakini zipo nchi pia ambazo zinapinga vitendo hivi. Hofu yangu ipo kwa Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutokana na hatua tunazochukua juu ya kukabiliana na suala hili. Kusema kweli bado hatujachukua hatua za kuridhisha na kuonesha u-*serious* wetu kama tunavyokuwa *serious* katika kupambana na majanga mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano; yakitokea maradhi ya kuambukiza nchi za jirani utakuta ghafla Serikali inaanza kuchukua jitihada za kufunga mipaka kuzuia wageni kuingia katika nchi hizi ambazo wageni wanatoka katika nchi ambazo zinasadikika kuwa na maradhi hayo. Lakini hali iko tofauti katika suala hili la ushoga. Changamoto tunazozikuta kutokana na suala hili, sisi tuliopitiwa na majimbo ambayo yamezungukwa na utalii ni kubwa mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani, na ni muumini wa kila siku; Tanzania tumekuwa na sheria nyingi zinazoweza kutosheleza kukabiliana na hali hii ya ushoga. Lakini changamoto inakuja katika suala zima la usimamiaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili ninapenda nitoe mfano, Jimbo langu la Nungwi ni jimbo la kitalii na ilivyojengeka au ilivyoaminika ni kwamba sehemu kubwa zinazoendesha biashara hizi za ushoga, za ndoa za kiume, ni sehemu ambazo zimepitiwa na sekta ya utalii. Kinachonihuzunisha, unaweza kuwakuta maaskari wanatoka nje ya Nungwi, wanatoka sehemu tofauti na Zanzibar kukiwa kuna sherehe au hali yoyote katika mazingira ya Nungwi unaweza ukakuta maaskari wapo wengi wanakuja kwa ajili ya kutunza mazingira ya pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha kusikitisha ni kwamba badala ya kwenda kufanya doria katika matukio waliopangiwa wale maaskari unaweza kuwakuta maaskari wamekwenda kuzongea na kuwanyang'anya waendesha bodaboda bodaboda zao na kuzipeleka kituo cha polisi kwa ajili ya mazungumzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachonisikitisha maana ya hiki ninachokizungumza kinatuweka na masuala mawili mazito. Inawezekana kwa Tanzania yetu ya kileo suala la waendesha bodaboda kukosa *helmet* likaonekana kwamba lina athari kubwa zaidi kuliko suala la ushoga.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nilikusudia nieleze kuhusiana na hatua ambazo Serikali kwa ujumla wake imechukua kuhusiana na changamoto hii ambayo Waheshimiwa Wabunge wameizungumza kwenye hotuba ya bajeti yangu kwa kirefu, lakini naona huu ni mchango takribani wa pili umekuwa ukiishutumu Serikali juu ya hii kadhia ambayo inaendelea duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ambayo nataka kutoa ni kwamba kwanza, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali kupitia kauli mbalimbali za viongozi wetu kuanzia Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, mara kadhaa wamelizungumzia na wameonesha hisia zao na hasira juu ya matatizo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna hatua ambazo tunachukua kama Serikali, zinaratibiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, atakuja kueleza mwenyewe. Lakini kwa upande wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ikiwa kama Wizara ambayo inasimamia usalama wa nchi hii na utekelezaji wa sheria hizo, kuna mambo mengi ambayo tumeyafanya ya kimkakati. Hofu yangu ni kwamba Waheshimiwa Wabunge wasidhani kwamba Serikali haichukui hatua kwenye jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi; kuna masuala ambayo yanahusu usimamizi wa sheria kwa upande wa Jeshi la Polisi, kuna watu wengi ambao wanahusika katika mambo kama haya wameshachukuliwa hatua mbalimbali, na wengine wapo katika uchunguzi. Kuna hatua za kiuhamiaji kwa wale ambao wanajihusisha na masuala haya wanaotoka nje ya nchi kupitia taasisi mbalimbali, hatua hizo za kiuhamiaji vilevile zimeshachukuliwa za kiuhamiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hatua za kitaasisi kupitia taasisi mbalimbali ama jumuiya zinazojishughulisha na mambo haya, tunashirikiana vizuri na Mheshimiwa Waziri, Dkt. Gwajima, ambaye anasimamia *NGOs* na mimi nasimamia jumuiya za kiraia, kushughulika na taasisi na jumuiya hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hatua ziko nyingi sana. Niombe Waheshimiwa Wabunge pale ambapo nitakuja kusoma hotuba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi tutaeleza kwa kina.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, waelewe tu kwamba Serikali iko *very serious* na tatizo hili na hatua nyingi zinachukuliwa na pongezi kwa jitihada zao ambazo wanaendelea.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Simai, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuchangia hoja yangu; naipokea taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuendelea, maaskari wamekuwa waki-*deal* zaidi na waendesha bodaboda, kitu ambacho kinawapa hofu Watanzania juu ya ukubwa wa waendesha bodaboda kukosa *helmet* na suala la ushoga. Kitu kinachotia hofu zaidi ni kwamba hivi kuna ugomvi gani baina ya vijana wetu wa bodaboda na maaskari polisi? Lakini hivi kuna uswahiba gani uliopo kati ya baadhi ya maaskari na wale wanaojihusisha na vitendo vya ushoga? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ni maisha, tuwasome kisha tuwasomeshe kwa vizazi vyetu. Mwanadamu amekuwa akinywa pombe zaidi kuliko maji safi na salama kwa afya yake. Mwanadamu amekuwa akiwatupa na kuwatelekeza viumbe ambao amevizaa yeye mwenyewe wakati kuku na bata wanaendelea na utaratibu wao uleule wa kuwalea na kuwa na mapenzi kwa watoto wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanadamu wamekuwa na tabia ya kutaka kuzaa na wale waliowazaa au watakaowazaa lakini simba wanaendelea na utaratibu wa kuwafukuza watoto wao wanapofikia umri wa balehe na kuwataka waende wakajitegemee ili kuepusha tu kuzaa na wazazi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi sote hapa ni wazazi, sote ni walezi na sote tuna familia. Mzazi na mlezi wa kweli ni yule anayeguswa na changamoto za mtoto wa mwenzake. Katika hili wanyama tangu walipoumbwa hawajawahi

kubadilisha tabia zao lakini binadamu tumebadilika na kuwa na tabia za kinyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mashekhe, mapadre, wanaendelea kupaza sauti kukemea ushoga na vitendo hivi vinavyoambatana na mambo hayo, Serikali iko bize zaidi katika kukusanya mapato na tozo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukijifanya hatuyaoni haya, tunayafumbia macho, badala yake tukiacha kudumisha mila na kuendekeza nguvu zaidi katika kukusanya mapato kwa wahisani na wawekezaji ambao baadhi yao hawana tija.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya miaka michache tutakuwa na chanzo kipya cha kukusanya mapato kupitia mashoga.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, taarifa hiyo iwe fupi tafadhali.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba tumekuwa tukipigana vita kubwa sana katika kuhakikisha tunatunza maadili ya nchi hii na vizazi vyetu; tumekuwa tukiongea sana. Jambo ambalo nimeliona ni kwamba ufuatiliaji wa nini Serikali inafanya kwa Watanzania wengi na wawakilishi wao siyo mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeimba mpaka nyimbo za *don't touch here, here and there* kama vile tunachekesha, ni kupeleka hamasa hiyo, tumetengeneza SMAUJATA, Jeshi la

Jamii la Wazalendo, wako kule wanafanya maandamano… Kilimanjaro jana…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yote hiyo ni kuamsha, na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imepeleka barua kwamba *agenda* hii iwe ya kudumu kwenye mabaraza yetu ya halmashauri ya Madiwani na Kata.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachangia.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Simai, endelea na mchango wako.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningelipenda niendelee na hoja yangu nakusisitiza kwamba kama tutaendelea kuwa *busy* zaidi katika masuala ya kukusanya mapato kuliko ku-*deal* na mila na desturi za Kitanzania basi tujiandae Watanzania kuwa na chanzo kipya cha kukusanya mapato kupitia mashoga kwa sababu kasi ya ushoga inaongezeka kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile maana ya …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ahsante muda wako umeisha malizia. Ahsante sana Mheshimiwa Sumayi.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Venant Daud Protas atafuatiwa na Mheshimiwa haji, Mheshimiwa Rashid Abdalla ajiandae.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi kuwa mmoja wa wachangiaji katika ofisi ya Waziri Mkuu katika bajeti ya mwaka 2023/2024.

Kwanza mimi niwaombe Waheshimiwa Mawaziri, mna muda mzuri sana wa kujibu hoja za Wabunge, kwa hiyo tupunguze miongozo. Tumekuja humu kuleta kero na matatizo ya wananchi na ninyi kazi yenu ni kutatua kero na matatizo ya wananchi tunawategemea katika hilo, sasa anaposema Mbunge na nanyi mnanyanyuka mnakuwa mnatuingilia *Hansard* hazikai sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze kwa mchango wangu nategemea mimi sipati mwongozo mpaka namaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kupongeza Serikali kwa kazi nzuri inayoifanya kwa kuwahakikishia wananchi kuwaletea maendelea. Leo tunapozungumza hapa ukiangalia Serikali zote zilizo pita Serikali ya Awamu ya Sita imevunja rekodi kwa kuleta maendeleo chapu chapu; na sisi viongozi au Wabunge wapya tulioingia mwaka huu tumepata mserereko mkubwa sana, kwa sababu kila kitu tulichokisema kimekwenda. Uiangalia jimbo langu ahadi zote

tumemaliza isipokuwa kuna ahadi chache chache tu, na hizo ahadi itabidi niziseme leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kupongeza Serikali, kwanza mimi nishukuru Serikali, tuna mradi mkubwa wa *SGR* ambapo takriban asilimia 70 au 80 ya Mradi wa Makotopora - Tabora umepita Jimbo la Igalula; hapa ninaombi kidogo kwa Mheshimiwa Waziri Mbalawa. Kuna wananchi ambao reli imewafuata na kuna wanachi ambao wameifuata. Mimi nikuombe, wale wananchi ambao waliifuata reli, wakazi wa kata ya Nsololo na mmoja ambaye ana athirika kwa kubomolewa nyumba yake anataka asilipwe alikuwa mgombea mwenzangu, wa Ubunge wa *ACT*. Kwa kuwa Mheshimiwa Rais ameweka maridhiano, mimi naomba, kwa sababu wale watu walijenga zaidi ya miaka 20,30 iliyopita basi muwafikirie kuwalipa hata fidia kidogo, basi msiwabomolee na kuwaacha hivyo hivyo. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri Mbalawa katika bajeti hii hao wananchi 20 ambao hawajaingizwa kwenye fidia naomba waingizwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema hapa Mheshimiwa Rais amefanya kazi nzuri na yenye mfano katika vipindi vyote vya marais. Na mimi nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu; anazunguka nchi hii kwenda kuwatia matumaini wananchi kwa kile kinachofanywa na Serikali; na Mheshimiwa Waziri Mkuu inawezekana kuna muda unapiga kazi mpaka watu wanakuhisi hisi mimi nikuhakikishie piga kazi na sisi kama wawakilishi wa wananchi tuko nyuma yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sisi wawakilishi wa wananchi; ndio hicho nilichosema wananchi mnatakiwa mtujibu hoja, tunapokuja humu tunawaambia Mawaziri kuna changamoto katika majimbo yetu, Waziri anakuahidi tunakwenda jimboni kwa lengo la kwenda kutatua kero na sio kuongeza kero nyingine. Hii lazima tuikemee. Kumekuwa na Waziri tunakwenda nao kwenye majimbo wanakwenda kutuletea matatizo badala ya kutatua matatizo.

Wanakwenda kuahidi vitu ambavyo haviwezi kutekelezeka, mnatuachia kero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mimi nina ahadi za tangu Mbunge Mfutakamba Jimbo la Igalula hamjapeleka, akaja Musa Ntimizi hamjapeleka, nimekuja mimi mmenipiga fiksi tena, nimekaribia kumaliza muda wangu hamtapeleka. Mimi niwaombe kama kitu hakiwezekani tusiwalaghai wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivi kwa sababu Mheshimiwa Jafo alikwenda mwaka 2019 katika Kata ya Igalula akawaambia wananchi; yaani mimi nikienda tu Dar es Salaam hii wodi yenu nitaimaliza nitaleta shilingi milioni 80, mpaka leo milioni 80 haijaenda; mpaka Jafo amehama Wizara sijui nane sijui ngapi, mpaka leo. Sasa wa kumdai ni nani? Ni akina nani wanao ratibu ahadi za viongozi? Sasa ninyi mnakwenda na msafara mkubwa halafu hamfanyi chochote; sasa mna maana gani ya Kwenda? Mheshimiwa Waziri Mkuu nimekusifia hapa lakini na wewe uliacha deni huko. Kuna shilingi milioni 80 katika Kijiji cha Imalakaseko, ulikwenda na jiwe lako la kumbukumbu liko pale, haijaenda tangu mwaka 2017. Ulikuja na msafara, una Katibu na nani, Dereva, nani mpaka leo haijaenda; sasa walienda kufanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaomba ili tuwape hadhi viongozi wetu wa kitaifa wanapokuja kwenye majimbo yetu msituletee matatizo mengine. Sasa wanakuja kutuambia wewe Mbunge tulikwambia upeleke kero yetu.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Nani tena huyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Venance kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Maganga.

**T A A R I F A**

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nataka nimpe taarifa Mheshimiwa, kwamba mchango wake ni mzuri sana, kweli anaongea vya ukweli kabisa. Ni kweli, unaweza ukapata wageni lakini baadaye wakakuletea matatizo makubwa. Kwa hiyo naomba Serikali ichukue mchango wake maana yapo majimbo mengi viongozi wakiwemo mawaziri wameingia kwenye majimbo yetu na kutuachia ahadi na hazitekelezeki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maganga, ahsante. Mheshimiwa Venant taarifa unaipokea?

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ninaipokea, ndiyo haya matatizo ambayo tunayazungumza. Halafu mbaya zaidi mnampiga fiksi mpaka kiongozi wa Kitaifa. Mheshimiwa Rais alikuja ziara mwaka jana katika Mkoa wetu wa Tabora, alisimama katika Kata ya Kigwa. Mimi mwakilishi wao nikamwambia Mheshimiwa Rais tuna changamoto ya umaliziaji wa maji ya Ziwa Victoria katika kata ya Gowekwe, Igalula na Nsololo na Kigwa akamsimamisha Mheshimiwa Waziri wa Maji. Waziri akaniambia Mheshimiwa Rais hilo limeisha, mwezi wa 12 Maji watayapata hapa; mpaka leo hata dalili hakuna. Sasa wananchi wanachanganyikiwa sasa mpaka Rais anapigwa fiksi sasa sisi ni akina nani, sasa Mwenyekiti…

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Athuman Almas Maige.

**T A A R I F A**

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili analoliongelea pacha wangu wa Igalula nami nililiongelea. Marais watatu wana ahadi ya kituo cha afya Uyuwi, Tabora Kaskazini, mpaka leo mwaka wa tano.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Venant, taariifa hiyo unaipokea.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea hiyo taarifa. Kwa hiyo CAG anapokagua fedha kupotea hata hizi ahadi akague. Awakague viongozi ambao wanachimba mashimo kwa wananchi ili sasa tuwe na Serikali ambayo ni yenye matumaini kwa wananchi na si Serikali yenye mashaka kwa wananchi. Kwa hiyo mimi nilitaka nichangie katika hoja hiyo ahadi za viongozi zifuatiliwe.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Venant, ahsante muda wako umeisha.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kengele ya kwanza, au imeisha hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Haji Amour Haji atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Abdalla Rashid, Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani ajiandae.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuweza kunipa nafasi na mimi niweze kuongea machache kujaribu kuzungumzia hotuba ya Waziri Mkuu.

Kwanza napenda kuishukuru Serikali yangu kwa kazi kubwa ambayo wameifanya, na katika moja ya kazi ambazo wamefanya; nimejaribu kuangalia miradi ambayo ni miradi mikubwa sana ambayo imezungumzwa katika taarifa ya Waziri Mkuu; kwamba kuna miradi takriban saba ambayo imetumia fedha nyingi sana; na fedha hizo ni kweli nitasema kwamba ni pesa ambazo kwa kiasi fulani tujipe moyo Tanzania inasonga mbele. Kama alivyozungumza Rais wetu mpendwa mama Samia Suluhu Hassan kazi iendelee, kweli kazi inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejaribu kufanya ziara na Kamati yangu ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, tumepita miradi kadhaa. Ndani ya nchi hii kuna vitu ambavyo vinafanywa ni vikubwa sana; na hii inaonesha uhalisia kwamba nchi yetu inapiga hatua na uchumi unaweza ukakua kwa kiasi fulani. Hata hivyo, kwenye miradi hii ningependa pengine kuishauri Serikali; miradi ni mikubwa lakini kitu muhimu zaidi ni kuweza kujua namna na adhma ya ile miradi yetu. Lengo ni kuhakikisha uchumi wa nchi unakua.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Serikali ilipojenga reli ya *Standard gauge* ilikuwa na dhima maalum. Maana yake ni kwamba tukimaliza ujenzi wa reli hiyo tujue adhma ya Serikali ni kitu gani pamoja na miradi yote ambayo ilikuwepo, ikiwemo ya meli na miradi mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nije katika mchango wangu kuhusiana na taarifa ya Bajeti ya Waziri Mkuu, nijaribu kugusia taasisi moja ambayo inahusiana na masuala ya Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania *(TaESA)*. Hii taasisi kwa kweli inafanya kazi zake kubwa sana kwa mujibu ambavyo

ilivyo na *objective* zake zilivyo au malengo yake yalivyo, lakini shida ambayo iliyokuwepo ni kwamba *TaESA* ni kama ni *agency;* tunasema kwamba imemeza kila kitu. Tukiangalia katika hali ya sasa kwa dunia hii ya leo *TaESA* mimi nadhani kungelikuwa na uwezekano tukawa na kamisheni itakuwa inafanya uratibu wa shughuli hizo. Baadhi ya shughuli za *TaESA* tuwaachie mawakala wa ajira ili kuhakikisha kwamba tunaleta muunganiko mzuri katika masuala ya uajiri; na hii inakuja kwa sababu ya mtazamo wa kidunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtazamo wa kidunia ni mpana sana. Mtazamo wa kidunia hasa katika suala la soko la ajira limekuwa la pembe tatu. Kuna suala la mawakala wa ajira, kuna suala la muajiri pamoja na yule anayeajiriwa, sasa ili kuweza kupata ajira maana yake ni lazima uanze kwa wakala wa ajira twende kwa mwajiri pamoja na yule *candidate* kuweza kufikiwa katika shughuli zake. Kwa sasa hivi inakuwa kama kuna *monopolize* ya hili soko, maana hata hao mawakala wa ajira waliokuwepo katika Taifa letu hili la Tanzania wanafanya, kisheria, kama ni *brokers* kwa sababu wale sio mawakala hasa. Kwa sababu wao watafute ajira au watafute kazi kisha wazipeleke kwa *TaESA* ambapo TaESA ndiye atakayeweza kuhakikisha kwamba mtu yule anapatiwa ajira kwa namna gani na hususani katika ajira ambazo ni za nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili mimi pengine ningeshauri Wizara, ili kuwe na ufanisi mzuri na mkubwa zaidi katika hii taasisi ambayo inahusiana na masuala ya ajira iache baadhi ya *loop hole* kwa upande wa mawakala wa ajira. Hii ni kwa sababu sasa hivi kidunia tumesaini mikataba *(conventions)* mbalimbali ya kimataifa zinazohuaiana na *labour,* ambayo ni lazima tuifuate. Kuna mashirika kwa mfano kama *A.I.O, I.O.M* ambayo yanahusiana na masuala ya uhamiaji, wale wote wanatakiwa kuratibiwa

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri zaidi kila mhamiaji anapokuja, anapotafuta nafasi ya ajira apitie kwa wakala maalum ambaye ndiye ataweza kumpatia nafasi ya ajira. Sasa kazi ya taasisi inayoshughulika na ajira maana yake ifanye kazi ya *coordinate* na kuchukua *data* kupitia kwa wale mawakala. Nadhani kwamba inaweza ikafanyika kazi nzuri zaidi na hii inakuja hata kwenye vibali vya ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutasema tuna vibali *almost* 8,576 vya kazi, vibali vile ndizo kazi zenyewe za watu wetu ambazo wamepatiwa watu wa nje. Tusiseme kwamba tumepata vibali vingi, kwamba sasa vimetuongezea mapato, tujaribu kuangalia kwa upande wa pili; kwamba zile ni ajira za watu wetu kwamba sasa wamepatiwa ajira watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili suala ili kuwe na ufanisi kwa suala la ajira na kusiwe na ule ulegevu ambao; kama kuna Mbunge mwenzangu mmoja alizungumza jana; kwamba imekuwa kama *TaESA* haina meno, shida yenyewe ni kwamba taasisi ya *TaESA* ilivyozinduliwa kwa wakati ule ilikuwa kuna haja hiyo. Hata hivyo kwa wakati ambao tunao kwa sasa hivi ni wakati ambao unakwenda katika sayansi na teknolojia, hivyo lazima kuna baadhi ya mambo wajipunguzie ili kuweza kwenda katika hali ya usawa, vinginevyo siku zote ajira zitakuwa zina shida; lakini kama zitakuwa zinapitia katika mlengo wa kimawakala kwenda kwa waajiri ingekuwa ni vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na lingine ambalo naweza kulizungumza ni kwamba *TaESA* kama ni mawakala ni vizuri zaidi kila baada ya mwaka wakatengeneza kitu kinaitwa *career fare;* ambacho kitakuwa kinakusanya mawakala, waajiri pamoja na *candidate* kwa mujibu wa fani zao walizo nazo. Sasa kama mwajiri atakuwa anahitaji mfanya kazi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, shukrani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Abdalla Rashid atafuatiwa na Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani.

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii na mimi leo niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu. Kwanza na mimi niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwatumikia wananchi; lakini hii ni moja kati ya kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kadhalika nimpongeze Mheshimiwa Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi naye kwa kazi kubwa anayoifanya ya kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu kuhusiana na hotuba hii ya Waziri Mkuu kwa kuanza na *TASAF*. Kwanza nishukuru Serikali kwa kazi kubwa iliyofanya katika jimbo langu la kuniletea shilingi milioni 475 kwa ujenzi wa kituo kikubwa cha daraja la pili, kitu ambacho kitawasaidia wananchi wa Jimbo la Kiwani pamoja na jimbo jirani. Kituo hiki kilipata baraka kubwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kuweka jiwe la msingi lakini na Mheshimiwa Makamo wa Rais Dkt. Mpango kwenda kukifungua. Hata hivyo, changamoto kubwa ya kituo hiki kwa sasa ambayo wananchi tunakabiliana nacho ni vifaa tiba, wakati Makamo wa Rais anafungua kituo kile aliagiza kwamba vifaa tiba kwenye kituo kile vipatikane ili lile lengo la Serikali la kujenga kituo kile na wananchi kupata huduma liweze kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Waziri ambaye anahusika, kwamba sasa hivi vitu ambavyo tunahitaji pale kituoni ni *ultra sound X-ray* pamoja na kile kiti cha meno, tukianza hivyo vitu kile kituo kitafanya kazi na wananchi

wataweza kunufaika na kile kituo na zile ahadi ambazo tuliziweka za kuimarisha huduma za afya tutakuwa tumeweza kuzitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande huo huo wa *TASAF* nishukuru huu mpango wa ajira za muda ambao ni programu maalum iliyotekelezwa na *TASAF* ya kuwapatia wananchi wetu ajira za muda lakini sambamba na kutengeneza miundo mbinu ya barabara kwa kiwango cha udongo. Hata hivyo hapa napo kuna changamoto ndogo ambayo napenda *TASAF* kwa mara nyingine waweze kuongeza bajeti ili zile kazi ziweze kufanikiwa na kuleta ufanisi wa hali ya juu na zile fedha ambazo zimetumika kwa kuwalipa wananchi ziweze kufanya kazi inavyopaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwa upande wa mazingira pia nishukuru Serikali hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutupatia mradi mmoja mkubwa sana wa shilingi zaidi ya bilioni moja na nusu za ujenzi wa tuta la kuzuia maji ya chumvi katika jimbo langu na jimbo jirani la Mtambile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kazi ni kubwa na kazi hii kwa kweli lazima tushukuru kwamba imewasaidia sana wananchi na wanafunzi ambao walikuwa wanatumia kivuko cha maji, lakini sasa tunapata daraja hili la kuzuia maji lakini kadhalika tunapata njia za kutumia. Nishukuru kwa kuleta fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Wizara wa Mambo ya Ndani, nishukuru kwamba tumepiga kelele hapa na nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri alifanya ziara kwenye Kituo cha Polisi Kengeja na juzi katika kujibu swali hapa alituahidi kwamba tayari wameshatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo kile. Haya yatakuwa ni mapinduzi makubwa kwenye kituo kile ambacho kilijengwa tangu enzi za wakoloni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije katika suala la zima hili la habari ushoga. Suala hili ilikuwa niseme kwamba, mpango ule wa akinamama wajawazito kuwa ni lazima kupimwa ni mpango mzuri na umeleta matokeo mazuri sana na mafanikio makubwa yamepatikana. Ninachoomba sasa, sisi tunapiga kelele sana juu ya jambo hili, lakini ninachosema kama kuna taratibu za sheria, kanuni kwamba Bunge liamue sasa kwanza Wabunge wote wapimwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakipimwa hawa Wabunge tutaweza kujua kwamba Wabunge sasa tunatoka tunakwenda kufanya kazi hii ya kuhakikisha tunawalinda wananchi wetu baada ya sisi kuwa tumeshatangulia kupimwa. Sasa kama humu wamo, tunajua kwamba wale watu wa unga kulikuwa kuna *Sober house* wanaweka na kama humu ndani watakuwa wamo Wasenge na Wasagaji, nao sasa iwepo namna ya kuhakikisha kwamba tunawaweka kwenye *Sober house*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tusikilizane. Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, naomba tujaribu kutumia lugha za kistaha kwenye Bunge letu tafadhari sana.

Haya Mchangiaji wa Mwisho ni Mheshimiwa Ahmed Katani.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kukushukuru sana. Nitakuwa na mambo mawili tu; moja hili ambalo mzungumzaji aliyemaliza kuchangia amezungumza, lakini la pili pia linahusiana na hili hili tunalolisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu ya Maendeleo ya Jamii, tunao Maafisa Ustawi wa Jamii wako mtaani kule, leo

kumetokea changamoto hii kubwa ya tatizo, hili janga la kitaifa, maana hili limeshakuwa janga la kitaifa. Vile vile tuna wanafunzi waliohitimu elimu ya ustawi wa jamii na ni wataalam wamezagaa mtaani. Hivi vitendo vinavyozungumzwa mchangiaji amezungumza vizuri sana na Mwenyekiti umeshauri tuzungumze kwa stara. Haya mambo ni ya mtambuka, kuna haya tunayoyaona kwa macho, yapo tusiyoyaona kwa macho na yanafanywa majumbani kwetu. Ndiyo maana mchangiaji akashauri hapa ikiwezekana maana utaratibu wa Jeshini watu wakienda wanapimwa. Vile vile na sisi ni wawakilishi wa wananchi lazima tupimwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni wawakilishi wa wananchi na ni lazima tuwe kioo cha jamii. Sasa hatuwezi kuwa kioo cha jamii kuna watu wanakuja hapa kumbe wanashughulikiwa, itakuwa sio sawa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jambo hili Mama Masaburi alikuwa anachangia pale, akawa ananukuu vitabu vya Mungu…

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Katani, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kunti Majala.

**T A A R I F A**

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Napenda kumpa tu taarifa Mheshimiwa Katani kwamba suala la Wabunge sisi kupimwa naamini halishindikani na Bunge limekuwa na tabia ya kutuletea Madaktari kwa ajili ya ku-*check* afya zetu. Sasa naamini wiki ijayo kuanzia Jumatatu litafanyika hilo, Wabunge wote wataletwa Madaktari hapa tutaanza kupimwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Katani, taarifa unaipokea?

**MHE. KATANI A. KATANI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hiyo na Waziri mwenye dhamana ya Wizara ya Afya yupo, nikuombe sana dada yangu kwenye jambo hili tuwe *serious.*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Katani kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hili jambo nampa taarifa mzungumzaji kwamba tunalichukulia kama mzaha na Watanzania wanaangalia Bunge *live*. Tukizungumza mambo ya ufisadi watu tuna-*concetrate* kusikiliza, sasa tukizungumza suala la Wasenge linakuwa kama ni utani. Hata hiyo, nampa taarifa mzungumzaji kwamba nchi yetu imepitia majaribio mengi sana. Tulikuwa na jaribio la Kibiti na Lindi, Serikali ilishughulika likaisha, tumepata la *Corona,* Serikali imeshughulika limeisha wala hatukujadili humu, tuliwaachia wataalam, tumepata janga juzi la mwisho la panya *road,* leo hawapo. Sasa hili lina ugumu gani kulimaliza kimya kimya kuliko kulileta Bungeni? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa unaipokea?

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa naipokea, lakini nadhani anatoa maelekezo kwa Waziri Mkuu, ninavyohisi wala hanipi mimi taarifa hiyo, maana anasema washughulikie huko Serikali. Sasa kwa sababu mimi sio Serikali mimi ni upande wa Bunge, sisi tunatunga Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema dada yangu Mheshimiwa Ummy yupo hapa na naamini tunavyo vifaa vya kutosha. Kunti ameshauri jambo jema sana, tusisubiri subiri hapa wamezungumza mambo ya supu ya mbwa inanywewa ikiwa ya moto. Hili jambo tusisubiri subiri, Mama kama wataalamu wapo waje hata kesho shughuli ianze.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Katani endelea, muda umekwenda.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama Masaburi pale kumbe vitabu vya dini hivi viko sawasawa sana. Mama alikuwa anakumbusha kitabu cha Lutu ambacho na sisi kwenye Quran ipo. Sura ya 11, surat Hud ukienda aya ya 82 watu wa Lutu walishatolewa hukumu ya kuuawa, walawiti wale nchi ilipinduliwa kukawa na vitu kama mawe kwenye *Quran*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna hadithi hapa sahihi kabisa ya Mtume Muhammad *(S.A.W) "Raawu Imam Abu Dawud an ibn Abbas qala; qala Rasulu Allah, Swala-Allah Alayh Wasallam, idhaa raaytum man yaf-al amara kaumi Luutwi faktulu fa'ila walmafuula bih*." Imepokewa na Imamu Abu Daud kutoka kwa Ibn Abbas amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa sisi Waislamu ni hadithi sahihi; mtakayemkuta anafanya kitendo cha watu wa Lutwi, ulawiti, kuingiliana kinyume na utaratibu, vitabu vyote kila kiungo cha mwanadamu kimetengenezwa kwa ajili ya kazi maalum. Binadamu sisi tumekuwa wanyama unakwenda kufanya jambo kwenye sehemu ambayo ya kutolea uchafu wa mwanadamu. Hii ni dhambi, watu hawa wameamuliwa kuuawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Bunge tunayo nafasi kubwa, tunaogopa nini? Ndio misaada inayosemwa? Yaani

Taifa liangamie kwa kuogopa misaada ya wafadhili? Wanaoleta hizi taasisi za watu wa kufanya mambo ya hovyo wapo mtaani. Watu hawa tutunge sheria hapa. Uganda wamefanya mfano pale miaka 10 sisi tusisite. Sheria zilikwishatungwa toka mwanzo, alete sheria hapa Waziri mwenye dhamana tupitishe sheria hapa. Ili watu wakome ni kunyongwa tu. Tukisema wanyongwe tu, hakuna mtu atachezea chezea, hakuna mtu atacheza huu mchezo na hata majumbani huku ndio maana tukasema tupimane hapa, wanaume kwa wanawake tupimane. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo kama Bunge lazima tuone kwamba tuko *serious,* Taifa haliwezi kupotea hivi. Hii ni nguvu kazi, tusipoanza sisi kwenda kuwaambia wananchi huko wapime itakuwa shida. Ilikuja *corona* hapa ilikuwa ni lazima, huwezi kusafiri bila kupima *corona* na sisi Wabunge huwezi kuingia ndani kama hukupima, tutapima wote hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa aya nzuri sana, kila kiungo kina matumizi yake, sio wanaume tu hata wanawake wanaoshughulikiwa huko na wenyewe wapimwe tu, maana kila kitu kimewekwa kwa uhalali wake, ndio maana nikasema mlangoni pale dada yangu Mheshimiwa Ummy alete wataalam na wakiletwa wataalam ili tuingie humu kila mtu atapima.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Katani, ahsante sana muda wako umeisha.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, ratiba yetu ya jioni imefika mwisho, orodha ya wachangiaji kwa leo imekamilika.

Niwakumbushe tu kwamba leo jioni Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameandaa futari kwenye viwanja vya Bunge, kwa hiyo kuanzia saa kumi na mbili na nusu tusogee maeneo hayo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, basi baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 12.08 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamis, Tarehe 13 Aprili, 2023, Saa Tatu Asubuhi)*